ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR
MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Rashid Seif Suleiman	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ziwani.
9.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge
10.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa

11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa
12.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Gando
13.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Kuteuliwa.
14.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Jang'ombe
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la Makunduchi
18. Mhe. Shawana Bukheti Hassan	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/ Jimbo la Dole
19. Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu

22.Mhe. Issa Haji Ussi	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka
23.Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake
29. Mhe. Mohammed Said Mohammed	Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi/ Jimbo la Mpendae
30.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
31.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
32. Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa
33.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
34.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini
35. Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
36.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake

37. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
38.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
40.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
42.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
43.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
44.Mhe. Hamad Masoud Hamad	Jimbo la Ole
45.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
46.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
47.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
48.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu	Jimbo la Bububu
49.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
50.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
51.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
52.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Jimbo la Kikwajuni
53.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
54.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	Jimbo la Kiembesamaki
55.Mhe. Marina Joel Thomas	Kateuliwa na Rais
56.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa	Jimbo la Mkwajuni
57.Mhe. Mgeni Hassan Juma	Nafasi za Wanawake
58.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma	Jimbo la Bumbwini

59.Mhe. Mohammed Haji Khalid Jimbo la Mtambile

60.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad Jimbo la Chambani

61.Mhe. Mussa Ali Hassan Jimbo la Koani

62.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali Jimbo la Uzini

63.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa Nafasi za Wanawake

64.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi Nafasi za Wanawake

65.Mhe. Nassor Salim Ali Jimbo la Rahaleo

66.Mhe. Omar Ali Shehe Jimbo la Chake-Chake

67.Mhe. Panya Ali Abdalla Nafasi za Wanawake

68.Mhe. Raya Suleiman Hamad Nafasi za Wanawake

69.Mhe. Rufai Said Rufai Jimbo la Tumbe

70.Mhe. Saleh Nassor Juma Jimbo la Wawi

71.Mhe. Salim Abdalla Hamad Jimbo la Mtambwe

72.Mhe. Salma Mohammed Ali Nafasi za Wanawake

73.Mhe. Salma Mussa Bilali Nafasi za Wanawake

74.Mhe. Salmin Awadh Salmin Jimbo la Magomeni

75.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman Nafasi za Wanawake

76.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha Jimbo la Mwanakwerekwe
77.Mhe. Subeit Khamis Faki Jimbo la Micheweni
78.Mhe. Suleiman Hemed Khamis Jimbo la Konde
79.Mhe. Ussi Jecha Simai Jimbo la Chaani
80.Mhe. Viwe Khamis Abdalla Nafasi za Wanawake
81.Mhe. Wanu Hafidh Ameir Nafasi za Wanawake

Ndugu Yahya Khamis Hamad Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Tisa - Tarehe 26 Juni, 2013

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi

DUA

Mhe.Naibu Spika: (Ali Abdalla Ali) alisoma Dua

HATI ZA KUWASILISHWA MEZANI

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha Hati Mezani kuhusu Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa Mwaka 2013/2014.

Mhe. Shadya Mohamed Suleiman (Kny: Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa): Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha Hati Mezani ya Maoni ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kuhusu Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa mwaka 2013/2014. Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha. (*Makofi*).

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 81

Motisha kwa Vijana Wanaoshiriki Polisi Jamii

Mhe. Saleh Nassor Juma - Aliuliza**:-**

Kwa kuwa Jeshi la Polisi kupitia Makamanda wake wa Mikoa na Wilaya kwa kushirikiana na ulinzi shirikishi (polisi jamii) wamefanya kazi nzuri kwa kuweza kupunguza uhalifu, wizi pamoja na ngono zembe katika maeneo mengi ya Unguja na Pemba. Na kwa kuwa hawa vijana wetu wa Polisi jamii wamekuwa wakijituma na kujitolea muda wao mwingi. Je, serikali huwa angalau inatoa shukurani na motisha kwa vijana hawa.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais - Alijibu**:-**

Mhe. Naibu Spika**,** kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, kabla ya kumjibu Mhe. Saleh Nassor Juma swali lake nambari 81 naomba kutoa maelezo kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika**,** ni kweli Jeshi la Polisi kupitia Makamanda wake wa Mikoa na Wilaya kwa kushirikiana na walinzi shirikishi (Polisi jamii) wamefanya kazi nzuri kwa kuweza kupunguza uhalifu, wizi pamoja na ngono zembe katika maeneo mengi ya Unguja na Pemba.

Mhe. Naibu Spika**,** kwa niaba ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar napenda kutoa shukurani kwa jeshi la Polisi kwa ubunifu wao ulileta mafanikio makubwa katika ulinzi shirikishi (Polisi jamii), kadhalika shukurani za pekee ziwafikie wananchi wote waliokubali na kushiriki katika kazi ya ulinzi wa maeneo yao jambo ambalo kwa kiasi kikubwa limepunguza uhalifu nchini.

Mhe. Naibu Spika**,** Serikali inaelewa umuhimu wa kusaidia vikundi vya Polisi Jamii na itaendelea kuunga mkono vikundi hivyo kwa kutoa vivutio mbali mbali vitakavyohamasisha utendaji wa kazi zao.

Mhe. Naibu Spika, hivi karibuni Serikali kwa kupitia Kamishna wa Polisi Zanzibar imetoa Shilingi 1,000,000/= kwa polisi jamii wa Jimbo la Mji Mkongwe na Shilingi 1,000,000/= kwa Shehia ya Ngombeni Kijiji cha Jondeni Pemba. Aidha, kikundi cha Shehia ya Chambani Mkoa wa Kusini Pemba kimepatiwa mifuko 90 ya saruji na kikundi cha Shehia ya Kianga kimepatiwa mashine moja ya kufyatulia matofali. Kadhalika Shehia moja kwa kila Wilaya ya Unguja na Pemba imekabidhiwa baiskeli moja kwa ajili ya kikundi cha Polisi Jamii. Hata hivyo Serikali itaendelea kuunga mkono jitihada hizo kwa kadri uwezo wa kifedha utavyoruhusu.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri mdogo wangu hapa naomba kumuuliza swali dogo tu la nyongeza kama ifuatavyo:

Kwa kuwa katika swali langu la msingi nimesema kwamba hawa vijana wa Polisi Jamii wamesaidia sana pamoja na kupunguza mambo ya uhalifu, lakini hata kupunguza mambo ya ngono zembe ambazo mara nyingi huwa zinatokea katika maeneo pembezoni mwa bahari, vichakani humo na hata katika vigesti uchwara. Kwa kuwa huwa vijana wamepunguza sana kupunguza ngono zembe ambazo ndio chanzo cha mambo ya Ukimwi katika nchi hii.

(a) Je, anaonaje lile fungu ambalo Waheshimiwa jana wakibisha waliokuwa wanasema kwamba hili linapelekwa katika mambo ya Ukimwi halitumiki hili fungu hili. Je, unaonaje asilimia 50 ya fungu lile wakasaidiwa Polisi Jamii ili wakaweza kufanya kazi vizuri ya kuzuia ngono zembe pamoja na uhalifu katika vijiji vyetu.

(b) Kwanza napenda niipongeze Serikali kwa hili kwamba wametoa shilingi milioni moja Mjini Magharibi na kwengine sijui wapi. Lakini wakapeleka mfuko wa saruji Kusini Pemba. Kwa sababu Mhe. Naibu Spika, hii mvua ikibakia kunyesha hata kama ikinyesha ya masika isinyeshe ya vuli tuu ienee. Unaonaje na kule ukapeleka kiwango hiki hiki cha fedha kule Pemba kwa Polisi Jamii katika, Wilaya ya Chake-Chake, Micheweni, Mkoani na kadhalika.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba tena kujibu swali ya nyongeza kaka yangu Mhe. Saleh Nassor Juma kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, katika masuala yote yanayohusu ugawaji wa ardhi na fukwe haya yako chini ya Sheria za Ardhi na tunajitahidi sana hapa kuhimiza kwamba Sheria za Ardhi zifuatwe ili kuepuka migogoro ya ardhi. Kwa hiyo, wananchi hawa wa Polisi Jamii kama wanahitaji wote kwa shughuli za fukwe kwa ajili ya maendeleo yao na maendeleo ya nchi basi wafuate hizo taratibu zilizowekwa kwa nia ya kuomba hilo ambalo wanalihitajia kwa maendeleo yao na wananchi kwa jumla. Ni vizuri kwa vikundi hivi kuanzisha miradi ya maendeleo katika maeneo yao. Kwa hiyo, si vibaya kama wana miradi ya msingi ya maendeleo kufanya.

Lakini si katika *open space*, *open space* haziruhusiwi kufanya shughuli za miradi kama hiyo ya hoteli. Zimewekwa wananchi wote watumie maeneo hayo ili yaendelee kuwa wazi. Lakini katika maeneo ambayo wao wanaweza kufanya shughuli za kiuchumi na yapo kwa ajili ya shughuli hizo basi waombe na Serikali itawapa kipaumbele.

Kuhusu kupeleka fedha katika vikundi vyote vya Polisi Jamii nia ya Serikali kufanya hivyo pale ambapo Serikali inayo uwezo na kadri ya mahitaji ya kikundi kilivyo, basi si tatizo uwezo ukiwepo kusaidia vikundi hivi ili ziweze kufanya wajibu wao vizuri.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi na mimi kuuliza maswali ya nyongeza.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa vijana hawa wa Polisi Jamii wanakazi nzito hasa nyakati za usiku,

(a) Je, vijana hawa ni mafunzo yepi waliyoyapata na silaha gani walizozipata ili kuweza kujihami wakitokezewa na matatizo kama ya kuzidiwa na hawa majambazi.

(b) Kwa kuwa zipo baadhi ya Shehia hawataki kuweka Polisi Jamii. Je, Shehia kama hizi yanapotokezea matatizo hatua gani zitachukuliwa yakitokezea matatizo kama hayo ya ujambazi.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi maswali yake (a) na (b) kama ifuatavyo:

(a) Kwa kuwa Polisi Jamii ni vijana na wananchi wameamua kujitolea kufanya kazi ya kusaidia ulinzi katika Shehia zao, na kwa kuwa katika kila Shehia yupo askari wa Polisi Jamii huyu yeye ndiye anapaswa kuwa na silaha katika shughuli za ulinzi. Polisi Jamii hawa hawapaswi kuwa na zana za silaha kama vile bunduki na nyengine kutumia wao.

Isipokuwa wao Polisi Jamii hasa wanatakiwa kutoa taarifa na kumkamata mhalifu. Wale wahalifu ambao wana silaha kali kwa vyovyote vile wanapaswa kwenda polisi na kupiga ripoti kwa sababu kama kuna jambazi ambalo lina silaha kali hilo ni tatizo na ni vizuri bado wana Polisi Jamii hawa wakashirikiana na askari wa Polisi ili wawe na Polisi katika kufanya ulinzi wakati wa usiku kwa nia ile ile ya polisi kuwa na silaha ili waweze kujihami pale ambapo litatokea tatizo.

(b) Kuhusu Shehia ambazo hazitaki kushiriki katika Ulinzi wa Polisi Jamii ni jukumu la Serikali na Polisi wenyewe kutoa elimu zaidi kwa wananchi kwa umma ili waelewe umuhimu wa Polisi Jamii katika Shehi hizi na Shehia hizo nazo ziunge mkono ulinzi huu shirikishi. Kwa sababu ulinzi huu shirikishi ni ulinzi wa kujilinda wenyewe na kwa manufaa yetu wenyewe.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Naibu Spika, kwa sababu Polisi Jamii wanafanya kazi kubwa sana ya uzalendo tena katika nyakati za usiku na kusababisha kuiweka nchi yetu katika amani kama ilivyo.

(a) Kwa nini Mhe. Waziri haoni umuhimu wa vijana wetu hawa kwa wale wenye sifa wakapata ajira za mwanzo wakati Serikali inapoajiri vikosi.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, Polisi Jamii si vijana peke yao wanaotakiwa kufanya shughuli za Polisi Jamii ni sote hata sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi katika maeneo yetu tunapaswa kushirikiana na wananchi katika kulinda maeneo yetu. Kwa hiyo, si vijana peke yao wanaofanyakazi hii ya Polisi Jamii. Kazi hii inafanywa kwa nia ya kulinda maeneo yao.

Kwenye suala la ajira kuna taratibu zake za kupata ajira. Kwa hivyo, vijana wetu hawa wafuate utaratibu ili wapate ajira wanazozipenda kama ni kwenye vikosi ama polisi au Jeshi la Wananchi kama zile sifa zinatimizwa. Kwa vyovyote vile kwa kuwa watakuwa ni wakakamavu, wazoefu kwa sababu ya kufanya shughuli mbali mbali za ulinzi usiku, basi kwa njia moja au nyengine watapewa upendeleo maalum.

Nam. 41

Ukarabati wa Bandari ya Wete

Mhe. Salim Abdalla Hamad- Aliuliza**:-**

Bandari ya Wete ni moja kati ya bandari ambazo zinatumika sana kwa usafiri wa baharini lakini kwa bahati mbaya gati yetu haitoshelezi kutoa huduma ipasavyo. Wizara hasa imejiandaa vipi kuijenga upya/kuifanyia matengenezo gati hiyo ili iweze kutumika ipasavyo kwa muda wote.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano – Alijibu**:-**

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Salim Abdalla Hamad swali lake Nam. 41 kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, kwanza nakubaliana na mawazo yake kwamba bandari ya Wete ni moja kati ya bandari muhimu za Zanzíbar na inasaidia kutoa huduma za usafiri wa watu na mizigo kwa upande wa wananchi wa Mkoa wa Kaskazini Pemba au Pemba kwa ujumla.

Mhe. Naibu Spika, kutokana na umuhimu huo wizara yangu kupitia Shirika la Bandari imekuwa ikiimarisha bandari ya Wete kwa awamu ambapo katika mwaka 2004 gati ya bandari hiyo ilijengwa upya na mwaka 2007 gati hiyo ilirefushwa kufikia kina kikubwa cha maji pamoja na kujengwa jengo jipya la abiria katika mwaka wa 2008.

Katika programu yake ya uimarishaji wa bandari za Pemba Shirika la Bandari limepanga kuendelea na uimarishaji wa bandari hiyo kwa kujenga jengo jipya

la Afisi za Bandari pamoja na kuifanyia matengenezo gati yake sehemu ya mbele ambayo imeonesha kudidimia ili iweze kutoa huduma ipasavyo.

Mhe. Naibu Spika, kwa vile Serikali iko katika hali ya kutengeneza mpango wa kutayarisha gati kubwa ya Maruhubi. Lakini gati hii itakuwa zaidi ni kwa ajili ya kuteremsha na kupakia mizigo. Kwa hivyo, sisi wizara vile vile katika kipindi hichi hichi tumeanza utaratibu wa kutafuta *fund* ya kuweza kufanya *study* kwa bandari zetu nyengine zilizoko Unguja na Pemba.

Kwa hivyo, kuna tamaa kubwa sana ya kupitia Kampuni moja ya Korea kupata *fund,* hivi karibuni tulifanya *study* ya bandari ya Mkaoni, Wete na bandari ya Mkokotoni, ili kuimarisha usafiri wa ndani wa abiria na mizigo. Lengo la Serikali kupitia Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano ni upatikanaji wa bandari wa Maruhubi basi wende sambamba na kuimarishwa bandari zetu hizi kwa ajili ya usafirishaji wa mizigo na abiria. Kwa hivyo, hivi sasa uimarishaji wa bandari ya Wete nadhani utafanywa mara baada kukamilika hiyo *study*. Kwa sababu utaratibu wote wa makampuni au wafadhili wanahitaji kwanza wapate *study* ya pale, eneo hili liweze kujulikana hasa kitu gani kinawezekana na gharama yake na mambo ambayo yanahusiana na hayo.

Kwa hivyo, namuhakikishia Mhe. Mwakilishi kwamba baada ya kukamilika *study* hizi basi programu kamili ya ufuatiliaji wa *study* hiyo utafanyika ili uende sambamba na ujenzi wa hiyo bandari Kuu. Lakini na hizi bandari tatu ziweze kuimarishwa ili usafiri wa abiria na mizigo ndani ya visiwa vyetu uweze kuimarika.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Naibu Spika, nashukuru sana kwa majibu ya Mhe. Waziri wa Miundimbinu na Mawasiliano.

Mhe. Naibu Spika, kwa sababu wakati bandari kuu ya Malindi ilipofanyiwa matengenezo ilitoka kauli kama hii kuwa ikifanyiwa matenengezo na bandari ya Mkoani itaimarishwa katika hali ya kimataifa na hili halikufanyika.

(a) Mhe. Waziri kwa matengenezo haya au kwa tamaa hii ya utengenezaji wa bandari ya Mpigaduri ambao utakwenda sambamba na *feasibility study* ya bandari nyengine kuimarishwa katumia *formular* gani nyengine ili ionekane kama mambo haya mazito yataweza kufanyika na kwa wakati mmoja.

(b) Bandari ni moja ya njia kuu ya kuingizaji uchumi katika nchi hii na wizara inakusanya mapato makubwa kwa vile bandari ya Wete ni ya enzi na enzi na kazi aliyoisifu katika awamu na awamu. Mhe. Naibu

Spika, mpaka leo maji yanajaa ndio vyombo vikaja juu. Haoni Mhe. Waziri kwa kukuza uchumi na kuondoa umaskini iko haja hasa ya makusudi ya kukusudia kuona kwamba bandari ya Wete imeimarishwa katika hali ya kuwa kama bandari nyengine ili iweze kutoa ufanisi wa hali ya juu na vile vile kuingiza mapato ya kutosha katika Serikali hii.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Naibu Spika naomba swali la mwanzo alirejee kwa sababu sikulipata uzuri.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Naibu Spika, ni kuwa ilipotengenezwa bandari ya Malindi miaka michache iliyopita tulipewa kauli kama hiyo wakati inatengenezwa. Kwa hivyo, bandari ya Mkaoni itafanyiwa matengenezo ili iweze kutumika kimataifa yaani mpaka vyombo vikubwa viende kule, makontena na kila kitu na hakikufanyika. Sasa yeye katumia njia ile ile ya kutoa jibu. Katumia *formular* gani nyengine kwa kusema kuwa patakapokuwa na matengenezo ya bandari ya Mpigaduri na bandari ya Wete na nyengine zitatengenezwa katumia *formular* ipi ili mambo hayo yaweze kufanyika wakati huko nyuma yalishindikana tuliangalia kuwa fedha nyingi inayotumika na utengenezaji wa bandari si gharama dogo.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano:

(a) Mhe. Naibu ni kweli kwamba bandari ya Mkoani ilikusudiwa kutengenezwa. Sasa wafanyabiashara wanaomba Shirika la Bandari waweke zana za kuteremshia mizigo ili waweze kuteremsha makontena yao moja kwa moja na Shirika la Bandari limewaambia walete mizigo kwanza. Sasa kitandawili hicho kitateguliwa mara baada ya Shirika la Bandari litakapopata uwezo wa kununua *crane* yenye uwezo mkubwa wa kuteremsha makontena pale Bandari ya Mkoani.

Na hili limo *pipe line* kwa sababu ni kweli wafanyabiashara wanataka kuteremsha mizigo yao Mkoani wale wanaopeleka mizigo Pemba kwa sababu ya kupunguza gharama na usumbufu. Lakini Shirika la Bandari halikuwa na uwezo wa kununua *crane* kubwa ya kuweza kuteremshia makontena.

Lakini kwa kuimarika bandari ya Malindi hivi sasa kwa zana za kushushia mizigo naamini kipindi kifupi kijacho tunaweza kupata kununua *crane* kubwa za kuteremshia makontena Pemba. Kwa sababu kina cha maji kinatosheleza kwa meli kwenda kufunga. Mhe. Naibu Spika, hilo ni suala la ukwasi kwa Shirika la Bandari wenyewe ambalo sio sera ambayo ilikuwa inatumikia.

(b) Mhe. Naibu Spika, kuhusu bandari ya Wete ni kweli ilikuwa ni ya zamani sana na ikitumika kwa hali zote. Lakini namuomba Mhe. Mwakilishi azingatie kwamba aina ya usafiri sasa hivi imebadilika. Kule tulikuwa tukitumia meli halafu zikaenda mashua na kwenda kuchukua watu .

Kwa hivyo, kweli bandari ilikuwepo kubwa lakini meli ikikaa nje halafu mashua zinakwenda kuchukua watu. Sasa aina ya usafiri huo ushapitwa na wakati, watu wanataka kupanda chombo waweze kushuka kwenye gati na kwenda nyumbani. Sasa kama nilivyosema kwamba kwa sababu ya kina cha maji na mambo mengine ambayo yanahitajika kujulikana pale basi *study* ya kufanywa kwenye gati ya Wete ni muhimu sana ili tuweze kujua tunataka gati ya aina gani na gharama zake ni kiasi gani.

Kwa hivyo, kama nilivyokuhakikishia kwamba Wizara inafahamu, Serikali inafahamu kwamba gati ya Wete ni muhimu kwa sababu hata wenye vyombo wanajua kwamba abiria wengi zaidi wanaotoka ni Mkoa wa Kaskazini kwa sababu *population* iliyoko kubwa zaidi. Lakini tatizo kama ukifanya jambo ulifanye kwa uhakika na kitaalamu.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na naomba nimuulize Mhe. Waziri swali la nyongeza kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:

(a) Mhe. Naibu Spika, mara kadhaa Serikali imekuwa ikiripoti kwamba imefanya tafiti mbali mbali kwa ajili ya kujenga bandari katika eneo la Mkumbuu na kwamba eneo lile lina kina kikubwa sana cha maji kikitofautiana Mkoani na Wete. Kwa kuwa tafiti zimefanywa zamani na iligundua kwamba Mkumbuu kuna eneo zuri la kina cha maji. Kwa nini tugharimu fedha nyingi kwa kufanya utafiti wetu na sehemu nyengine wakati eneo tayari limefanywa utafiti la Mkumbuu tusiekeze huko kwa ajili ya kujenga hiyo bandari.

(b) Nichukue nafasi hii Mhe. Naibu Spika, kupongeza sana kampuni ya *Azam Marine* kwa kuchukua juhudi za Serikali kwa kutengeneza maeneo ya kukaa abiria bandarini Malindi. Hivi karibuni tulipata taarifa kwamba kampuni hii ina malengo ya kupeleka vyombo vyake Pemba Wete kwa ajili ya kuanzisha usafiri wa Wete - Tanga na imeomba eneo kwa ajili ya kujenga mazingira mazuri kama yalivyo Malindi kwa ajili ya abiria wake wa *Azam Marine* na eneo la

kuegesha meli zake kule Wete. Naomba nijue, Wizara imechukua hatua gani kama ombi lile limefika kwa *Azam Marine.*

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, naomba nimjibu Mhe. Hija Hassan Hija swali lake la nyongeza lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Kuhusu bandari ya Mkumbuu suala hili nitamletea kwa maandishi hali ilipofikia kwa sababu sasa hivi inavyoangaliwa ni bandari ya Mpigaduri. Lakini uwezekano wa kujenga bandari Mkumbuu upo, kwa sababu maji yako kina kikubwa.

Tunazungumza gati za Mkoani na Wete kwa sababu ndizo zilizomo sasa hivi na ndizo ambazo zinatumika. Kwa hivyo, kwanza ni muhimu kuzitengeneza na kukiimarisha kile ulichonacho ili kiweze kutumika kwa ufanisi zaidi na kwa manufaa zaidi. Tunajua na wewe unajua kwamba kuna safari nyingi zinazofanywa baina ya Wete na Tanga na bandari zaidi inayotumika ni ya Wete. kwa hivyo ni muhimu sana baada ya kutizama yale malengo makuu ni kutizama na wastani na malengo madogo madogo ya muda mfupi. Malengo yenyewe ni kama:-

(1) Bandari ya Mkumbuu itakuwa ni malengo ya muda mrefu.
(2) Kuhusiana na azma hiyo mimi binafsi sijapata taarifa kwamba kumekuja barua rasmi. Lakini hilo ni suala ambalo anawasiliana na Shirika la Bandar, kwa hivyo Shirika la Bandari litaweza kumuelekeza nini cha kufanya kama ambavyo aliwasiliana na Shirika la Bandari hapa Unguja na wewe umetoa pongezi. Kazi yote ile waliwasiliana na wanashirikiana na Shirika la Bandari na kwa hivyo, popote pale wanapotaka kufanya ziada ya kazi au wanapotaka kusaidia wanawasiliana na Shirika la Bandari linao uwezo kamili wa kuweza kumuelekeza na kumpa ruhusa ambayo itakuwa ni ruhusa ya wizara.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri wetu naomba niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Mhe. Naibu Spika, bandari ya Wete sio tu ni muhimu kwa usafiri wa abiria lakini hata kwa usafirishaji wa bidhaa kutoka Mombasa, Tanga, Pemba na Unguja na kwa kuwa katika MKUZA II imetiliwa sana umuhimu huu wa *Poverty Reduction and Income Generation,* yaani kwa wananchi wetu kuongeza kipato na kupunguza umaskini.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa serikali yetu kila kukicha haijajipanga, ina mpango mkakati, ilimradi mambo tu, tuko mbioni mbio zilizokuwa hazifikwi. Je, kwa kuendelea nyinyi kuwa katika mpango mkakati, mko mbioni na huku

vijana wetu wanashindwa kuingiza bidhaa, kama pale Pemba kutoka Tanga, au kutoka Mombasa kupitia bandari ya Wete.

Je,…

Mhe. Naibu Spika: Uliza swali Mhe. Mjumbe.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante, ilikuwa ni mipangilio tu Mhe. Naibu Spika, baada ya utangulizi huo naomba kumuuliza je, kwa kufanya hivyo hamuoni wizara yako inakwenda kinyume na mpango huu na kukiuka MKUZA II. Hiyo ni moja.

Je, Mhe. Naibu Spika, kwa kufanya hivyo hamuoni kwamba hawa vijana wetu badala ya kuchukua tungule hawana pa kupitia pale, watajiingiza katika ile biashara haramu ambayo sisi siku zote tunaikataza ya kukaa vijiweni na kuanza kuvuta mabangi na mambo mengine.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Naibu Spika, katika majibu yangu mama nilisema kwamba serikali na wizara kwa jumla zinaelewa umuhimu wa *gate* za ndani katika usafirishaji wa abiria na mizigo. Ndio maana nikasema mwanzo kwamba tunaandaa *study* ya kuifanya kati ya *gate* ya Mkoani, Wete na Mkokotoni ili ziweze kuhudumia ipasavyo hizo shughuli za usafiri.

Lakini nataka nikukumbushe tena kwamba hakuna njia ya urahisi katika utekelezaji wa kazi hizi za kitaalamu, ni lazima ukubali kwamba wako wataalamu ambao wanaweza kuja kufanya *study*, wakaelewa uzito wa kazi iliopo na gharama yake kabla wewe hujaianza. Ukiingia tukifua moja kwa moja basi unaweza ukamalizia hivi hivi tu, huna lolote unalolipata. Kwa hivyo, ni lazima tukubali kwamba hizi zifanyiwe *study* ili ziweze kujulikana hasa, tunafanya nini na kwa gharama gani na muda upi. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Nam. 52

Uanzishwaji wa Kitivo cha Sayansi ya Mazingira (*Faculity of Enviromental Science*) katika Chuo Kikuu cha Taifa (SUZA).

Mhe. Saleh Nassor Juma - Aliuliza:-

Kwa kuwa mabadiliko ya tabia nchi imekuwa ni tatizo kubwa sio tu kwa mazingira ya nchi yetu lakini hata kuathiri uchumi wa nchi mbali mbali hususani hizi nchi zilizoko kusini mwa jangwa la Sahara.

(a) Je, ile programu ya Chuo Kikuu cha Taifa (SUZA) ya kuanzisha '*Faculty of Enviromental Science'* tayari imeanza.

(b) Kama bado tatizo liko wapi.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali - Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mheshimiwa, mkereketwa swahibu yangu swali lake nambari 52 lenye sehemu (a) na (b) kwanza napenda kutoa maelezo ya utangulizi kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, ni kweli kuwa mabadiliko ya tabia nchi imekuwa ni tatizo sugu sana katika dunia yetu na hasa katika nchi maskini kama ilivyo Zanzibar. Nchi hizi zinaandaa mikakati mbali mbali ya kupambana na tabia nchi na matatizo yake. Pamoja na mikakati mingi iliyopangwa, mikakati ya Zanzibar ni kusomesha wataalamu wetu ili waweze kusaidia kupambana na matatizo haya ya tabia nchi. Baada ya maelezo hayo ya utangulizi, naomba kujibu swali la Mhe. Mwakilishi nambari 52 lenye vipengele (a) na (b) kama hivi ifuatavyo;-

a) Mhe. Naibu Spika, katika mwaka wa masomo wa 2013/2014, Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar kinakusudia kuanzisha masomo yafuatayo, yaani fani ya mazingira ya afya. (*Environmental Health*); Shahada ya Sanaa katika Jiografia na Mazingira (*Geography and Environment*) na Shahada ya Uzamili katika masuala ya mazingira.

   Mhe. Naibu Spika, wizara yangu sasa hivi haina tatizo la kuanzisha masomo hayo. Mara tu tukimaliza bajeti yetu fedha zitakuwepo, wahadhiri wapo na nafasi za kusomesha nafasi hizo zipo na tutaanza mara moja.

b) Kama nilivyotangulia kusema masomo hayo yataanzishwa baada ya kumaliza wakati wetu huu wa bajeti ili tupate fedha za kuanzisha masomo hayo.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya mzee wangu pale Mhe. Waziri. Kabla ya kuuliza swali la nyongeza napenda nimpongeze *Vice Chanceller* wa Chuo Kikuu cha SUZA *profesor* Idrissa Rai pamoja na jopo zima la wataalamu kwa kuweza kutuendeshea chuo chetu hiki kwa umakini mkubwa mno. Basi kwa niaba

yangu na niaba ya wapiga kura wa Jimbo langu la Wawi, tunampongeza sana *profesor* Idrissa Rai na jopo lake la wataalamu kwa hilo.

Baada ya maelezo hayo naomba kuuliza swali moja la nyongeza kama ifuatavyo. Kwa sababu *Professor* Rai na jopo lake la wataalamu huu mpango wa kuanzisha digrii hii inayohusiana na mambo ya *Environmental Sciences* ilikuwa ni karibu miaka 4 nyuma, lakini kwa sababu bajeti ndogo sana ndio imebidi wapate shida mpaka wanataka kuanzisha sasa.

Je, ni lini serikali itapanua bajeti ya chuo kile ili kiende sambamba na vyuo vyengine vya kimataifa pale kitakapoanzisha programu zake iweze kupanua kwa urahisi, hivi sasa kimekuwa kinasua sua kila mara. Je, ni lini watawapanulia bajeti SUZA ili waweze ku- *focus* hizi programu zao kwa wakati wanaohitaji.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Naibu Spika, masomo hayo niliyoyataja yatasomeshwa katika jengo la sayansi jamii linatosha kabisa kwa kusomesha masomo hayo yote niliyoyataja.

Pia nataka nimkumbushe kwamba hivi juzi tulizindua rasmi chuo chetu pamoja na wale wafadhili wetu wa *BADEA*. Katika uzinduzi tulisema tunakwenda sasa katika awamu ya pili na awamu ya pili ipo, eneo lipo limeshapimwa na limeshatolewa hati miliki lipo. Tukasema tupate fedha za kutosha za kujenga hii awamu ya pili. *BADEA* pale pale bila kusita walitaja fedha zipo, sizikumbuki walizozitaja lakini fedha zipo na kwa hivyo fedha za kuanzisha awamu ya pili zitatosha.

Kwa hivyo, sio tu kwamba tunalo eneo hivi sasa la kuyaanzisha hayo masomo niliyokutajia ya mazingira, lakini bado chuo chetu tunakipanua tumemaliza awamu ya kwanza. Sasa tunaingia awamu ya pili na chuo chetu kitakuwa kikubwa miongoni mwa vyuo vya Afrika Mashariki.

Nam. 71

Ukosefu wa Usafiri kwa Wafanyakazi wa Hospitali ya Mnazi Mmoja

Mhe. Saleh Nassor Juma - Aliuliza**:-**

Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kabla swali langu nambari 71 halijajibiwa, naomba kufanya marekebisho katika ukurasa wa 3 sio asubuhi hadi usiku, ni asubuhi hadi mchana. Katika ukurasa wa 6, utakutia neno saa 5:00 na kuwaondoka, hapana ni saa 5:00 usiku na kuondoka hospitali usiku.

Halafu ukurasa wa 9, hospitalini hapo angalau, unaliondosha neno hospitalini hapo angalau, inabakia kuwaondosha wafanyakazi mpaka kwenye kituo cha daladala, hili neno hospitalini hapo angalau linaondoka kabisa ni *printing mistake*. Baada ya marekebisho hayo Mhe. Naibu Spika, kwa heshima kubwa na taadhima ya hali ya juu, naomba swali langu nambari 71 lijibiwe.

Kwa kuwa wafanyakazi wa Wizara ya Afya wakiwemo madaktari na manesi, hulazimika kuingia kazini kwa awamu (*shift*), kwa maana asubuhi hadi usiku. Mchana hadi saa 4 usiku na usiku hadi asubuhi na kwa kuwa baadhi ya wafanyakazi wakike hulazimika kutoka kazini zaidi ya saa 5.00 usiku na kuondoka hospitali usiku huo hadi kituo cha daladala Darajani kwa miguu, ikitiliwa maanani kuwa hospitalini hapo hakuna usafiri wa kuondosha wafanyakazi hospitalini hapo angalau mpaka kwenye kituo cha daladala, jambo ambalo linaweza kusababisha madhara makubwa ya kuibiwa pamoja na kubakwa.

(a) Je, Serikali inalitambua tatizo hilo.

(b) Ni lini serikali itatafuta usafiri maalum kwa ajili ya wafanyakazi hao.

Mhe. Waziri wa Afya – Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 71. lenye vifungu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, kama nimemuelewa masahihisho aliyoyafanya ni kwamba sio saa 5:00 na sisi tulikuwa tumeshaandika humu kwamba hakuna *shifti* yetu inayofika saa 5:00 za usiku.

Baada ya maelezo hayo naomba kujibu swali lake kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, vipindi vya kazi (*shifti*) za wafanyakazi wa mahospitali yote Zanzibar isipokuwa madaktari na wapiga picha za *X- ray* ni masaa 8 au saa 8 kwa lugha sahihi, *shift* za asubuhi ni saa 1:00 mpaka saa 8:00, mchana saa 8 mpaka saa 3:00 usiku na *shifti* ya usiku ni saa 3:00 usiku mpaka saa 12:00 asubuhi. Kama alivyosahihisha ni kwamba hakuna *shifti* inayofika saa 5:00 ya usiku.

Kwa taarifa yake Mhe. Mwakilishi wafanyakazi wa Wizara ya Afya wakiwemo wa Mnazi Mmoja ndani ya mshahara wao, tulivyoelezwa na utumishi kwamba inakuwepo sehemu ya posho la usafiri. Kuchukua jukumu la kuwatafutia gari wafanyakazi wa Mnazi Mmoja itatakiwa liwe jukumu la

hospitali ya Mnazi Mmoja na uongozi wake, kitu ambacho kiko nje ya uwezo wake hospitali hiyo kwa hivi sasa.

Kwa usalama wao kuwasaidia wanawake na wanaume, maana yeye kataja wanawake tu, wa hospitali ya Mnazi Mmoja wasipate tabu ya kuingia na kutoka usiku, wizara imezungumza na uongozi wa hospitali ili washauriane na wafanyakazi wao wanaoingia *shift*.
Kuna mfano mzuri unaofaa kuigwa ni ule wa Hospitali ya Muhimbili ambao nao walikuwa na tatizo hilo hilo la usafiri, ikifika saa 12:00 magari hayendi huko, yaani hayafiki pale Muhimbili hasa daladala. Walichokifanya wamepunguza masaa ya *shift* ya saa 8 inakwisha saa 6:00 na ile ya mpaka saa 12:00 na kuongezea muda kwa *shift* ya usiku ambayo inaanza saa 12:00 mpaka asubuhi. Sasa ni juu yao kukubali mabadiliko au kukataa tumewaachia wenyewe Hospitali ya Mnazi Mmoja. Ni ushauri unaoweza kutatua tatizo hili, ahsante.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Naibu Spika, uongozi wa Hospitali ya Mnazi Mmoja kwa kuwa unawajibika kwa wizara na kwa kuwa kilio hiki sio cha kubahatisha. Mimi nilikuwa ni mjumbe wa Kamati ya Ustawi wa Jamii, nimekipata katika vikao vya kamati kutoka kwa hao hao ma-*nurses* na madaktari wa pale ndio waliotuelezea na kwa kuwa katika kipindi chote hiki uongozi wa Hospitali ya Mnazi Mmoja umeshindwa kulitafutia tiba tatizo hili, kiasi ambacho wafanyakazi hawa wanalazimika kuwakimbia vibaka kwa kunyang'anywa dhahabu zao pamoja na wao wenyewe kufanyiwa vitendo vya udhalilishaji ukiwemo wa jinsia.

a) Je, Mhe. Waziri haoni kwamba sasa umefika wakati wizara kuingilia kati uongozi wa Hospitali ya Mnazi Mmoja ili kufanya maarifa ya kupata usafiri pale wa kuwaokoa angalau pale Mnazi Mmoja mpaka kwenye kituo cha daladala ili kuepusha wale ma-*nurses* wetu wazuri wadogo wadogo kubakwa na vibaka.

b) Mhe. Naibu Spika, mimi nashangaa sana kwamba *Laurant School* ni *private school* na kuna hospitali hizi za *private* vile vile wana-*afford* kupeleka usafiri na sio wa kuchukua wafanyakazi tu, lakini mpaka wanafunzi wao. Hospitali kubwa kama Mnazi Mmoja ambayo tumeiasisi sisi hapa tokea miaka ya 1960 hospitali ile kushindwa kupata kuwa-*afford* wafanyakazi wake pale mpaka kituoni. Hii si aibu sio kwa Hospitali ya Mnazi Mmoja tu lakini mpaka kwa serikali kwa jumla.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, suala la kuingilia kati wizara ni suala la msingi lakini Wawakilishi hawa hawa mara nyengine huwa wanatuambia kwamba tusiziingilie shirika na maidara wafanye kazi zao. Kwa

hivyo, katika daraja ya uongozi wa Mnazi Mmoja wajibu wetu ni kuwashauri na tumewashauri.

a) Lakini Mhe. Naibu Spika, kuna tatizo vile vile tulijaribu kuwaambia waambiwe wafanyakazi wakubaliane na wenye daladala maalum ambapo sio suala gumu, ili iwe hiyo daladala iwe inabaki pale katika kituo cha daladala kusubiri wafanyakazi hao wawe wanaondoka saa 3:00 za usiku. Suala gumu lililokuja je hao wafanayakazi watasubiri, isiwe daladala ikabaki pale, halafu ikawa mmoja kasema anakwenda mazikoni, mwengine anakwenda harusini, ikawa ile daladala badala ya kupata wafanyakazi kujaza wakawapeleka wanakostahiki basi likabaki tupu. Likaonekana nalo sio rahisi kulifanya hivi. Suala la wizara kuingilia pale tutakapopata nafasi na kupata fedha tunaweza kusaidia. Lakini ni vizuri ifahamike kwamba tatizo la usafiri kwa wafanyakazi wa Wizara ya Afya ni kubwa zaidi kwa wafanyakazi wanaofanyakazi vituo vya shamba ambao hakuna nyumba na wanaofanyakazi katika hospitali za Pemba. Mara nyingi hospitali ya Wete, Chake Chake na Mkoani ikifika saa 12:00 hakuna daladala na wengi wanakaa mashamba. Kwa hivyo, sio tatizo la Mnazi Mmoja tu kama ni kusaidia usafiri.

b) Ni kweli hospitali za binafsi na skuli zinawapa mabasi wanafunzi na walimu. Mhe. Saleh Nassor anaujua utaratibu wao. Si ajabu kwamba nako wanachangishwa walimu kulipia ile fedha baada ya lile basi kuwepo, siwezi kujua kuna utaratibu gani kwenye hospitali za binafsi.

Mhe. Salma Mohamed Ali: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru baada ya majibu mazuri ya Mhe. Waziri, naomba nimuulize swali moja la nyongeza lenye vifungu (a) na (b). Kwa kuwa Mhe. Waziri alipokuwa akizungumza na wafanyakazi wa Wizara ya Afya, katika ziara ya Makamu wa Kwanza wa Rais Pemba mwaka jana. Wafanyakazi hao walimlalamikia kwa kunyimwa fedha zao za *overtime* na usafiri. Kwa kuwa watendaji waliahidi kulishughulikia suala hili.

a) Je, Mhe. Waziri anajua kwamba hadi leo haijatekelezwa ahadi hiyo.

b) Ikiwa ni hivyo, Mhe. Waziri atawasimamia vipi watendaji wake ili kuitimiza ahadi iliyotolewa mbele ya Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, ni kweli wafanyakazi wa Pemba walilalamika hivyo na viongozi tuliahidi mbele ya Makamu wa Rais. Lakini suala linalohusu *overtime* ni suala linalohusu fedha na madamu linahusu fedha inabidi liingizwe kwenye bajeti na lijulikane kwa utaratibu maalum, sio suala la moja kwa moja la Wizara ya Fedha.

Pale tulipoweza kufanya mawasiliano na Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, tulipewa kile kilichostahiki, tutakapopata nafasi tutafanya wajibu wetu. Lakini hatuwezi kusema kwamba tutawapa wakati fedha tutakuwa hatuna.

Suala la pili kuhusu kuwasimamia watendaji wetu tunawasimamia na tutaendelea kuwasimamia kwa lile linalostahiki. Lakini *overtime* nayo vile vile ina utaratibu wake. Utaratibu wa *overtime* una masharti yake hasa kwa Wizara ya Afya. Kuna watu wanaofanya *shift*, na *shift* haina *overtime*, *overtime* italipwa kwa yule mtu ambaye anafanyakazi zaidi ya ule wakati unaopindukia na muajiri wake au msimamizi wake lazima aweke kumbukumbu inayostahiki, kwa lile litakalostahiki tutawalipa wafanyakazi hao kama tunavyowajibika.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa fursa hii kuweza kumuuliza swali la nyongeza Mhe. Waziri wa Afya. Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri wa Afya katika jibu lake la sasa hivi amekiri kama ni kweli kuwa Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais alipotembelea na wao walichukua dhamana hiyo ya kusema kuwa watatekeleza.

a) Je, Mhe. Naibu Spika, huoni kama hapo kutokutekeleza ni kumdhalilisha Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais.

b) Kwa sasa hivi wako matajiri wengi wanatoa *offer* za kukopesha vyombo wafanyakazi. Huoni sasa hivi Mhe. Waziri ukatoa fursa hiyo ili wafanyakazi wakaweza kukopa gari na kukopa vespa kwa kupitia matajiri hao.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, kutokulipwa *allowance* au *overtime* ni utaratibu wa utawala, hauna mawasiliano na kumdhalilisha kiongozi. Kiongozi anaagiza na watendaji tunawajibika, lakini tunawajibika kwa kufuata taratibu zilizokuwepo na taratibu hizo ni mbili. Ni za fedha na za utumishi, kwa hivyo hatumdhalilishi Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais.

Suala la pili, ni suala zuri sana alilolizungumza Mhe. Mshimba, nafurahi sana kwa ushauri wake. Hii ni moja katika taratibu tunazoshirikiana na watu wa utumishi na Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo katika sehemu ya motisha ya wafanyakazi, lakini nalo mpaka likubalike na serikali na nani atakuwa dhamana wa kulipa mikopo hiyo. Maana usisahau Mhe. Mwakilishi kwamba kukopa ni rahisi na kulipa ni matanga. Kwa hivyo, ni suala linalohitaji utaratibu, anachukua dhamana nani na litalipwa vipi.

Mhe. Naibu Spika, gari ni ghali pesa zake zinazohitajika kulipwa ni nyingi, mishahara yetu tunaijua. Sasa unapoamua kukopa ukaambiwa utalipa shilingi 10,000 au shilingi 30,000 au laki mbili kwa mwezi, usije ukenda kwenye *vocher* ukazikuta shilingi 30,000 ukalalamika, maana yake zitakuwa zinakatwa moja kwa moja ndio utaratibu ambao wewe utakubali. Kwa hivyo, ni ushauri mzuri lakini suala litakalomalizwa na Mhe. Waziri wa Utumishi wa Umma na Utawala Bora na Mhe. Waziri yuko hapa anaweza kusaidia kuona utaratibu huo upo tayari au unaendelea kutayarishwa. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Nam. 7

Mradi wa Maji Kutoka Japan

Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Aliuliza**:-**

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya Awamu ya Sita, kwa kushirikiana na Serikali ya Japan ilianzisha mradi mkubwa wa maji ili kumaliza tatizo la maji katika Mkoa wa Mjini/Magharibi. Hata hivyo, bado wananchi wa Mkoa huo wanakabiliwa na tatizo kubwa la maji.

(a) Kwa kuwa mradi huo ni mkubwa na Serikali imetumia fedha nyingi. Je, ina mpango gani wa kumalizia mradi huo ili wananchi wafaidike na huduma safi na salama.

(b) Je, kwa hatua iliyofikia sasa, mradi umegharimu kiasi gani cha fedha.

(c) Hivi ni asilimia ngapi ya wananchi wa Mkoa wa Mjini/Magharibi wanapata maji safi na salama.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati - Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 7 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Naibu Spika, mradi wa maji wa Mkoa wa Mjini/Magharibi umekamilika tangu mwaka 2009, lakini kwa bahatí mbaya mradi huo haukuwa na mafanikio makubwa kwa baadhi ya maeneo. Hata hivyo, wizara yangu na Mamlaka ya Maji ina mpango wa kuchimba visima tisa vyengine, ili kuongeza wingi wa maji katika mkoa huo na hadi sasa tayari imeshachimba visima vitano katika maeneo ya Chumbuni, visima vitatu Saateni na visima viwili Chumbuni. Jitihada za kuchimba visima vyengine vinne vitakamilika mara tu hali ya fedha itakaporuhusu.

(b) Mhe. Naibu Spika, mradi wa Mkoa wa Mjini/Magharibi uliofadhiliwa na Serikali ya Japan hadi kukamilika kwake, umegharimu jumla ya shilingi za Kitanzania bilioni thalathini na mbili na milioni mia tano (Tshs. 32,500,000,000.00) ambazo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzíbar ilichangia jumla ya Shilingi za Kitanzania milioni mia tano (Tshs. 500,000,000.00) na Serikali ya Japan ilichangia Shilingi za Kitanzania bilioni thalathini na mbili (Tshs. 32,000,000,000.00).

(c) Wananchi wa Mkoa wa Mjini/Magharibi hadi sasa wanapata maji safi na salama kwa asilimia 65 tu, kiwango ambacho ni kidogo. Wizara yangu bado haijaridhishwa na kiwango hicho na ndio maana inaongeza kuchimba visima, ili kupunguza tatizo la mgao wa maji uliopo ili hatimae kuondosha kabisa tatizo la maji hapa visiwani.

Mhe. Hussein Ibrahim Makungu: Nakushukuru Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuuliza swali moja la nyongeza. Kwanza nampongeza sana Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri. Mhe. Naibu Spika, kama tunavyojua Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar inajitahidi sana kuboresha miundombinu ya barabara. Skuli ya Bububu Kwahanzari kwenda Mwanyanya ilikuwa kuboreshwa kwake kutiwa kifusi barabara ile, lakini kwa bahati mbaya miundombinu ya mabomba ya maji kutokea Mwanyanya yote yamekatika kabisa na wananchi hao hawapati maji kwa sasa.

Je, Mhe. Waziri suala hili unawaambia nini wananchi wa eneo hilo wanaloishi na mwezi wa Ramadhani unakuja na maji hawapati kabisa, ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Naibu Spika, ni kweli kabisa wizara yangu inajua kuwa kuna matatizo ya mabomba yaliyokatika na mengine yamechakaa, kwa sababu hiyo ndio na mimi nafanya jitihada ya kuomba msaada kutoka *Afrikan Development Bank*, katika mradi unaoitwa *ADF* 12 ambao tayari tumeshautia saini, kwa madhumuni ya kutengeneza mabomba haya ambayo yale yaliyotoboka na mengine yaliyochakaa.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwezi Mtukufu wa Ramadhani mpango tulioufanya ni kusambaza maji kwa magari kama tulivyofanya mwaka jana katika maeneo mbali mbali ya mkoa huu.

Mhe. Nassor Salim Ali: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana na mimi kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza pamoja na majibu mazuri ya Mhe.

Waziri. Lakini bado tatizo la maji hususani Wilaya ya Mjini katika maeneo ya Jimbo la Rahaleo, Kikwajuni na Kwahani.

Katika Jimbo la Rahaleo hususan kwenye Shehia za Gulioni, Mwembeladu, Makadara, Mlandege na pamoja na Shehia ya Rahaleo yenyewe. Kwa kweli tatizo ambalo limesababisha upungufu wa maji ni miundombinu ambao imekuwa ni mibovu.
Je, wizara ina mpango gani wa kufanya miundombinu mipya ili kutatua tatizo la maji katika Jimbo la Rahaleo na majimbo jirani. Vile vile katika kipindi hichi cha mwezi Mtukufu wa Ramadhani. Je, imejipanga vipi kuondoa tatizo hilo katika maeneo hayo.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Naibu Spika, katika Mkoa wa Mjini/Magharibi maji tunayoyahitaji tuyapate ili kila mtu apate maji ni lita 54 milioni. Sasa asilimia 65 niliyoitaja maana yake ni lita 35 milioni na hizo ndizo tunazozipata kwa vyovyote vile hazikidhi katika Mkoa wa Mjini/Magharibi.

Kutokana na hali hiyo, ndio maana tumeanzisha jitihada ya kuchimba visima vyengine vipya ili kujaliza viwango vya maji, kwa sababu hata hayo matangi ambayo tunayo basi bado hayajai kutokana na tatizo la tabianchi ambalo nimelizungumza muda mfupi uliopita hivi sasa.

Kwa hivyo, mimi ninamuomba Mhe. Mwakilishi kwamba tatizo hili sio katika Wilaya ya Mjini tu, isipokuwa ni wilaya zote mbili na ni tatizo kubwa kwa kutafuta hilo pengo la maji, kwa sababu lita 54 milioni tunalo pengo kubwa kabisa ambalo la lita kama 19 milioni, ili kuweza kutosheleza maji katika Mkoa wa Mjini/Magharibi ndio tunachimba hivyo visima.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu suala la miundombinu chakavu ndio nikasema kwamba wizara yangu kwa kushirikiana na *ZAWA* wamejitahidi kutafuta wafadhili, ili tuweze kupata fedha za kuweza kutengeneza hii miundombinu michakavu, ndio maana tumeanzisha mradi ambapo hivi sasa anatafuta mkandarasi kwa sababu fedha tayari zimeshapatikana kwa ajili ya kutengeneza miundombinu ya maji katika Mkoa wa Mjini/Magharibi.

Vile vile kuhusu mwezi Mtukufu wa Ramadhani tutakachokifanya ni kama tulivyofanya mwaka jana tutasambaza maji katika maeneo mbali mbali ya mjini. Mhe. Naibu Spika, kuhusiana na suala hilo tayari tumeshajipanga vizuri katika wizara pamoja na *ZAWA* wenyewe kuifanya hiyo kazi.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa ya kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza.

Kuna maeneo ambayo yalikuwa yakipata maji na hivi sasa hayapati maji eneo moja ni Welezo juu karibu na Makufuli kwenye matangi ya maji. Kwa kweli eneo lile ilikuwa wananchi wanapata maji bila ya matatizo yoyote na kwa sababu maji yao yalichukuliwa akaungiwa mfanyabiashara ambaye anamwagilia maji yule mwenye kufuga wanyama kule, hivyo wananchi wa pale hawapati maji hata kidogo yaani hata siku moja.
Je, Mhe. Waziri haoni kama kuwakosesha wananchi maji na ukayapeleka kwa mfanyabiashara na wao wakawa wanakosa, hali hii ni kuwakosesha matunda ya maendeleo ya serikali yao. Je, kama hivyo ndivyo, haoni kama kuna haja kwa kipindi hichi cha Ramadhani wananchi wale wanaokunywa maji ya vipuji wanarejeshewa maji, ili wapate wafaidike.

Mhe. Naibu Spika, kama hivyo ndivyo basi ni lini wizara yako itafanya bidii ya kuwarejeshea maji wananchi wale ili na wao wafaidike.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Naibu Spika, kwa kweli asivunjike moyo, lakini nitamjibu hali halisi ninayoijua. Kwa kweli mimi sina taarifa kwamba kuna maji yamechukuliwa ambayo yalikuwa yanakwenda kwa wananchi na kupelekewa mfanyabiashara anayelima mboga sina taarifa hiyo. Lakini nashukuru kwamba taarifa hiyo nimeipata kutoka kwake yeye hivi sasa katika kuuliza swali hili.

Mhe. Naibu Spika, taarifa niliyonayo ni kwamba Mwakilishi wa Jimbo la Magogoni amekuja kuniambia kwamba kuna tatizo la maji Welezo na anahitaji kuchimbiwa kisima ili wananchi wale wapate maji katika eneo lile na taarifa hiyo ninayo rasmi.

Kwa bahati mbaya mashine yetu ya kuchimbia kisima ni mbovu na kwa sababu hiyo tulikuwa tumeshaagiza mashine nyengine mpya ya kuchimbia kisima na tumeshaipata na tayari imeshafika Zanzibar, basi tutakwenda kuchimba kisima katika maeneo hayo. Lakini katika mwezi Mtukufu wa Ramadhani tutakachokifanya tutasambaza maji pamoja na Welezo na sehemu nyengine kama tunavyofanya. *(Makofi)*

UTARATIBU

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Naibu Spika, kuhusu kauli ya Mhe. Waziri sikusema kama anamwagilia mboga mboga, isipokuwa anayo mifugo ya wanyama ndio anamwagilia kwenye wanyama na sio mambo ya mboga mboga.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe, sawa na alivyokujibu kwamba hana taarifa lakini kama umeshampa taarifa atafuatilia. *(Makofi).*

Nam. 21

Ukosefu wa Ajira kwa Vijana Zanzibar

Mhe. Nassor Salim Ali (Kny: Mhe. Jaku Hashim Ayoub) – Aliuliza:-

Vijana wengi hivi sasa wanaomaliza elimu ya juu na sekondari hawana kazi Zanzibar na wengine kujihusisha na vitendo vya matumizi ya dawa za kulevya na uhalifu.

(a) Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wananchi Kiuchumi na Ushirika imefanya utafiti ni vijana wangapi waliomaliza elimu ya juu lakini bado hawajapata kazi.

(b) Je, serikali inachukua hatua gani za kuondoa tatizo hilo.

(c) Kwa kuwa Zanzibar imezungukwa na bahari serikali imechukua hatua gani ya kuanzisha viwanda vya kusindika samaki au kununua boti za uvuvi.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wananchi Kiuchumi na Ushirika – Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 21 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, kabla ya kumjibu swali kwanza naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Idadi ya watu ikiwemo vijana imekuwa ikiongezeka mwaka hadi mwaka duniani kote. Nchi zinazoendelea hasa za Kusini mwa Afrika zinaelezwa kuwa na ongezeko la kasi zaidi la idadi ya watu kuliko nchi nyengine duniani. Sababu mbali mbali zimeelezwa kuwa chanzo cha ongezeko hilo, ikiwemo umaskini, suala la uhamiaji na uzazi usio wa mpango.

Taarifa za sensa mbali mbali zilizofanywa nchini kwetu zinaonesha Zanzibar kuwa na ongezeko la watu la wastani wa kati ya asilimia 2.7 na 3.1 kadri miaka inavyokwenda. Sensa ya mwaka 1967 Zanzibar ilikuwa na watu 354,815 na mwaka 2012 imeripotiwa kuwa na watu 1,303,569. Ongezeko hili la watu ni pamoja na vijana.

Kwa kuzingatia ongezeko hili, ni wazi kuwa uorodheshwaji wa wanafunzi kujiunga na masomo utakuwa mkubwa. Aidha, wahitimu nao wataongezeka.

Hivyo kila mwaka vijana wengi wahitimu wa vyuo au sekondari watakuwa katika mchakato wa kutafuta ajira, jambo ambalo ni la kawaida duniani kote.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo, sasa napenda kujibu vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Serikali inafahamu matatizo yanayowakabili vijana wake kutokana na ukosefu wa ajira. Hivyo imeandaa mikakati mbali mbali ya kuwasaidia vijana hao kuweza kuajiriwa au kujiajiri wenyewe. Mikakati hiyo ni pamoja na:-

i) Programu ya Kazi Nje Nje ambao inatoa taaluma ya ujasiriamali kwa vijana, ili wafahamu fursa zilizopo na waweze kujiajiri. Mafunzo hayo yanahusisha masuala ya kubuni wazo la biashara, kuanzisha biashara na mpango wa biashara.

ii) Kutoa taaluma ya kuwashajiisha vijana kubadili mtazamo wao kuhusu kazi, ili wawe na tabia ya kupenda kazi na kuacha kuchagua kazi.

iii) Kuwashajihisha waajiri kwenye sekta binafsi kama mahoteli, kuwaajiri vijana wa maeneo yao. Katika kipindi cha 2011/2012, jumla ya vijana 90 waliunganishwa na waajiri na kupatiwa kazi kwenye sekta binafsi. Idadi hii ni kwa waliyojiorodheshwa Wizarani. Aidha, jumla ya vijana 238 waliajiriwa serikalini na mashirika katika kipindi hicho.

iv) Vijana na wananchi wengine wamekuwa wakipatiwa mikopo ya masharti nafuu kupitia mifuko ya mikopo iliyopo ikiwemo Mfuko wa Rais wa Kujitegemea na Mfuko wa Vijana.

Katika kipindi cha Julai, 2012 hadi Machi, 2013 jumla ya mikopo 156 yenye thamani ya shilingi milioni 118,300,000/= imetolewa kupitia Mfuko wa Kujitegemea. Mikopo sita kwa wakopaji wa kuendeleza yenye thamani ya shilingi milioni 23,500,000/= ilitolewa kupitia Mfuko wa AK na JK Unguja na Pemba.

Aidha jumla ya mikopo yenye thamani ya shilingi 1,100,000,000/= imetolewa kupitia asasi nyengine zinazotoa mikopo ikiwemo CHANGAMOTO, *WEDTF*, *YOSEFO*,

Melinne *SACCOS*, *CRDB* na *Chamber of Commence* ambazo zote zinatoa mikopo kwa wajasiriamali wadogo wadogo Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, pia jumla ya shilingi 300,003,000/= zimetolewa kwa vikundi 199 kwa Unguja na Pemba wenye wastani wa wanachama 20 kwa kila kikundi kupitia Mfuko wa ZAKA.

v) Vijana pia wamekuwa wakishajihishwa kujiunga na vyama vya ushirika kama njia mojawapo ya ajira.

(b) Serikali ya Mapinduzi ya Zanzíbar inathamini sana wananchi wake ikiwemo mchango wa vijana katika kuleta maendeleo. Katika mwaka wa fedha 2012/2013, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imetenga jumla ya shilingi bilioni 1.1 kwa utekelezaji wa *program* ya kukuza ajira kwa vijana. Kupitia *program* hiyo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inakusudia kukunua boti za uvuvi wa bahari kuu ili kusaidia ajira kwa vijana.

Aidha Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar moja katika mipango yake mikuu ni kuanzisha viwanda vya kusindika samaki kama Mhe. Mwakilishi alivyoshauri.

Mhe. Naibu Spika, napenda kumjulisha na kumtoa wasi wasi kwamba serikali kupitia wizara inayoshughulikia masuala ya uvuvi inaendelea kutafiti kwa makini suala hilo, kwa lengo la kuwapunguzia wananchi na vijana tatizo la ajira, kuongeza kipato chao na kusaidia ukuaji wa pato la taifa kwa jumla. *(Makofi).*

(c) Wizara bado haijafanya utafiti wa kina kubaini vijana ambao wamemaliza elimu ya juu na hawajabahatika kupata kazi. Hata hivyo, wizara imeshajadiliana hili na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali. Aidha wizara imekuwa ikiwaorodhesha na kuwasajili vijana wanaomaliza elimu ya juu na ya ngazi nyengine ili pale inapotokea fursa waweze kuunganishwa na waajiri kwa kupatiwa kazi.

Pia hivi sasa, wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali zinaendelea na maandalizi ya kufanya tafiti mbili muhimu zinazohusiana na masuala ya kazi.

(i) Utafiti wa watu wenye uwezo wa kufanya kazi; na
(ii) Utafiti kuhusu sekta isiyo rasmi.

Mhe. Nassor Salim Ali: Mhe. Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza.

Mhe. Naibu Spika, kwanza nichukue fursa hii kumpongeza sana Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri na yenye mpangilio wa kuleta maendeleo kwa vijana wetu, pamoja na kuishukuru serikali kwa mipango mbali mbali ambayo Mhe. Waziri ameieleza.

Kwa kuwa kwenye majibu yake ameeleza kwamba kulikuwa na mafunzo mbali mbali ya kupewa taaluma vijana wetu pamoja na mikopo ambayo imetolewa. Je, ni utaratibu gani ambao huwa wanapatikana vijana hawa kwa ajili ya kupewa taaluma pamoja na mikopo.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Naibu Spika, utaratibu unaotumika ni kwamba vikundi vyenyewe ambavyo vimejisajili kama vikundi vya ushirika huwa wanaleta maombi yao. Kwa kweli wakati mwengine Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wengi wao wameleta maombi yao ya kutaka kupatiwa mafunzo wananchi wao kwenye maeneo yao.

Kutokana na hali hiyo, kama hawajafanya hivyo baadhi yetu basi nakuombeni mufanye hivyo kwamba ni vizuri wizara kwenye hivi sasa kuna mtaalamu ambaye alikuwa Rwanda kutoka India ambaye amefanyakazi nzuri sana Rwanda ya kuanzisha programu mbali mbali za kutoa taaluma kwa vijana wetu na hizo ni programu za wiki moja hadi mbili. Sasa anapomaliza programu zile basi vijana wale huwa sasa wanaweza kuanzisha miradi yao wenyewe na wizara kazi yao ni kuwawezesha. Kwa hivyo, ni vizuri tutumie fursa hii adhimu na mtaalamu huyo yupo pamoja na wataalamu wetu wa wizara wapo, basi tutakapokuwa tayari wakati wowote na ninakuombeni Waheshimiwa Wajumbe muwe tayari, kwa sababu wakati wenyewe ndio huu na vijana wanatuhitajia.

Mhe. Naibu Spika, jukumu hili tusiisubiri serikali peke yake kuwakusanya vijana, sote kama ni Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na viongozi mbali mbali katika maeneo tushirikiane na serikali kupitia wizara yetu pamoja na Wizara ya Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Wanawake na Watoto, ili kuhakikisha suala hili tunalisimamia kwa pamoja na tunalifanyia kazi kwa lengo la kusaidia vijana wetu.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana na mimi kunipa fursa ya kuweza kuuliza swali dogo la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ambayo Mhe. Waziri ametoa.

Mhe. Naibu Spika, katika kumbukumbu zangu mwaka 2011 tuliulizia suala hili la viwanda vya kuweza kusindika samaki hapa Zanzibar na kwa wakati ule tulijibiwa kwamba suala hilo liko mbioni na muda si mrefu litatolewa ufafanuzi, ili tuweze kupata mwelekeo wa kuona namna gani tunaweza kutumia raslimali ya bahari ambayo imetuzunguka katika visiwa vyetu vya Zanzibar.

Je, Mhe. Waziri suala hili leo limerudi tena ni lini hasa serikali itatoa mwelekeo wa kuweza kuanzisha viwanda hivi kwa sababu ya kuwasaidia vijana wetu ambao kwa sasa hawana kazi katika visiwa vyetu vya Zanzibar.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Naibu Spika, swali hili linaelekezwa kwangu ingawa si langu, isipokuwa ni la wizara inayohusika na mambo ya uvuvi. Lakini kwa bahati mimi nilibahatika kwenda Vietnam na Mhe. Rais na Waziri wa Uvuvi na Mifugo tulikuwa naye na juzi tu Mhe. Rais amekwenda China na bahati nzuri tena Waziri wa Uvuvi na Mifugo alikuwemo na nina hakika kwamba serikali imepanga mikakati mizuri.

Sasa nadhani nimuombe Mhe. Mjumbe swali hili aliandae vizuri kwa ruhusa yako Mhe. Naibu Spika, na alipeleke katika wizara inayohusika atapata jibu zuri. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, kazi yangu mimi wakeshakujiandaa wao ni kutafuta uwezo wa kuwapa fedha na kuwawezesha na wakeshakuwa tayari, basi na sisi tutakuwa tayari kuwawezesha. *(Makofi)*

Mhe. Farida Amour Mohammed: Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kumuuliza swali Mhe. Waziri lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, kuna wimbi la vijana wanaomaliza vyuo vikuu wanakimbilia Tanzania Bara kwa kufanya kazi katika sekta muhimu kama vile afya na elimu. Je, sisi Zanzibar kitaalamu tumeshajitosheleza na wataalamu hao.

Je, kama bado serikali inachukua juhudi gani kuzuia wimbi hilo la uhamaji wa vijana wetu wataalamu hapa Zanzibar.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Naibu Spika, swali hili pia lingefaa kuulizwa Wizara ya Nchi, (OR),

Utumishi wa Umma na Utawala Bora, lakini naamini kwa vile niko serikalini nitasaidia.

Kwa kweli Mhe. Rais ameanzisha Wizara hii ya Kazi, Uwezeshaji, Wananchi, Kiuchumi na Ushirika na pia suala la kuwawezesha vijana liko kwenye Wizara ya Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Wanawake na Watoto. Jambo la msingi hapa kama kuna wimbi hilo la watu kukimbia kwenda kufanya kazi serikali haijazuia kufanya hivyo.

Vile vile serikali inajitahidi kwa upande wake, safari hii kuna karibu nafasi 2552 kupitia serikali ambazo zimetangaziwa na tayari kwa taarifa nilizopata karibu 2300 wameajiriwa na wengi wao walioajiriwa ni vijana wa hapa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, pia ndipo tunaposema kwamba ajira sio lazima serikalini na wizara yetu iko tayari. Mhe. Naibu Spika, namuomba Mhe. Mjumbe kama kuna vijana ambao wamesoma basi awalete pale wizarani kwetu kuna kituo maalum cha kujiorodhesha wale wote ambao wanaomaliza vyuo vikuu, skuli za sekondari, ambao hawakubahatika kuendelea na masomo yao na pale zinapopatikana fursa kutoka taasisi za sekta binafsi, basi huwa tunapeleka vijana wale na ajira zinapatikana.

Nimesema hapa katika kipindi hichi karibu vijana 90 wamepata ajira kwa utaratibu huu. Kwa hivyo, Mhe. Mjumbe nakushauri kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, kwamba awashauri vijana hao na ninachukua nafasi hii kulieleza Baraza lako tukufu Mhe. Naibu Spika, na kutoa wito kwa vijana wote popote pale walipo ambao wamemaliza skuli basi waje pale wizarani wajiorodheshe na *Inshaallah* wakae mkao wa kupata ajira katika sekta binafsi au ikiwezekana kwenye sekta za serikali.

UTARATIBU

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Mhe. Naibu Spika, kwa sababu swali ambalo tumeliuliza linahusu mtambuka na waziri husika yupo na serikali inafanyakazi kwa pamoja kwa faida ya Wajumbe pamoja na wananchi basi tunaomba kupata jawabu ya swali hilo.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe, utaratibu wa maswali unaandika swali wizara husika. Kwa hivyo, nakuomba ujiandae na upeleke wizara inayohusika na utajibiwa, kama ingelikuwa kwenye bajeti basi angeingia waziri mwengine akajibu. *(Vicheko/Makofi).*

Tunaendelea Katibu.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, tunashukuru kwamba jana tulipata wachangiaji na leo ratiba yetu inatwambia ilikuwa hivi asubuhi tulete wachangiaji wachache, ili Mhe. Waziri Waziri aweze kufanya majumuisho. Lakini Mhe. Waziri ameomba kwa hoja nzito muliotoa majumuisho atafanya kipindi cha jioni. *(Makofi).*

Kwa hivyo, sasa ninao wachangiaji 11 waliobakia naomba twende vizuri ili tuweze kuutumia muda huu wa asubuhi. Mchangiaji wa mwanzo nampa Mhe. Salim Abdalla Hamad, ambaye alipata dakika 6 jana jioni, basi amalizie muda wake kwa dakika 15 na baadaye afuatie Mhe. Rufai Said Rufai na Mhe. Fatma Mbarouk Said.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Naibu Spika, nashukuru kwa kupata fursa hii ya kuendelea kuchangia bajeti ya Wizara ya Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea na mchango wangu katika ukurasa wa 14 kifungu cha 36 kitabu cha bajeti kinachohusiana na uangamizaji wa kunguru weusi.

Mhe. Naibu Spika, kunguru weusi wapo Zanzibar kwa miaka mingi sana, lakini wanaonekana wanaharibu mazingira na katika awamu kadhaa walikuwa wakishughulikiwa kupunguzwa kwa kuuliwa, lakini nashukuru katika awamu hii upo mpango maalum wa kupambana na kunguru hawa.

Kwanza mimi sina matatizo na mradi huu isipokuwa naomba nipatiwe maelezo kidogo. Mhe. Naibu Spika, kama nilivyotangulia kusema kwamba hawa kunguru wapo kwa muda mrefu ambapo wana hasara ndio wakaangamizwa kwa kuuliwa, lakini kuwepo kwao hapa Zanzibar lazima kuna faida fulani wailete na kulikuwa na sababu ya kuletwa hapa.

Sasa unapofanya kitu vizuri basi yale mema ambayo ukikiondoa kitu kile yatakuwa nayo yameondoka uyatayarishe. Kwa hivyo, mimi naomba kumuuliza Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, kwa vile ni mwanasayansi na anafahamu vizuri mambo haya, anajua kwamba

tukiwaondoa hawa kunguru kuna mambo muhimu ambayo walikuwa wakiyafanya kwa maslahi ya jamii yatakosekana.

Je, amejitayarisha vipi kuweka nyama mbadala au ndege ama chochote ili wawe wanafanyakazi ambayo ni muhimu waliyokuwa wakiifanya hawa kunguru ambao wanaangamizwa kwa kasi kubwa sana hivi sasa.

Jambo jengine kwa sababu kunguru hawa weusi pia Pemba wameshahamia na wapo na kule wako kunguru wenye vidoa vyeupe ambao hawajatiwa katika suala hili la kuangamizwa na kunguru hawa hawaangamizwi kwa risasi au vyovyote isipokuwa ni kwa sumu, ambapo kunguru yoyote anaweza akaila.

Je, kwa sababu hawafai kukaa katika jamii kutokana na mambo yao, watafanya rai gani ya kuwangamiza wale kunguru ambao wako Pemba weusi na wale wengi bado hawajaleta kero wakaweza kubakia kwa wakati huo huo.

Mhe. Naibu Spika, tukitizama kwenye kifungu hichi cha 36 imeandikwa kuwa katika utekelezaji wa mradi huu hadi kufikia mwezi wa Mei 2013 jumla ya kunguru 18,000 wameuliwa kwa kutumia mitego na sumu kwa mwaka wa fedha 2012/2013. Jumla ya shilingi milioni 30 ndizo zilizopatikana kwa ajili ya kufanya kazi hiyo ambayo ni sawa na asilimia 60. Sasa mambo yaliyofanyika kwa fedha hizo ni pamoja na kutengeneza mitego 6.

Kwa hiyo, hapa ninataka kujua mitego 6 hii iligharimu kiasi gani na iligaiwa vipi pamoja na kuwa imeelezwa kwamba imeenezwa sehemu mbali mbali ambazo hazijulikani na kama mitego hii na kule Pemba imefika au laa?

Vile vile kulinunuliwa dawa ambayo ni kilo moja na nusu kutoka Newzealand na kunguru walioiliwa ni 18,000 sijui dawa hii ilitosha kuulia kunguru hao au bado ipo, na kila hii moja na nusu mpaka kufika hapa iligharimu kiasi gani, je hakuna uwezekano wa kufanya dawa sisi wenyewe Tanzania kwa kupunguza gharama na kadhalika. Mhe. Naibu Spika, naomba maelezo.

Halafu kuna vifaa mbali mbali vikiwemo mabeseni, ndoo, sinia, vijiko, *gloves*, mapanga na majembe pamoja na kununua chombo cha kutumika kwenye sumu na miteko. Sasa hichi chombo cha kutumika kwenye sumu na mitego ni chombo gani nataka nikijue na kazi ya vyombo vyengine vyote hivyo, majembe, sinia, vijiko kwa ajili ya kazi gani?

Mwisho kuhusiana na kunguru kwa sababu kunguru wameonekana ni kero na ninashukuru wizara hii husika imeshakuwa na utaalamu wa kuwaua pamoja na gowa wao, lakini wameshazoea kuwaua. Kwa kweli mradi huu umeelekezwa kuwa utapelekwa katika Wizara ya Kilimo na Maliasili.

Mhe. Naibu Spika, Wizara ya Kilimo na Maliasili sijui kuwa inahusika sana na mambo haya ya kunguru wakati tunayo Wizara ya Mifugo na Uvuvi, kwa sababu hawa ni viumbe na wanaingia kwenye mifugo. Kwa hivyo, kwa nini haikuonekana ni bora kupelekwa katika Wizara ya Mifugo na Uvuvi kazi hii kwa vile ndiko kunakohusika zaidi ikapelekwa Wizara ya Kilimo na Maliasili, Mhe. Naibu Spika naomba jibu kuhusiana na hilo.

Nikiendelea na mchango wangu sasa naomba nizungumzie kuhusu madawa ya kulevya. Mhe. Naibu Spika, madawa ya kulevya ni kweli tatizo kubwa sana katika nchi hii na inazungumzwa vibaya kwamba Zanzibar ni sehemu au kituo cha kupitishia madawa ya kulevya na Zanzibar madawa ya kulevya yanatumika.

Kwanza nitoe pongezi kwa Mhe. Waziri pamoja na wizara yake pamoja na wote wale walioshirikiana kumsaidia, kwani tukiangalia mazingira yalivyo hivi sasa si kama tulivyoanza hapo mwanzo. Kwa kweli utumiaji wa madawa ya kulevya umepungua sana katika nchi yetu kwa hili napongeza sana na Mwenyezi Mungu ampe nguvu zaidi na azidi juhudi na tushirikiane naye ili balaa hili lituondokee.

Mhe. Naibu Spika, madawa ya kulevya si kwa kuwa yanatengenezwa hapa tu lakini madawa ya kulevya hasa yanatoka nje ni mtandao mkubwa tumeona kwenye semina unahitaji kazi ngumu ya kuweza kuudhibiti.

Kwa hivyo, njia kuu tunavyoelekezwa zinazopitia madawa ya kulevya ni pamoja na bandari zetu kuu, bandari za panya pamoja na uwanja wa ndege. Mhe. Naibu Spika, nashukuru kwa kazi inayofanywa ya kupambana nayo, lakini hapa kidogo naomba maelezo kuhusu uwanja wa ndege. Kwa fikra zangu Mhe. Naibu Spika, mambo kama haya ambayo ni ya hatari sana na hii ni fikra yangu mwenye kwa wale wanaohusika hutafuta njia wafanye wafanikiwe bila ya kukamatwa.

Vile vile tulijadili katika kipindi kilichopita na tukaona kuwa kwa hapa kiwanja cha ndege cha kimataifa cha Zanzibar dawa hizi huwa zinapitia kwenye Chumba cha *VIP* na tulipata pata mnong'ono huo na sijui ikawa ndio sababu katika nchi hii viongozi watano tu wangazi za juu wasipekuliwe wengine sote ikabidi tupekuliwe tunapopita kule. Kupita kwetu pengine iliweza kusaidia mpaka hali ikaweza kupungua kwa sababu panakuwa na waheshimiwa lazima mtu aliyekuwa na matatizo atazidi kujilinda na si rahisi kupitia katika njia ya kawaida, kwa sababu hiyo na ishara ya mafanikio imeonekana.

Mimi Mhe. Spika, nasikitika sana na Inshallah Mwenyezi Mungu tukijaaliwa nitakuja kuchangia katika hii wizara, sioni sababu kuwa uwanja wa ndege kuna chumba makusudio ni *VIP* na sisi ikiwa tumo tumepewa uheshimiwa na wananchi leo tukaambiwa tusipite mpaka tulipie kwa pesa zetu mfukoni, sio kuwa serikali itulipie. Ile kuonekana chumba kile kuwa sasa Waheshimiwa hawapiti na Mheshimiwa ana hadhi yake, naamini ni kuweka njia wazi kwa wale wenye uwezo na mizigo yao kupita pale na kufanya yale ambayo tunataka kuepukana nayo.

Mhe. Spika, mimi siridhiki na wala sio uamuzi wa busara kuwa mtu anajua thamani ya *VIP* akasema mnaweza mkapita kule kama wanakopita wengine, hamna shilingi ishirini. Hapa naamini pana siri ambayo haina *formular* imewekwa kwa nini tuondolewe. Ili kumsaidia Mhe. Waziri na mambo haya si kila mtu anayeingia mle kwenye makochi na kwenda zake, tunaingia kwa maslahi ya kuangalia mwenendo mzima katika nchi yetu na kumsaidia Mhe. Waziri, shilingi ishirini ziondolewe, tukae mule, tutawanyike na kadhalika, tumsaidie Mhe. Waziri vyenginevyo mpaka tupate sababu za msingi. Kwa nini tuondolewe pale kwa sababu ukiambiwa hapa usipite mpaka ulipe, ina maana ile heshima yako imebomolewa moja kwa moja ikawa sasa mambo haya yameshaanza kutia wasi wasi, ikiwekwa sehemu ile kwa sababu kila mtu anaweza akapita, kwa hivyo haya mambo yatarudi.

Mhe. Spika, tukiangalia kitabu chetu kifungu cha 92 ukurusa wa 63 kuhusu mambo haya yanayohusikana na madawa ya kulevya ni kuwa,

Kifungu cha 92 " Tume ya Kuratibu na Kudhibiti madawa ya kulevya ina majukumu yake ikiwa moja ni:

1. Kuratibu mapambano dhidi ya biashara, matumizi, uingizaji na usafirishaji wa dawa za kulevya.

2. Kutoa taaluma kwa jamii pamoja na kutoa taaluma kwa jamii pamoja na kutoa ushauri nasaha kwa watumiaji wa dawa za kulevya."

Katika kufanya kazi zao imefanikiwa nashukuru sana na katika kuyatafuta madawa ya kulevya, ukurasa wa 34 kifungu kile cha 96 imeelezwa kuwa wapo watu 22 katika watu 22 hawa 21 ni wanaume na mmoja ni mwanamke, wana kesi mahakamani zinazohusiana na madawa ya kulevya. Lakini kesi zilizokuwepo ni 21 na waliokamatwa ni 22. Nikitaka kujua huyu mmoja

kaonekana kwamba sio madawa ya kulevya, kadhaniwa tu au bado mazingira yake ya kuingizwa Mahakamani hayajafikia.

Mhe. Spika, nikitaka kujua kwa mwaka huu wa fedha tunaomaliza ni watu wangapi waliokamatwa, wangapi wametiwa hatiani na wangapi wamesameheka. Wizara kama wizara inachukua mkazo gani wa kuona kuwa hukumu zinakwenda ipasavyo. Nasema hivyo japo kuwa Mahakama tumeambiwa iko huru lakini watu wasingeliweka mawakili kuona kwa kweli hii hukmu inakwenda ipasavyo au rushwa inatoka ndio mambo haya yakaendelea, kwa sababu bado madawa ya kulevya yanaingia.

Mhe. Naibu Spika, jengine kesi hizi mpaka hivi sasa imechukua muda gani wakati sheria zimetungwa na nzito na ilikuwa ni ya hukumu ya hapo kwa hapo, mtu akikamatwa au shughuli ziendelee ili hukumu itoke mapema.

Mhe. Naibu Spika, ninalopenda kuzungumza ni kuwa katika malengo ya mwaka huu ya fedha ya 2013/2014, Wizara imejipangia malengo yake. Lakini kabla ya kusema hayo malengo, ukiangalia ukurasa wa 34 Kifungu Nam. 93 ya kitabu hichi cha bajeti kimeeleza kuwa,

"Sehemu ya kuratibu na udhibiti wa madawa ya kulevya ilijipangia malengo yafuatayo:

1. Kuratibu na kuendeleza mapambano dhidi ya uingizaji na usafirishaji wa dawa za kulevya.

2. Kuimarisha mazingira mazuri ya kazi katika kuleta ufanisi.

3. Kuongeza muamko wa jamii juu ya athari na udhibiti wa dawa za kulevya.

4. Kuratibu na kuimarisha juhudi za taasisi katika kushughulikia mapambano dhidi ya dawa za kulevya".

Lakini Mhe. Naibu Spika, hayo ndiyo malengo yaliyojipangia ukenda ukiangalia kifungu cha 102 ukurasa wa 36 ambacho kinaeleza kuhusu malengo kwa mwaka huu fedha wa 2013/2014. Ukilinganisha na yale ya 2012/2013, malengo yaliyopo ni kupunguza matumizi ya dawa za kulevya, kupunguza uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa dawa za kulevya. Tukisema kupunguza matumizi maana yake labda hii hali kidogo inatofautiana na huku nyuma ilikuwa kuna mapambano na mimi nilifikiria kwamba mapambano yataendelea. Unapofanya kitu ukapata mafanikio maana yake uongeze ile juhudi. Ikiwa hapa ni kupunguza basi sijui inaonekana

kwamba haya madawa ya kulevya hayana athari kubwa sana hivi sasa mpaka iwe tupunguze tu na kwa nini tusipambane. Nataka nipate maelezo.

Mhe. Naibu Spika, kupunguza usafirishaji, uzalishaji na usambazaji wa dawa za kulevya. Mimi hapa jambo linalonisikitisha tukisema tupunguze usafirishaji ni kama tunajifunga kuwa sisi hapa tunasafirisha. Kwa hivyo hii kasi tunaipunguza. Tukisema tupunguze uzalishaji ina maana na sisi pia tunazalisha na tukisema tupunguze usambazaji wa hii kazi pia ina maana kwamba tunaifanya na sisi tunazalisha. Kwa nini tusiandike kupambana na matumizi ya dawa za kulevya, kupambana na usafirishaji, uzalishaji na usambazaji wa dawa za kulevya au kuendelea kupambana kwa sababu kazi hii imeshaanza tokea kipindi hichi cha bajeti kinachomalizan na hapo naomba nipate maelezo.

Moja kwa moja Mhe. Naibu Spika, tukitoka hapo sasa nitaingia ukurasa wa 64 wa kitabu hiki na ukurasa huu unaeleza kuhusu namna Wizara yetu inavyoshughulikia nyumba za kurekebisha tabia walioacha dawa za kulevya zilizopatiwa ruzuku. Hapa walioacha dawa za kulevya mimi nafikiri tungeliandika walioachana na utumiaji wa dawa za kulevya. Ukiangalia tukisema nyumba hizi zilizopatiwa ruzuku ina maana kuna nyumba nyengine kama hizi hazikupatiwa ruzuku na kuwa na sababu zozote ambazo Mhe. Waziri atatueleza. Lakini mimi kwa hili nikitaka nijue ni kigezo gani kilichotumika mpaka katika kisiwa cha Unguja zikapatiwa ruzuku za shilingi milioni moja na laki tano kwa kila nyumba kwa nyumba saba na Pemba ikawa ruzuku kama hiyo kwa nyuma mbili tu. Nikitaka kujua kwa vile Unguja kuna *sober house* ya wanawake Nam. 4 pale imeandikwa. Je, Pemba hakuna wanawake wanaotumia madawa ya kulevya mpaka leo. Ikiwa wapo mbona hatukuona kuwa ipo *sober house* ya wanawake kule Pemba. Hizi milioni moja na laki tano kwa ruzuku kwa kila nyumba ni kwa shughuli gani, kodi ya nyumba, chakula au kwa maendeleo.

Hizi milioni moja na laki tano kwa ruzuku kwa kila nyumba ni kwa shughuli gani kwa kodi ya nyumba, chakula au kwa maendeleo. Kwa sababu hawa watu walikuwa wanatumia madawa ya kulevya na wameacha kutumia madawa ya kulevya. Mimi nawapongeza sana kwa sababu nilitembelea moja katika hizi *sober house* iliyoko Nyarugusu. Kule tulikutia watu ambao walikuwa wataalamu kweli kweli lakini walikuwa wanajihusisha na madawa ya kulevya na sasa wamekuwa ni walimu kwa wenziwao, wamefanya kazi kubwa sana.

Kero la watu hawa kutokana na kile kitendo walichokuwa nacho sasa hivi wengine wapo tayari kurudi nyumbani, lakini ile hali ya mazingira waliyokuwa nayo hivi sasa wakenda kidogo inatisha tisha. Kwa vile hawa

tayari wamefanya jambo la maana sana kweli kweli kwa maslahi yao na maslahi ya taifa. Kwa sababu Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika haioni kuwa Mhe. Waziri sasa hivi iwe bega kwa bega kwa sababu yeye ndiye anayetoa misaada kwa vikundi mbali mbali. Hivi ni vikundi wakati mnakaa kwenye majumba vipatiwe msaada wa kujiendeleza ili tuthamini ule uamuzi wao wa kuona kuwa sisi ni bora kuacha madawa ya kulevya na wakaweza kuwafahamisha wenzao na kazi inaendelea vizuri.

Mhe. Naibu Spika, kwa sababu ya wakati na si kwa sababu ya kuchangia naomba tena kama nilivyoomba jana Mhe. Naibu Spika, kazi ya wizara hii ni ngumu sana, wanapambana na walevi, Ukimwi, mazingira machafu, majani na kadhalika. Ni kazi ngumu sana na bahati mbaya kila kazi ina Wizara yake. Naziomba Wizara husika ziisaidie wizara hii ili malengo yaliyokusudiwa yaweze kufikiwa. Mhe. Nibu Spika, nakushukuru.

Mhe. Rufai Said Rufai: Ahsante Mhe. Naibu Spika, awali ya yote na mimi sina budi nimshukuru Allah kwa asubuhi hii kutujaalia kupata nafasi ya kuchangia hoja iliyokuwepo mbele yetu hotuba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais.

Mhe. Naibu Spika, mimi sina budi kumpa hongera kubwa sana Mhe. Waziri kwa umakini wake alioufanya jana hapa kutuwasilishia hotuba hii kwa uangalifu mkubwa na umahiri mkubwa.

Mhe. Naibu Spika, mimi niende moja kwa moja katika hotuba hii kwenye ukurasa 12 kifungu cha kuanzia 30, kinaelezea mradi wa kuimarisha usimamizi wa mazingira na kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi. Hili ni suala moja kubwa katika nchi yetu ambayo imekumbwa sana na mabadiliko ya tabia nchi. Kama Mhe. Waziri alivyoeleza hakutakuwa na mashirikiano baina Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Ofisi ya Fedha, Uchumi, Mipango na Maendeleo, Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati, pamoja na Wizara ya Kilimo, basi kwa Ofisi ya Makamu wa Kwanza tu basi suala hili litakuwa ni tatizo moja zito sana kuweza kupambana na mabadiliko haya ya tabia nchi.

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli visiwa vyetu vya Unguja na Pemba limefikwa na janga hili kubwa lakini hasa kisiwani Pemba. Ndani ya Pemba na jimbo langu la Tumbe limeathiriwa sana na haya mazingira ya tabia nchi, hasa ukanda wa Kusini Mashariki na Mashariki Kaskazini. Maeneo haya yameathirika vya kutosha kabisa na Mhe. Waziri ni shahidi kwamba niliwahi kumuandikia barua kuja kuyaangalia maeneo hayo. Nashukuru kwamba barua yangu aliijali na kazi ile akaifuatilia vya kutosha kabisa.

Mhe. Naibu Spika, mazingira haya ya tabia nchi mabadiliko tunayoyapata kwa kweli imefikia pahali wananchi wetu wamekosa maeneo ya kujiendeleza kimaisha hasa kilimo cha mpunga. Nashukuru juzi Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais alitaja kwamba katika mfuko ule wa TASAF wametujengea tuta moja pale Sizini, tunashukuru, kiasi fulani wananchi pale wameanza kupata mabonde ya kuweza kulima mipunga yao. Lakini Mhe. Spika, maeneo hayo niliyokutajia ukanda wa Mashariki ya Kusini na ya Kaskazini wananchi wengi wamekosa kuweza kupata kilimo hichi cha mpunga na kuendeleza maisha yao.

Mhe. Naibu Spika, ukianza pale Tumbe bandarini mabadiliko haya yamechukua nafasi kubwa sana, mabonde yaliyokuwepo pale hivi sasa wananchi hawapati tena kulima mipunga. Lakini cha kusikitisha Wizara ya Mifugo na Uvuvi wanapojenga lile soko pale walikuja wakachimba msingi kupeleka kule baharini na huku maji ya chumvi tayari yana njia nyengine yanapita katika maeneo yale kuingia katika maeneo ya mabonde ya watu wanayolima mipunga. Sasa msingi ule ukachangia zaidi kuyafanya maji ya bahari yawe na kasi zaidi kuingia katika maeneo haya ambayo wananchi wanayojipatia riziki zao. Kwa hivyo hili tatizo limekuwa sugu, limekuwa kubwa mno. Ningelimuomba sana Mhe. Waziri ashirikiane na hizi wizara ambazo nimezitaja, kutafuta ufadhili popote duniani ili kulinusuru janga hili wananchi wetu waweze kufaidika na vile vilimo vyao wanavyolima.

Lakini pia Mhe. Waziri ni shahidi nilikwenda katika bonde lile la Kwapape. Huku ni eneo moja mno la wananchi wanaojipatia rizki zao lakini mashaka haya ya mabadiliko ya tabia nchi yamelichukua eneo hilo karibuni nusu na robo. Kwa hivyo wananchi wa Kinowe kule hawapati kuendeleza kilimo ili kuweza kupambana na hali ngumu hii ya maisha tuliyonayo. Ningemuomba sana Mhe. Waziri suala hili wakati atakapokuja kujibu angalau aje atupe maelezo ni hatua gani serikali wamechukua. Kwa sababu toka kwenda nao katika maeneo haya karibuni inafika mwaka mmoja, angalau niweze kujua serikali imechukua hatua gani kuhusu mabadiliko ya tabia nchi katika maeneo haya ya jimbo langu la Tume na maeneo mengine katika Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, nikiondoka hapo niende katika ukurasa wa 22 kifungu cha 57 mpaka 64, lakini nitakapozugumza mimi ni suala zima la Idara hii ya Mazingira. Katika kifungu hichi Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri alitoa ufafanuzi baina ya Idara ya Mazingira ilijipangia kutekeleza, malengo yafuatayo, katika malengo sita yaliyopo mimi nataka nizungumzie baadhi tu ya maeneo mawili Nam. 4 na 5. Naomba ninukuu.

Kifungu cha 57	"(4) Kuongeza uwelewa wa elimu ya mazingira kwa jamii na wadau wengine."

Mhe. Naibu Spika, hili ni jambo la maana sana kwa sababu kila kitu kinahitaji elimu, bila ya elimu hakuna jambo lolote ambalo litakuwa. Elimu ni ufunguo wa maisha na watu wanaendela kuharibu mazingira kwa mambo mawili tu Mhe. Naibu Spika, ima moja ni kutokana na kukosa elimu, la pili ni kutokana na hali ya ngumu ya maisha katika baadhi ya maeneo. Kama wananchi wetu hatukuwapa taaluma basi mazingira yataendelea kuchafuliwa. Kutokana na hali ngumu ya maisha watu wanakata miti ovyo, watu wanachimba mchanga ovyo, watu wanachimba mawe maeneo ambayo hayahusiki kuchimba mawe ovyo. Tatizo ni ukosefu wa elimu au ni hali ngumu ya maisha.

Mhe. Naibu Spika, Waswahili wansema kwamba njaa haialiki mwari, kwa hali yoyote utastahamili na njaa siku moja, ya pili, ya tatu utatoa maamuzi kama ni kwenda kuchimba mchanga, kukata miti, kuchimba mawe au kumuibia mtu mwengine. Lakini kwa hali yoyote maamuzi yatapatikana. Kwa hivyo ili kuwanasua wananchi wetu katika huu uharibifu wa mazingira basi panahitajika elimu ya kutosha. Lakini pia mtu utakapomtoa katika eneo fulani kama hapa anaharibu mazingira humwambii tu kwa maneno ikawa hali hiyo imekwisha hapana, unamtafutia utaratibu mwengine ili wa kuweza kuendelea na kuweza kuishi katika maisha yake. Lakini tukiwaambia tu wanaharibu mazingira Mahakamani faini lakini muelekeze ili aweze kupata kuishi katika maisha yatakayokuwa ni bora. Kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, kama hatutokuwa na mabadiliko ya kuwataka wananchi wetu baada ya kuacha kuchafua mazingira lakini fanyeni haya ili muweze kuendeleza maisha basi uharibifu wa mazingira bado utaendelea zaidi na zaidi. Kwa hivyo tuwatafutie mipango endelevu ambavyo yataweza kupambana na ugumu huu wa maisha.

Lakini pia Mhe. Waziri alisema kwamba kuimarisha utekelezaji wa sera, sheria na kanuni za mazingira. Sasa hata wewe Mhe. Naibu Spika, nimeshangaa kwa kiasi fulani suala hili tokea uingie uharibifu wa mazingira ni muda mrefu, kama kwamba ndio kwanza Mhe. Waziri anatwambia anataka kuimarisha utekelezaji wa sera, sheria na kanuni. Ah! huu muda umeshakuwa mrefu sana na kama Mhe. Waziri kutwambia kwamba unataka kuanza sasa kuimarisha kwa kweli tumechelewa, wananchi hawatusubiri sisi, wananchi wanaendelea na kazi zao.

Sasa katika kuimarisha kwako basi ni vyema haya mambo uyarahisishe yakafika Barazani kwa zile sheria ili zikaweza kupewa nguvu na wewe ukapata meno ya kuendeleza suala hili. Lakini kama itakuwa unaimarisha tu lakini hazifiki hapa kwa kweli kazi hii itakuwa ni ngumu kwako pamoja na wizara yako kwa jumla. Ningelikuomba sana haya mambo ukayaharakisha ili yakafika hapa na yakaweza kupata baraka ili hii kazi ikaweza kwenda vizuri.

Mhe. Naibu Spika, nikenda katika ukurasa wa 37 kifungu cha 104 pale kuna Tume ya Ukimwi. Suala hili la Tume ya Ukimwi wenzangu wengi wamelichangia na mimi naungana nao katika suala hili la Ukimwi. Tulipata semina moja tukaambiwa kwamba kama sijasahau, Ukimwi hapa Zanzibar aliyeanza kuonekana mtu wa mwanzo mwaka 1984 kama sisahau. Lakini mpaka tunakabidhiwa kitabu hichi jana tuna asilimia 1.0, hao ni watu wengi kwa nchi yetu ilivyo. Asilimia hiyo ni kwa wale waliopita katika njia za hospitali naamini kwamba asilimia hii kuna uwezekano ikaongezeka ikawa kubwa kulikoni hapo Mhe. Waziri alivyotuandikia habari hii.

Mhe. Naibu Spika, Tume ya Ukimwi mimi naona kwamba haifanyi kazi ya kudhibiti ukimwi na kupunguza ongezeko la Ukimwi bali ni mradi wa kuwafanya watu wa Tume ya Ukimwi ili waendelee kupata mapato na kujiendeleza katika shughuli zao nyengine. Kama ingelikuwa suala hili wanadhibiti tusingelitoka mtu mmoja mpaka sasa hivi tukafika asilimia 1.0. Halafu mambo mengi yaliyoelezwa kwenye semina sio kuwaelimisha wananchi hasa tuliposomewa katika hotuba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais inasemi kuwa watapewa semina wafanyakazi. Mimi nahisi kwamba wafanyakazi ni watu wenye taaluma. Ikiwa wafanyakazi ni watu wenye taaluma lakini kuna wananchi wetu si wafanyakazi wala hawana taaluma ndio wakupewa semina. Ina maana pesa hizi zinazunguka hapa hapa serikalini tu, maidarani, mawizarani wale wananchi wanyonge ambao hawana taaluma ya aina yoyote hakuna, mafunzo, hakuna chochote isipokuwa linaloendelea ni ile kuongezeka kwa Ukimwi. Hapa itakuwa hatujawafanyia la maana Wazanzibari waliokuwepo katika nchi hii.

Mhe. Naibu Spika, ukimwi bado Wazanzibari tunaupalilia uzidi kuendelea na watu waweze kujaza matumbo yao na huku wananchi wetu wakipata gonjwa ambalo linasababishwa na wengine hata hawajakusudia kufanya matendo yale ili liweze kupatikana. Kutokana na urahisi tulionao Zanzibar kutokana na sheria tulizoziweka hapa tunafuata zaidi utandawazi wa Magharibi, tukajisahau kwamba Zanzibar tuna sheria zetu. Lakini leo hii tunashuhudia sote si wanawake si wanaume, watu wanakwenda uchi wa mnyama. Hivi sasa ukitoka barabarani ukiangalia asilimia ya vijana suruwali zao ziko nusu ya uchi zinaning'inia. Hilo ni chimbuko la kuupata Ukimwi. Ukiangalia ndugu zetu wanawake nguo zao ni fupi mno, kitu kibaya sana kuona ukishakuona akili itafanya kazi.

Kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, ni lazima turejee katika sheria zetu za Zanzibar ambazo tunazo. Suala hili ili liweze kuondoka basi tufuate taratibu za nchi, lazima wanawake wanaume tuvae nguo zetu vizuri. Lakini pia Mhe. Naibu Spika, haya mabaa yaliyoenea katika nchi yetu ya Zanzibar, kumbi za starehe zilizoenea na haya yote yanachangia suala hili, lakini tunayanyamazia,

tunaambiana kwamba tusanyanyapaane, haya kama tusinyanyapaane lakini na Ukimwi utakuja juu zaidi, kama si mimi ni wewe. Kwa hivyo tujitahidi sana kusimamia suala hili ili wananchi wetu watoke na janga hili baya la Ukimwi ili waweze kujenga afya zao na jamaa zao na maeneo yao.

Mhe. Naibu Spika, nakuona kwamba unataka unambie kwamba muda wangu umeshamaliza, lakini nakuomba kidogo unipe nafasi kidogo nimalize.

Mhe. Naibu Spika, nizungumzie Idara ya Watu wenye Ulemavu kidogo tu. Hapa Mhe. Naibu Spika, katika kitabu cha Mhe. Waziri kwenye viambatanisho huku nilipata shaka tu kidogo naomba aniweke sawa kiambatanisho nambari 6 ametueleza kwamba kuna Wilaya hapa amezichambua. Lakini kila nikihesabu Wilaya za hapa Zanzibar hazifiki idadi yake nimekuta kama kuna Wilaya nane. Sasa Wilaya ya Kaskazini A na Wilaya ya Kaskazini B jawabu lake sijaliona wao wana kiasi gani cha watu wenye ulemavu. Naomba hapa nipate maelezo ili na wao tujue kama wenzetu hawana walemavu basi niwape hongera sana. Mwenyezi Mungu awajaalie watokane na majanga haya mbali mbali ya ajali zinazotokea na mambo mengine na wale waliozaliwa kimaumbile, awajaalie wasiwe na watu kama hawa. Lakini kama Wilaya hizi na wao pengine wapo ni kipi kilichoonesha kwamba hakuna takwimu yao katika hotuba hii.

Mhe. Naibu Spika, ninashukuru sana kuniachia muda wako huu, kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Tumbe naunga mkono hoja.

Mhe. Fatma Said Mbarouk: Ahsante Mhe. Naibu Spika, na mimi kwanza nimshukuru Mungu Subhana Wataala kwa kuniwezesha kuamka leo nikiwa mzima na kuja katika kazi ambazo nimeziomba kwa wananchi wangu wa Jimbo langu la Amani.

Mhe. Naibu Spika, nichukue fursa hii kumshukuru Mhe. Waziri kuleta hotuba yake hii, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, niseme kwamba nimshukuru sana kwa kuiwasilisha kwetu sisi Wajumbe wa Baraza hili tukufu na vile vile niwashukuru pamoja na watendaji wake akiwemo Katibu wangu Mkuu Dr. Omar Dadi Shajak ni watu niseme *committed* kabisa na nishukuru kwa kumpa msaada mkubwa sana Mhe. Waziri Fatma mwenzangu hapa ambaye tunalingana mpaka majina, kwa hivyo nishukuru kwa hilo.

Mhe. Naibu Spika, nikianza na hotuba yake Waziri nakwenda ukurasa wa 19 Idara ya Uendeshaji na Utumishi. Kwa kweli Mhe. Naibu Spika, idara hii ina majukumu ya kusimamia raslimali watu na utawala na masuala ya nidhamu uwajibikaji, mafunzo na stahiki za wafanyakazi. Lakini hapa katika Idara hii

kuna malengo ya mwaka imejipangia kutekeleza malengo yafuatayo kwamba ni kusimamia majukumu ya utendaji wa wafanyakazi, kuimarisha mazingira na utendaji wa kazi, kuwajengea uwezo wafanyakazi na kuwapatia maslahi, kukuza na kuimarisha mawasiliano ya habari, kusimamia utaratibu wa udhibiti wa matumizi ya fedha.

Kwanza nishukuru kwa kuyaona malengo haya na hasa hili la kusimamia na kuratibu udhibiti wa matumizi ya fedha kwani hili ni tatizo kubwa ambalo linakuwa linatukabili katika sekta mbali mbali. Lakini vile vile kwenye malengo hayo hayo kwa mwaka wa 2013/14 nimeona kwamba kuna moja hili ambalo la kusimamia majukumu ya utendaji wa wafanyakazi limepunguka, kulikuwa na mapungufu hapo kwa mwaka ujao. Sasa nimuulize tu Mhe. Waziri hili la kusimamia majukumu na utendaji wa wafanyakazi limefanikiwa kiasi gani hata kwa 2013/2014 halikuwemo.

Vile vile Mhe. Naibu Spika, kuna ukurasa hapa nimeukiuka kidogo wa 17 ambao Mhe. Waziri ametuwasilishia hapa kwamba kuna miradi ya maendeleo ambayo mradi mmoja wa maendeleo ni mradi wa kuendeleza elimu ya mazingira. Vile vile kuna mradi wa ujenzi wa Kituo cha tiba na marekebisho ya tabia ya utumiaji wa dawa za kulevya ambazo pesa hizi, mradi huu wa kujenga kituo cha kurekebisha tabia ya watumiaji wa dawa za kulevya unatarajia kutumia fedha ya serikali ambayo ni shilingi milioni 100 na vile vile mradi wa kuendeleza elimu ya mazingira ambayo itatumia fedha za serikali vile vile milioni 50 na kuna mradi mwengine wa kuimarisha usimamizi wa mazingira kukabiliana na mabadiliko ya tabia ya nchi ambayo fedha zake unategemea fedha za wahisani na vile vile mradi wa kujenga uwezo wa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, vile vile mfuko huu unafadhiliwa na Wizara ya Fedha.

Kwa hivyo mimi niipongeze miradi hii na kwa sababu ni miradi ambayo inahitaji fedha kwa hivyo lazima fedha zile zitumike kama nilivyosema kama zitumike kwa kutumia sheria za fedha na kwa sababu ni miradi muhimu kabisa na hasa mradi huu wa kusimamia mazingara. Nimepata faraja kidogo kusikia kwamba kuna mpango wa kupanda miti ambao hii *urban forest* ambayo itasaidia kuleta vivuli na kupunguza ongezeko la hewa ambayo inasababisha kuleta mabadiliko ya tabia ya nchi. Kwa mujibu wa tafiti ni kwamba Pemba kule kumeathirika sana na maji Chumvi yanaingia katika maeneo ya kilimo. Kwa hivyo nimuulize tu Mhe. Waziri mikakati gani ambayo inachukuliwa kuwasaidia wananchi hao ambao mashamba yao sasa yameingiwa na maji ya chumvi.

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli Idara Mazingira ni muhimu sana lakini vile vile nikenda sehemu nyengine ya kitabu chake hiki Mhe. Waziri niende ukurasa

wa 28, hapa anasema kuna jumuiya ya watu wenye ulemavu imepatiwa ruzuku ya shilingi 1,700,000 kwa kila kikundi lakini hiyo iko kila jumuiya. Je, nimuulize Mhe. Waziri atakapokuja hapa kwamba mpango huu utakuwa ni endelevu kwa sababu kama wamewapa kwa kipindi kilichopita basi wanastahiki tena kuwa kila mara ili kuwaondolea matatizo wana jamii hii ni kuwapa uwezo pale inapohitajika.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea na mchango wangu niende ukurasa namba 31 ambayo Mhe. Waziri amesema kwenye Ofisi ya Makamu wa Rais kwamba katika kusimamia na kuratibu utekelezaji shughuli za Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais Pemba elimu juu ya athari ya dawa za kulevya ilitolewa katika skuli za sekondari. Niulize tu kwa sababu na wao wamo katika jamii ya watu wenye ulemavu, dawa za kulevya je hii katika kusimamia na kuratibu utekelezaji wa shughuli za Ofisi za Makamu wa Kwanza wa Rais Pemba elimu ya athari ya dawa za kulevya ilitolewa katika skuli mbali mbali. Je, niulize elimu hii pia inatolewa kwa watu wenye ulemavu pia huko Pemba inatolewa.

Vile vile Mhe. Naibu Spika, na mimi vile vile nimepata utata kama walivyokwisha kusema wenzangu na wamenifilisi kidogo kwenye malengo kwa mwaka 2013/2014 kupunguza matumizi ya dawa ya kulevya, kupunguza usafirishaji, uzalishaji na usambazaji wa dawa za kulevya. Kwa kweli na mimi hapa nimejenga hofu kidogo kusikia maelezo haya kwamba kupunguza usafirishaji, uzalishaji na usambazaji wa dawa za kulevya. Kwa hivyo hii imenitia hofu kidogo kiswahili hiki ambacho kimeingia katika kitabu hiki.

Vile vile Mhe. Naibu Spika, niseme kwenye matatizo haya ya uongezeko la ukimwi kama walivyokwisha kusema wenzangu kwamba najua Wizara ina mkakati wa kupunguza maambukizi, lakini bado Wizara hii ina lazima iwe na *co-ordination* na Wizara mbali mbali au Ofisi mbali mbali ikiwemo Wizara ya Afya, Wizara ya Kilimo na hata Wizara ya Fedha. Kwani sasa hivi nakubaliana na Waziri kwamba wana mkakati lakini bado maambukizi yapo mengi na sasa kila Shehia ukitizama basi utawakuta kuna walioambukizika na matatizo na ni kutokana kama alivyokwisha kusema mwenzangu Mhe. Rufai hapa kwamba sasa hivi starehe zimekuwa ni nyingi na hasa mitaani huko kwamba kuna majumba ya starehe na watoto wetu na vijana wetu kwa kweli wanashawishika na mambo hayo. Kwa hivyo ni lazima huu mkakati Mhe. Waziri ningemuomba basi kwanza watizame ni tatizo gani ambalo linazidisha uongezekaji wa virusi hivi vya ukimwi.

Kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo kwa sababu mengi wenzangu walikwisha kuyachangia na sioni vizuri kuwa narejea rejea mambo yale yale

na kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Amani niunge mkono hoja asilimia mia kwa mia. Ahsante.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kuzungumza machache juu ya bajeti hii lakini pia nichukue fursa hii kumpongeza sana Makamu wa Kwanza wa Rais na nimpongeze Mhe. Waziri katika Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais pamoja na watendaji wake wote, kwa kazi nzuri ambayo wameweza kuifanya.

Mhe. Naibu Spika, kabla sijaanza kuchangia nilitaka niseme maneno mawili, matatu. Kwanza nilitaka niseme ujinga huwa unakuwa wakati wa kwenda lakini wakati wa kurudi njia unakuwa ushaijua. Lakini pia bubu hutaka kusema mambo yanapomzidia. Mhe. Naibu Spika, mimi nimshukuru sana Makamu wa Pili wa Rais alivyokuwa akifanya majumuisho yake kwa kuvunja ule ukimya wake. Hii naona itapelekea wajumbe kuwa katika muelekeo mzuri ambao tulipaswa.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kwisha kusema hayo naomba nianze mchango katika ukurasa wa 17 ambapo unaelezea elimu ya mazingira. Mhe. Naibu Spika, mimi niiombe tu serikali kwamba suala hili la kutoa elimu juu ya mazingira ni suala ambalo linaweza likaleta manufaa makubwa kwa wananchi wetu kwani makosa mengi huwa tunayafanya pengine bila ya kujua tunachokifanya. Kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, mimi nimuombe Mhe. Waziri elimu hii iwe endelevu kwa sababu ya manufaa ya wananchi wetu na pia niiombe serikali kufuatilia kwa kina kwa sababu tunatoa elimu nyingi, lakini pengine baadae tunaishia njiani huwa hatufuatilii kwa kina na mipango yetu huwa inaharibika. Kwa hivyo niiombe elimu hii iwe endelevu lakini pia iweze kufuatiliwa ili Wizara iwe inapata kufanya tathmini na kuweza kuona vipi imeweza kufanikiwa.

Mhe. Naibu Spika, nende katika ukurasa wa 37 kwenye Tume ya Ukimwi. Waheshimiwa wenzangu wamesema mengi juu ya hili na mimi naungana nao kwa sababu ukimwi ni janga la kitaifa au la kimataifa na unaendelea kutupoteza siku hadi siku. Kwa hivyo Mheshimiwa mimi labda nichukue fursa hii kuwaomba viongozi wenzangu ambao tumo katika ukumbi huu, lakini pia niwaombe wananchi wa Zanzibar kwamba ukimwi hautakwisha kwa semina nyingi, wala ukimwi hautakwisha kwa kuimbwa sana, wala hautokwisha ukimwi labda kwa kutunga mashairi mengi, isipokuwa ukimwi utaondoka kwa kufuata maadili ambayo tumeamrishwa na Mwenyezi Mungu hasa ukitilia mkazo kwamba tuliache kabisa suala la zinaa. Hili litapelekea tukijiandaa kuwayawacha yale mabaya na machafu yote basi huu ukimwi Mwenyezi Mungu anaweza akatuondoshea.

Mhe. Naibu Spika, katika suala hili zima la ukimwi tunatumia fedha nyingi sana. Hili mimi naomba serikali izingatie wakati fedha hizi zingeweza kusaidia mambo mengine kwa sababu fedha tunazitumia lakini hali inazidi kuwa mbaya, imekuwa sasa kama huo ukimwi tunaununua. Niombe fedha hizi tuzipunguze ili zitumike katika mambo mengine ziweze kusaidia.

Mhe. Naibu Spika, niende ukurasa wa 27 ambapo kuna Idara ya Watu wenye Ulemavu. Hapa pia mimi sitaki niseme sana ili nikachukua muda wako niseme wenzangu wamezungumza vya kutosha juu ya suala hili. Kwa hivyo mimi nimuombe Mhe. Waziri kuyazingatia yale ambayo wameyasema wenzetu kwa kuwatekelezea haki zao hao wenye ulemavu kwa sababu mlemavu ni mtu yeyote. Mtu yeyote wakati wowote anaweza akawa mlemavu, kwa hivyo lazima hili tulijali sana.

Mhe. Naibu Spika, niende katika ukurasa wa 33 ambapo kuna Tume ya Kuratibu na Kudhibiti Madawa ya Kulevya. Mhe. Naibu Spika, kwenye Tume hii mimi niseme labda kazi yake kubwa kuratibu lakini tukenda katika udhibiti, maana yake bado haijaweza kufanikiwa juu ya suala hili. Dawa za kulevya ni tatizo kubwa sana na mimi najiuliza hawa waleta unga labda wao wana udogo wa kiasi gani ikawa wao hawawezi kuonekana kwa sababu hata yule mdudu wa malaria tukimuangalia kwenye *microscope* tunamuona. Sasa hawa wao nasikia kila siku hawaonekani, hawajulikani, hawapatikani au wao labda ni majini wanatuona wao, sisi hatuwaoni. Hili ni tatizo na tatizo hili ni kubwa hasa ukiangalia tatizo hili linawakumba vijana wetu na wao ndio nguvu kazi ya taifa letu.

Mhe. Naibu Spika, wao ndio wanaoweza kuingia katika mkumbo huu wa madawa siku hadi siku vijana wetu wanaathirika na tutakosa viongozi wa kuja kurithi nchi hii baadae.

Mhe. Naibu Spika, mimi nimuombe Mhe. Waziri kwa kuwa kuna vijana ambao tayari wamejikubalisha wao wenyewe kwa hiari zao kuacha madawa haya na tunawaombea Mwenyezi Mungu awape nguvu juu na imani hiyo waweze kuacha kweli kweli ili tupate watoto wetu waje watusaidie baadae. Niwaombe sana wale vijana walioko katika *Sober House* ambapo serikali inawasaidia lakini mimi bado nilitaka niseme serikali iongeze kuwasaidia kwa sababu iwape mitaji wakati ule wa kutoka waweze vijana hawa kujishughulisha na chochote, vyenginevyo vijana hawa watakapotoka pale wakawa hawana kazi ya kufanya basi wanaweza kukata tamaa na wakarudia kule kule walikotoka. Kwa sababu wakianza tu kutoka mle hata wale wazazi bado wanakuwa hawajawaamini vya kutosha jamii inakuwa imewatenga. Serikali bado isiwatenge vijana hawa iweze kuwathamini na kuwapa mitaji waweze kujishughulisha.

Mhe. Naibu Spika, mimi niende katika vifungu ili na mimi Waziri atakapokuja aweze kunitoa wasi wasi juu ya vifungu hivi. Nende katika kifungu 220500 vifaa vya kuandikia. Mwaka 2012/2013 hapa ilionekana kuna 3,243,000 lakini mwaka 2013/2014 kunaonekana kuna 13,925,000 mimi ningetaka ufafanuzi.

Lakini pia niende katika Tume ya Ukimwi kuna ada ya ushauri kifungu 220509 ambacho mwaka 2012/2013 ilionekana kuna milioni tano lakini mwaka 2013/2014 kunaonekana kuna milioni thathini. Pia hapa mimi ningeomba ushauri.

Pia katika ukurasa wa 98 katika kitabu hiki cha vifungu kuna sera na sheria 2012/2013 kuna milioni tano lakini 2013/2014 kuna milioni ishirini na tano. Ningeomba Mhe. Waziri atakapokuja uweze kunipatia ufafanuzi wa vifungu ili na mimi niridhike niweze kuipitisha bajeti hii ya serikali kwa manufaa ya wananchi wa Zanzibar.

Baada ya kusema hayo naunga mkono hoja kwa asilimia 100.

Mhe. Mgeni Hassan Juma: Ahsante Mhe. Naibu Spika, na mimi kunipa nafasi hii kuweza kuchangia hotuba ya Waziri wa Nchi, katika Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais. Awali ya yote kwanza nimshukuru Subhana Wataala ambaye ametujaalia leo kuja hapa tukiwa wazima wa afya na kuendelea na shughuli zetu ambazo tumejipangia.

Mhe. Naibu Spika, kwanza vile vile nachukua fursa hii adhimu kumpongeza sana Waziri kwa hotuba yake ambayo kwa kweli ni nzuri naweza kusema kusema kwamba ni *very efficient* lakini vile vile napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru sana watendaji wa Wizara yake hususan Katibu wake Mkuu pamoja na wakurugenzi wake.

Mhe. Naibu Spika, mimi katika kipindi kilichopita nilikuwa kwenye Kamati ya Kusimamia Viongozi Wakuu wa kitaifa ambapo moja katika Wizara iliyokuwa naisimamia ni hii. Naipa sifa kwa sababu nimefanya nao kazi na ninawaelewa vizuri utendaji wao. Kwa kweli ni mzuri sana lakini vile vile nachukua fursa hii kumpongeza sana Makamu wa Kwanza wa Rais kwa uongozi wake na usimamizi wake mzuri katika wizara hii ambao unaipatia sifa katika serikali yetu ya Mapinduzi.

Mhe. Naibu Spika, mimi nadhani sitokuwa na mengi sana ya kusema kwa sababu mengi yameshasemwa na wenzangu, kwa hivyo mimi nitadondoa tu baadhi ya mambo ambayo nimeyaona katika hotuba hii ya Waziri. Mhe. Naibu Spika, mimi nilikuwa nataka kuwapongeza vile vile Wizara kwa

kuw6+eza kutoa takwimu ambazo mara nyingi sana huwa ni kilio changu katika wizara nyingi, kutoa mchanganuo wa takwimu wa kijinsia. Mhe. Naibu Spika, ninawashukuru sana kwa sababu nimeona takwimu zao kwa kweli zimegaiwa kijinsia. Nasema hivi ingawa kuna baadhi ya maeneo hasa katika mafunzo ya ndani nimeona kwamba bado kazi hiyo haijafanyika, lakini nasema hivi kwa sababu sisi tumefunga mikataba ya jumuiya ya Kimataifa. Kwa hivyo iko haja ya kutekeleza ile mikataba ambayo tumeikubali wenyewe, kwa hivyo suala la kuweka *data* za jinsia ni muhimu sana katika kila wizara.

Mhe. Naibu Spika, sasa naingia katika suala la madawa ya kulevya ukurasa 33, Mhe. Waziri kwanza nikupe pole lakini nikupongeze vile vile kwa kazi ngumu ambayo uliyo nayo hii ni jukumu kubwa. Sisi sote ni wahanga wa madawa ya kulevya. Ndugu zetu, watoto wetu, jirani zetu na wengi tumewapoteza kwa sababu ya madawa ya kulevya, wengine wamepata athari katika viungo wengine wamepata matatizo ya akili kwa sababu ya madawa ya kulevya.

Serikali imeshachukua juhudi nyingi sana lakini kwa bahati mbaya katika kuzuia uingiaji wa madawa ya kulevya hapa Zanzibar limekuwa ni tatizo kubwa na mara nyingi huwa tunaitupia lawama serikali. Mimi naamini serikali haiwezi kufanya kazi peke yake iko haja sisi sote kuna tangazo moja mara nyingi linakuwepo *TBC* wanaweka *change* mimi, wewe kubadilika lazima ianze kwa nafsi. Sisi wenyewe tuna jukumu sana katika suala hili la madawa ya kulevya kwa sababu wanaouza madawa ya kulevya tunawajua wengine lakini hatusemi, kwa sababu wengine wapo katika maeneo yetu tunayoishi, hata na wale wanao-*distribute* maana yake wanaouza wale wakubwa lakini *distributers* wanajulikana. Kwa sababu wengine wametengeneza mpaka vidirisha vidogo unapita unaona. Sasa *seriousness* hapa haipo sisi wenyewe tusiinyooshee tu serikali kidole lakini sisi wenyewe hilo ni tatizo kubwa Mhe. Naibu Spika, kwetu tatizo kubwa kwamba tunawajua wako wapi, *distributers* ni akina nani lakini hatua hazichukuliwi. Najua kwamba tatizo ni kwamba wengine wanaogopa kupeleka taarifa lakini hata hizo taarifa zikipelekwa basi vile vile hawachukuliwi hatua. Kwa hivyo kwa ujumla athari hii ya madawa ya kulevya ni mzigo wetu sote na inabidi sote tushirikiane tufanye kazi kwa hili.

Mhe. Naibu Spika, mimi nilikuwa nataka kutoa rai moja ya kuweza kuzuia matumizi ya madawa ya kulevya kwa vijana wetu.. Mhe. Naibu Spika, hawa wanaouza dawa za kulevya kwa sababu nyingi tumeshindwa kuwakamata na kuwachukulia hatua basi sasa hivi tutumie njia mbadala ambayo wenzetu nchi ya Kenya wamewahi kuifanya na wamepata mafanikio kwa kiasi fulani. Mhe. Naibu Spika, Kenya hasa mji wa Mombasa walikuwa na tatizo kubwa sana,

lakini kama tulivyo sisi walikuwa wanawajua ni akina nani wanaouza. Kitu walichokifanya waliwaita wale wauzaji wakazungumza nao kama binadamu, wale ambao wameathirika na madawa ya kulevya wakazungumza nao, wazazi ambao wameathirika watoto wao walikuwepo, wakaitwa na Mashekhe na Mapadri wa dini mbali mbali wakazungumza nao, hawa wanaouza na wao ni binadamu, iko haja sasa ku-*intervene* kwa njia hiyo, hebu tuzungumze nao hawa, jamani mnatuulia watoto wetu hali ndio hii, huyu hana mguu, huyu kafa, huyu kafanya nini, acheni hii biashara, tafuteni biashara nyengine.

Mhe. Naibu Spika, mimi nafikiria njia hiyo kwa upande wa Mombasa walituambia kwamba imefanya kazi na wengine wakajitoa pale pale wakasema nimefanya kweli na ninaomba mnisamehe na niombeeni Mungu, niache shughuli hiyo na wamefanikiwa. Kwa hivyo na sisi labda tujaribu kutumia njia hiyo tunaweza tukafanikiwa.

Mhe. Naibu Spika, kuna suala moja ambalo mara nyingi ambalo huwa tunalisahau kuhusu huu uuzaji wa madawa ya kulevya. Hivi sasa huwezi kumaliza wiki moja bila ya kusikia kijana wa Kizanzibari kakamatwa nje ya nchi kwa kusafirisha madawa ya kulevya, Zanzibar imekuwa na taswira mbaya nchi za nje. Lakini wengine wanaingia kwenye madawa ya kulevya kusafirisha, tunasema kutokana na hali yao ya kiuchumi, kutokana na mambo mengi na ushawishi mwingi, lakini hawa tuwaelimishe vijana wetu Mhe. Waziri, hiyo kazi ya Wizara yako, mbali ya kutoa elimu ambayo itakuwa inazuia matumizi lakini umuhimu mkubwa sasa hivi upo katika kutoa elimu kwa vijana wetu wasijishughulishe na hii biashara ni hatari, wengi wako nje na wako kwenye jela, wazee wao, ndugu zao ambao walikuwa wanawategemea huku wake zao wengine wanaathirika, elimu kubwa itolewe kwamba huko mnakokwenda nje ukenda ukifanya biashara hii basi athari yake ni kifungo cha maisha, kifo au jengine lolote linaweza kumtokezea mtu. Sasa elimu hiyo naomba sana Wizara yako Mhe. Waziri itolewe sasa hivi kuwapa vijana wetu ambao wanadhania labda biashara ile ni kitu ambacho unaweze kukifanya kirahisi na ukafanikiwa, hali ni ngumu hakuna nchi yoyote ambayo inataka madawa ya kulevya yaingie katika nchi yake na mbinu ya kuwapata zipo, kama kwetu sisi kuingia ni rahisi lakini nchi za nje ni vigumu.

Mhe. Naibu Spika, kuna vijana wetu wengi wako China, Uturuki hizo zote ni nguvu kazi hiyo, wako Ugiriki, wameacha wazee wao huku, wameacha ndugu, wameacha watoto wanaowategemea. Naomba Mhe. Waziri, elimu kubwa itolewe katika upande huu.

Mhe. Naibu Spika, kulikuwa kuna mpango wa ujenzi wa kituo cha kurekebisha tabia Tunguu. Mimi nakumbuka tulipokuwa kwenye Kamati ya

Kusimamia Viongozi Wakuu tulikuwa tunaliulizia suala hili sana na tukaambiwa kwamba ule mpango upo unaendelea. Sasa mimi nilikuwa nataka kujua tu ni kitu gani ambacho kimekwaza ujenzi huu wa nyumba hii ya kurekebishia tabia ya vijana kwamba mpaka sasa hivi haujafanyika na kama upo mpango unaendelea na kama fedha zipo zimepatikana. Nimejaribu kupekua sana kwenye hili sijaona inawezekana lipo lakini sijaziona, kwa sababu niliambiwa kwamba unaweza ukaanza wakati wowote kwa sababu tayari wameshapata *go ahead.* Sasa nilikuwa nataka kujua kama kweli ujenzi huu utaendelea na lini vile vile unaweza ukamalizika.

Mhe.Naibu Spika, kwa upande wa madawa ya kulevya tulipokuwa kwenye Kamati tulikwenda Uwanja wa Ndege ambapo kumejengwa choo kwa ajili ya wale wanaoleta madawa ya kulevya kwa njia ya kumeza, ili pale ambapo wanawa-*suspect* wanawatilia mashaka ya kuwa na dawa za kulevya basi waweze kwenda chooni wakatoa yale madawa. Lakini miundo mbinu yake ya pale haikukamilika Mhe. Naibu Spika, na tulilizungumza hilo, kwa sababu kuna choo tu lakini mambo ambayo yanatakiwa kufanywa kabla ambapo mtu anapotoka kwenye ndege huwezi kumchukua ukamwambia twende chooni, lakini kuna *inspection* au kuna mambo ambayo anafanyiwa kwanza yule mtu, eneo halipo ambapo mtu anatakiwa kwanza aweko Afisa ambaye anashughulikia na mambo hayo amfanyie *interview* yule ili awe angalau na sababu ya kumpeleka kule chooni, lakini baada huyu mtu anatakiwa vile vile kupelekwa kupigwa X-*ray* ambayo ni mbali, pengine labda hospitali ya Mnazi Mmoja. Sasa sijui Wizara yake Mhe. Waziri imejipanga vipi katika hili. Tulilizungumza hili na wakasema kweli udhaifu huo wameuona lakini watalifanyia kazi. Sasa mimi nilikuwa naomba nijue imefikia hatua gani.

Mhe. Naibu Spika, vile vile jengine nilikuwa nataka kujua kwa sababu unapotengeneza kitu unakuwa una matumaini ya jambo Fulani. Sasa nataka kujua iwapo tayari kile choo kimeshaanza kutumika na watu wangapi wamekamatwa kwa kutumia njia ile ambayo imewekwa pale Uwanja wa Ndege.

Mhe. Naibu Spika, mimi nitazungumza kwenye suala la walemavu ukurasa wa 27, nayo ningependa vile vile kutoa ushauri. Tatizo kubwa Mhe. Naibu Spika, katika Idara ya Walemavu na wengi hapa wamezungumzia ni miundo mbinu na tumeona kweli katika majengo yetu mengi sana hakuna miundo mbinu ya walemavu, ni tatizo. Tunazungumzia suala la kuwaajiri walemavu lakini miundo mbinu haipo, tunazungumzia suala la kuwapa haki sawa walemavu lakini miundo mbinu haipo. Sasa mimi nataka kushauri kwamba ufanywe utafiti wa kina katika Wizara zetu zote za Serikali pamoja na Taasisi zake ambao utaweza kusaidia utafiti huo wa kuanza kuweka miundo mbinu hiyo katika Ofisi zote za Serikali pamoja Taasisi zake, na naomba sana utafiti

huu ufanywe na Wizara yake kwa sababu naamini ni Wizara yake tu ambayo atakuwa na uwezo kufanya utafiti huu na kuweza kupeleka Serikalini, wengine sio rahisi kuufanya. Kwa hiyo Mhe. Waziri, naomba hilo lifanyike.

Mhe. Naibu Spika, vile vile hili suala zima la walemavu Mhe. Waziri, amesema kwamba hapa walemavu wamesaidiwa katika vikundi mbali mbali ili waweze kujiajiri wenyewe. Sasa mimi ni mpenzi wa kuangalia *television* na mara nyingi naangalia za Tanzania Bara huona vipindi mbali mbali vya walemavu ambao wamejiajiri wenyewe na huwa inanipa faraja kubwa. Lakini kwa bahati mbaya inawezekana kwa upande wa Zanzibar pia vipindi vinatolewa lakini sijawahi kuona, sasa naomba vile vile ili na sisi tupate faraja tuwaone na wao basi wanafaidika kikweli kweli na hizi fedha ambazo wanapewa na Serikali, kwa maana ya kuwa tuone kuna mambo ambayo yanapendeza yakionekana. Kwa hivyo Mhe. Waziri baada ya kuwa unatoa fedha kwa vikundi hivi lakini sasa tuone nini wanazalisha na wanazalisha vipi, ili na sisi tupate moyo wengine wa kuweza kuwasaidia kwa sababu yule ambaye anajitahidi basi ni rahisi zaidi kumsaidia.

Mhe. Naibu Spika, la mwisho nazungumzia suala la mazingira, wengi wamesema mimi naunga mkono sana, kauli aliyoitoa Mhe. Marina Joel Thomas tuanzishe *pilot program* ambayo itatusaidia kuona kuwa ni kigezo kwa ajili ya Unguja na Pemba yote, hebu tusijaribu kufanya kwa kila pahala lakini tuanze na *program* ambayo tunaona hii ni *pilot*, tunafanya hapa pamefanikiwa tunakwenda sehemu nyengine. Kwa hivyo mimi nafikiria hilo ni muhimu sana na namshukuru sana Mhe. Marina Thomas kwa kutoa wazo hilo, lakini vile vile namshukuru sana Mwanasheria Mkuu kutueleza kwamba sasa hivi tuna hakika kwamba kisiwa cha Fungu Mbarak ni kisiwa chetu.

Mhe. Naibu Spika, mara nyingi sana huwa anazungumzia suala la ndege asilia Zanzibar wanapotea hatuwaoni tena, kisiwa hiki kimejaa ndege na kisiwa hiki tunaweza kukitumia kwa mambo mbali mbali ikiwemo utalii ambao ni uchumi wetu mkubwa. Mhe. Waziri nakuomba sana kwa sababu niliambiwa kwamba kuna utafiti ambao unafanywa kuhusiana na kuwaenzi na kuwaweka vizuri ndege asilia. Sasa mimi naomba kwa kutumia kisiwa hiki utafiti ambao sina hakika kwa sababu Mhe. Waziri labda utakuja hapa utaniambia utafiti huo kama umeanza au haujaanza, lakini najua kwamba upo. Kwa hivyo ningeomba sana kwamba kisiwa hiki sasa hivi ni wakati wa kukitumia kwa sababu tutapata *diversity* ya utalii, hapa tutapata tutajua kwamba na hiki ni kitu ambacho kinaweza kutuongezea katika uchumi wetu au katika masuala yote ya utalii.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kusema hayo machache nashukuru sana na kwa niaba ya wanawake wenzangu wote Unguja na Pemba naunga mkono hoja asilimia mia moja. Ahsante sana.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Ahsante Mhe. Naibu Spika, na mimi kunipatia nafasi hii angalau kutia baraka zangu katika hotuba hii ya bajeti ya Mhe. Waziri katika Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais. Mhe. Naibu Spika, sijui kama nitamaliza kwa dakika kumi lakini nitajitahidi kufanya ufupisho ili niweze ku-*cover* jambo kwa muhtasari haya niliyoyakusudia kuyasema.

Mhe. Naibu Spika, kwanza ninataka nianze na Ofisi Kuu Pemba. Katika hili nimefunua kitabu hiki cha Makadirio ya Mapato na Matumizi, kitabu cha kwanza ukurasa wa 77. Ukiangalia kwenye *bullet 211201* kuna kodi ya nyumba. Nilikuwa ninaomba kwanza Mhe. Waziri atuambie ni nyumba gani hii ambayo tunakodi, maana yake nafikiria fikiria tu kwamba labda ni ile nyumba ambayo ofisi yao ipo. Lakini hoja yangu ni kwamba kodi ya nyumba kwa mwaka imepangiwa 7,800,000/=. Halafu ukiangalia *bullet 211208* kuna huduma za ulinzi nayo imepangiwa 5,400,000/=. Sasa ukija Unguja kwenye Idara ya Faragha 211201 kuna kodi ya nyumba tena nayo imepangiwa 98,150,000/= kwa mwaka na ukiigawa kwa mwezi hiyo ni kila mwezi ni 8,179,166.6.

Mhe. Naibu Spika, hoja yangu ni kwamba hii Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais ni Ofisi ya kudumu kwa mujibu wa Katiba, tukiendelea kukodi nyumba ya kukaa Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais, kwa kiwango hichi, tukaendelea kukodi nyumba za ofisi, tukaendelea kukodi walinzi, mimi nadhani tutafika pahali siku moja utakuta tumeitia hasara Serikali pesa nyingi sana. Sasa naomba Waziri aje anifafanulie au anieleze Wizara hii ina mpango gani wa kutafuta majengo yake ya kudumu ya ofisi ya kule Pemba na nyumba ya kumuweka Makamu wa Kwanza wa Rais.

Vile vile Mhe. Naibu Spika, pia nimetia mashaka sana na kodi ya ulinzi. Mhe. Naibu Spika, 5,400,000/= kila mwaka kwa ulinzi na hii naona ni *special* kwa Ofisi hii ya Makamu wa Kwanza wa Rais. Nakumbuka katika nchi hii tuna vikosi 5 vya ulinzi na vinatoa huduma sidhani kama wanalipia, tuna Polisi wanatoa huduma za ulinzi, kwa nini hawatumiki hawa na Pemba wako wengi sana askari Polisi kule, vikosi vyetu hivi vya Idara Maalum viko vingi, kwa nini tukodi watu walinde kwa pesa, hebu Mhe. Waziri akija atupe ufafanuzi mzuri.

Mhe. Naibu Spika, sasa nataka niingie katika Idara ya Mazingira. Idara ya Mazingira kwanza ina umuhimu wa pekee katika nchi yetu, halafu ni idara ambayo kwa kweli inakabiliwa na changa moto kubwa sana, mambo mawili

ni mazito sana ambayo yanaratibiwa na idara hii. Kwanza ni mabadiliko ya tabia nchi, jambo ambalo kama tutalizingatia vizuri ni tishio sana la visiwa vyetu hivi. Mhe. Naibu Spika, visiwa vyetu vinazamishwa ndani ya maji kwa *speed* kubwa sana, kila mwaka ukipita basi kuna *centimeter* fulani ya ardhi yetu inazama kwenye maji na nilikuwa naomba sana hapa Mhe. Waziri atupe ufafanuzi au taarifa zile za kiutafiti kwamba nchi yetu katika miaka 10 hii iliyopita kwa mujibu wa utafiti ambao umefanywa, labda ni *kilometer* ngapi za mraba zishazama ndani ya maji. Nasema hivi kwa sababu lazima tuwe tunaangalia kwa sababu visiwa vyetu ni vidogo, ongezeko la idadi ya watu *speed* yake si ndogo nayo, itafika pahala katika nchi hii tutakuwa hatuna pa kukaa. Kwa hivyo naomba sana Mhe. Waziri atoe hii na isibakie hapa lakini iwe ni taaluma kwa waanchi.

Mhe. Naibu Spika, tatizo la pili kubwa ambalo Idara linakabiliana nalo ni matumizi mabaya ya rasmali zisizohamishika. Kuna uchimbaji wa mchanja wa ovyo ovyo na mawe, siku zote Mhe. Hija ananung'unikia suala hilo lakini pia kuna ukataji wa miti ovyo, na katika haya unajua kuna mambo ni ya lazima katika jamii yatokee lakini nadhani kitu cha msingi ni kuwa na sera na mikakati madhubuti ya kufanya *replacement* ya ile sehemu iliyoondolewa, wenzetu wanakata miti pia lakini wana mikakati ya kurejesha miti.

Sasa hapa mimi nadhani nataka nitoe lawama kidogo kwa Idara hii ya Mazingira na peke yao, lakini na Idara ya Misitu pia. Mhe. Naibu Spika, hawako makini hawa kwa sababu wanaoharibu mazingira kwa kuhamisha raslimali hizi ukiachilia hayo makampuni yanayokuja kujenga mabarabara na mambo mengine, lakini kuna mtu mmoja mmoja wanafanya hizi shughuli za kukata miti ovyo kwa kupiga makaa au chokaa na Idara ya Mazingira na Idara ya Misitu wanawajua, lakini wanashindwa kuwachukulia hatua na hali nataka Waziri anieleze vizuri kwa sababu mimi binafsi kuna mambo niliyachukulia hatua nikawaambia watu wa Mazingira na nikawaambia watu wa Misitu, na kila nipowaambia waliniambia hilo jambo tunalijua, wanaofanya tunawajua lakini wale wanafanya Mhe. Naibu Spika, wanaendelea. Sasa kwa sababu wanawajua na wanaendele maana yake nini hawako makini au wanashirikiana nao. Sasa naomba jawabu nzuri kabla sijazuia vifungu hapa.

Mhe. Naibu Spika, jambo jengine nimeona hapa katika maelezo ya Mhe. Waziri kwamba mwaka jana wahisani walitoa ahadi ya kuchangia 705,000,000/= lakini zilizopatikana ni 616,000,000/= namna zilivyotumika zimeelezwa kwenye kiambatisho nambari mbili, mambo ya kudhibiti mazingira hayo, sasa ukiangalia hichi kiambatisho nambari 2 kimeeleza tu Makamu wa Kwanza wa Rais kuna 363,000,000/=, Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) kuna 44.3, Jumuiya ya *CODECOZ* ina 20, Ofisi ya Rais, Fedha na Uchumi milioni sitini na sita lakini hakuna maelezo kwamba hizi

fedha walizifanyia nini kwa sababu mimi katika hili la mazingira kwa kweli nataka nipate mchanganuo mzuri hizi fedha walizitumiaje katika kudhibiti mazingira. Kwa hivyo naomba Mhe. Waziri akija atupe ufafanuzi kwamba hizi pesa, maana yake inaonekana hili suala ni suala Mtambuka kila Taasisi, si Taasisi yake tu ni Taasisi nyingi zina-*role* katika uhifadhi wa mazingira, lakini wamepewa mafungu haya naomba aje atufafanulie mafungu yao waliyatumiaje kwa mwaka huu kabla hatujaidhinisha milioni mia nane za mwaka huu.

Mhe. Mwenyekiti, nikiondoka hapo labda niingie kidogo kwenye Tume hii ya Kuratibu na Kudhibiti Madawa ya Kulevya. Hapo napo ni eneo la pili ambalo na mara nyingi huwa nasema na katika hili pia nailaumu serikali sana. Mhe. Naibu Spika, serikali ni dudu kubwa linalotisha na lenye uwezo wa kuchukua hatua na pale ambapo serikali inapotaka kuchukua hatua tunaona namna wanavyodhibiti. Mimi siamini hata siku kama serikali haiwajui wanaleta unga humu ndani ya nchi yetu, siamini hata siku moja, Serikali inawajua lakini kinachotokea ni kwamba sijui kuna usiri gani mpaka ikawa serikali inashindwa kuwadhibiti.

Sasa kwa sababu serikali inawajua na suala hili la unga ni suala baya sana ambalo linatumalizia nguvu kazi ya watu wetu, mimi nataka niseme kwamba serikali inashirikiana nao. Sasa kama haishirikiani nao Mhe. Waziri aje atwambie hapa kama hawajui, na mimi kuna maeneo mara nyingi napenda kuyasema kwanza maeneo ya mahoteli na kule ni *free port* kabisa, tusikae tu *Airport* tukafikiri unga utapita *Airport* au bandarini pale, haya mahoteli haya ndimo inamopita na kule hakuna uratibu wa aina yoyote unaofanywa na serikali. Mimi nadhani serikali kama inataka kuwagundua hawa wafanye uratibu kwenye mahoteli.

Mhe. Naibu Spika, mara moja niliwahi kusema hapa kwamba tena nilikuwa naiambia ofisi hii, kule Jimboni kwangu Tundauwa kuna mtu kauza sehemu ya ufukwe haijaiendeleza, kajenga kibanda kidogo cha kuja kupumzikia tu hivi lakini wananchi wa kule wanaendelea kuona yule aliyenunua eneo akija basi kuna boti inatoka baharini inakuja pale, wakifika wanazungumza maneno mawili matatu wanayoyajua wenyewe, halafu yule aliyenunua eneo anatoka na gari yake anarudi na boti inakwenda. Mimi nikawaambia nina wasi wasi na kwa huyo anayekwenda *possible* kuwa anafanya biashara hii. Sasa sijui kama wamefuatilia au vipi.

Mhe. Naibu Spika, mimi nadhani serikali bwana lazima ichukue uwezo wa kuchukua hatua serikali kuhusu hawa watu wanaovuta unga, watu hawa wenywe ukimwi wanajichanganya hapa hapa, mimi siku zote huwa nasema ushauri nasaha hausaidii. Mhe. Naibu Spika, mtu akipata *cancer* katika

kiungo chake kile kiungo kile na daktari hushauri kwamba kikatwe, sasa na sisi jamii yetu inatatizo ina *cancer* leo tunakwenda tunawakuta wanatoka madenda tunawatizama tu halafu tunawapa ushauri nasaha, kama ushauri nasaha unasaidia *qur-an* ingetosha Mwenyezi Mungu asingeumba moto, kwa sababu *qur-an* imeeleza kila kitu lakini Mwenyezi Mungu baada ya qur-an kaumba na moto kwa sababu binadamu ni wakorofi. Sasa mimi nadhani kuna *concept* hii mtu anapokuwa mkorofi katika jamii unamtenga na ile jamii, kwa nini watu hawa hatuwapeleki jela, wala tusiwaadhibu kule wakakae tu lakini wasiwemo ndani ya jamii watasababisha na watu wengine.

Mhe. Naibu Spika, muda haupo kuna *point* yangu moja sijaimaliza lakini mie nitaunga mkono hoja baada ya ufafanuzi.

Mhe. Ibrahim Hussein Makungu: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwanza na mimi nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa afya njema asubuhi hii ya leo. Pia nikushukuru wewe Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii nimpongeze Mhe. Waziri na Watendaji wake wote kwa hotuba hii ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, kuhusu makadirio ya fedha ya mwaka 2013/14. Mimi nichangie sehemu chache katika hotuba hii

Mhe. Naibu Spika, kwanza nianzie katika ukurasa wa 27 kifungu 70. Idara hii ina majukumu ya kuratibu masuala mbali mbali ya watu wenye ulemavu huo ni wajibu wa sheria ya Zanzibar. Pamoja na jitihada ya Serikali na Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, bado haijakuwa na nia ya dhati ya kusaidia watu wenye ulemavu, imekuwa na maneno mengi ya kusema na mambo yaliyokuwa si ya ukweli hasa kwa kuwakusudia watu wenye ulemavu.

Mhe. Naibu Spika, udhalilishaji wa watu wenye ulemavu bado unaendelea kwa kasi katika jamii yetu. Mhe. Naibu Spika, kwanza iwekwe sheria ya majengo yanayojengwa yawe na sehemu maalum kupitia watu wenye ulemavu, kuonesha kwamba inawajali na kuwawekea sehemu zao kwa ajili ya kufuatilia shughuli zao kwa karibu kabisa. Majengo kama ya serikali na ya watu binafsi. Mhe. Naibu Spika, tusisahau kwamba na sisi pia ni sehemu ya walemavu, unaweza ukatoka mzima lakini ukarudi ukawa huna mguu kwa kupata ajali au kwa maradhi ya aina mbali mbali kama tunavyojua.

Mhe. Naibu Spika, nimesema hivi kwa sababu sitaki niseme walemavu, tukiangalia suala kubwa la hawa wananchi wetu badhi ya walemavu, skuli zao wanazosoma kwa kweli haziko kwenye mazingira mazuri na kupata elimu ni muhimu katika maisha yetu.

Mhe. Naibu Spika, niseme kusomesha watoto wenye ulemavu vifaa maalum vya kusomeshea havipo, hasa watu wenye ulemavu wa macho vifaa vyao

hamna. Kwa kweli hawa watu wenye ulemavu wanapata shida sana Mhe. Naibu Spika, katika nchi yetu. Mfano kuna skuli moja niliwahi kutembelea hapa hapa Zanzibar Mwanakwerekwe 'C'. Mhe. Naibu Spika, inasikitisha wanafunzi hao wanavyosoma hamna viti, hawa maisha yao yako duni, jengo wanalosomea watoto hawa walimu wenyewe wanajitolea kwa kutafuta ada ya kulipia eneo hilo. Kwa kweli fedha zao inakuwa shida kupata kulipia jengo hilo.

Mhe. Naibu Spika, watoto wenye ulemavu wanapata shida sana lakini hao walimu wanatoa mchango mkubwa sana kwa watoto hao na kuwasaidia kuwasomesha pamoja na kuwapatia mawazo mbali mbali na kuwaweka katika sehemu nzuri. Naomba serikali wawaangalie sana hawa walimu kwa juhudi zao kubwa, lakini pia ningemuomba Mhe. Waziri siku moja afanye ziara awatembelee skuli hiyo iliyopo Mwanakwerekwe 'C' akaone mwenyewe hali halisi ya watoto hao wanavyosoma.

Mhe. Naibu Spika, skuli hiyo watoto wanaosoma hapo ulemavu wao kusema hawawezi na kusikia hawasikii. Hebu tufikirie walimu wao wanapata shida vipi kuwasomesha watoto hao. Naomba Mhe. Waziri siku yoyote akitaka twende pamoja nitafuatana naye kwenda kuwasaidia skuli hii ya watoto walemavu. Mimi na yeye kwa pamoja tutakwenda kuangalia hali halisi ya watoto hao.

Watoto wenye ulemavu wanapata tabu pia kusafiri, unakuta wakati mwengine watoto hawa hawana hata fedha ya usafiri kwa vile maisha yao ni duni. Kwa hivyo, naomba sana serikali iweze kuwapatia hawa watoto vitambulisho ili waweze kupata usafiri bure wasitozwe gharama. Mhe. Naibu Spika, naiomba sana serikali kama ikiwezekana kama nchi za wenzetu wanavyofanya watu wenye ulemavu wanawasaidia mpaka fedha kwa kila mwezi. Kwa hivyo, naomba Mhe. Waziri suala hili aliangalie sana kwa watu wenye ulemavu ikiwezekana kwenye bajeti yetu ya serikali basi tuwatengee fedha maalum kila mwezi tuweze kuwasaidia hawa watu wenye ulemavu iwe kama ni changamoto kuwatatulia matatizo yao ya kimaisha.

Mhe. Naibu Spika, niingike katika ukurasa wa 28 kifungu 74 hapa anasema katika kitabu hiki cha bajeti Jumuiya kumi za Watu wenye Ulemavu wamepatiwa ruzuku ya shilingi milioni moja laki saba kwa kila kikundi. Sasa Mhe. Naibu Spika, nakuuliza hizi fedha wanapewa kwa muda gani, kwa mwaka, kwa mwezi au kila baada ya muda fulani au mara moja tu wamesaidiwa hizi fedha? Kwa hivyo, naomba ufafanuzi wa kina kabisa kuhusu hivi vikundi na kama wanapewa hizi fedha basi tuwe na bajeti maalum ya kupewa kila baada ya mwezi au miezi sita wasaidiwe hizi fedha kuwasaidia watu hao wenye ulemavu.

Mhe. Naibu Spika, nikija kwenye ukurasa 28 kifungu 75, idara hii ipokee misaada ya visaidizi vya watu wenye ulemavu kutoka kwa Umoja wa Wazanzibari wanaoishi nchini Canada (*ZANCANA*) pamoja na watu wengine. Mhe. Naibu Spika, mimi nigusie kidogo suala hili kweli vifaa vimekuja kwa kutusaidia na ninawashukuru sana wananchi wanaoishi nchini Canada kuona kama wananchi wenzao wanapata shida kwa vifaa hivi. Wameliona suala hili na kutuletea vifaa hivyo, wanatujali na wanajua huku ndio nyumbani kwao na iko siku watarudi nyumbani kwao. Nawashukuru sana.

Mhe. Naibu Spika, mimi nataka nimwambie Mhe. Waziri misaada hiyo ililetwa kutoka Canada sijui waliofaidika ni sehemu gani na gani. Kwa hivyo naomba anisaidie kidogo ili kujua waliofaidika ni watu gani hao. Niseme hivi kwa sababu mimi mwenyewe binafsi katika Jimbo langu la Bububu nimetoa *wheelchair 20* kwa watu wenye ulemavu, lakini la kusikitisha kabisa *wheelchair 20* hizo hazikutosha Mheshimiwa na mpaka hivi leo bado kuna watu wana shida na vigari vile jinsi ya watumiaji hao walivyokuweko wengi. Kwa hivyo, nilikuwa namuomba Mhe. Waziri hawa waliofaidika na misaada hii anitajie ni nani hawa.

Mhe. Naibu Spika, kidogo nigusie suala la Hospitali yetu ya Kidongo Chekundu. Mhe. Naibu Spika, suala hili ni hali mbaya na inasikitisha sana kwa watu wenye ugonjwa wa akili hasa hospitali iliyoko Kidongo Chekundu, hali yao mbaya sana kwa wagonjwa wetu inasikitisha. Mimi nilifanya ziara ya kwenda kuangalia pale nimepata matatizo ya wagonjwa hawa ambao wanahitaji madawa ili waweze kuweza ku-*survive* na akili zao ziweze kurudi kwenye *level*. Lakini niseme tu kwamba dawa hizi wanataka wapatiwe kila mwezi, lakini unakuta ukienda hapo hospitali dawa hizi hamna na hao wagonjwa inabidi wanunue na dawa hzi za sindano moja shilingi 10,000/=, inaitwa *modecate injection*. Shindano hii lazima apate kila mwezi mgonjwa huyu ili apate ku-*survive* akili yake iwe na hali nzuri, lakini hospitalini hapo dawa hizo hamna. Dawa hizi mpaka ununue *pharmacy* za nje ambapo wanauza shilingi 10,000 kwa chupa moja.

Lakini Mhe. Naibu Spika, kuna dawa nashukuru sana, namshukuru sana Mhe. Waziri kuwa dawa hizo za *tablets* unapata bure na nashukuru sana kuwa *tablets* zenyewe ni hizi *largactil, carbamazepine, haloperidol* na *artten*. Hizi unapata bure nashukuru sana Mhe. Waziri kwa kuliona hili na dawa hizi zipo.

Namalizia kidogo na uingizaji wa madawa ya kulevya. Kwa sababu muda sina lakini nigusie kidogo tu. Mhe. Naibu Spika, utumiaji wa dawa za kulevya bado upo na unaendelea kwa kasi sana nchini. Lakini inaonekana hatujawa *serious* na suala hili. Mimi niulize haya madawa anayeleta nani. Inasikitisha

sana katika njia zote kuu za usafiri kuanzia Uwanja wa ndege Unguja na wa Pemba.

Mhe. Naibu Spika, mimi mwenyewe Mjumbe wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi na mara nyingi natembelea maeneo haya. Lakini utakuta hizi *X-Ray machine* zimepitwa na wakati haziwezi kuona madawa ya kulevya, vinaangalia baadhi ya vifaa tu lakini sio kuangalia madawa. Sababu kubwa inawezekana hizo *X-Ray* sio za kisasa naweza kusema zimepiwa na wakati kwa hivyo haya madawa yanaingia kama mchezo hapa, kama hatujawa *serious* kwa suala hili hatuwezi kuwadhibiti.

Kuhusu hawa wauzaji kama Waheshimiwa wenzangu walivyochangia kwamba wauzaji wanajulikana lakini hakuna hata mmoja aliyechukuliwa hatua. Mimi naomba hizi sheria zibadilike kabisa hawa waletaji wa biashara hii ya madawa ya kulevya kwa nini sheria hii isiwekwe wazi mtu anayeonekana na madawa ya kulevya akafungwa maisha au akanyongwa kabisa. Kwa sababu nchi za wenzetu sasa hivi kama vile China, Bangkok na nchi nyengine wanatoa kabisa adhabu ya kunyonga au wanakufunga maisha. Lakini sisi hatujaweka wazi suala hili na tukiweka wazi suala hili nafikiri Mhe. Naibu Spika, litapungua kwa kazi kwa sababu mtu ataogopa kufanya biashara hii kwa ajili ya maisha yake. Lakini niseme tu Mhe. Naibu Spika, Wizara ya Makamu wa Kwanza wa Rais inapoteza fedha nyingi sana kuwatibu wale walioathirika kwa madawa. Kwa mfano *Sober House*, wameshaathirika lakini utakuta wanapoingia katika *Sober House NGO* wanatakiwa walipe shilingi 150,000/= mtu kutoka Tanzania Bara, lakini kutoka Zanzibar anatakiwa alipe shilingi 130,000/=.

Sasa hizi fedha tunafanya kama mradi kuwapatia hawa wenye *Sober House*, lakini serikali ingechukua jukumu hasa la kuwakamata hawa na kuwadhibiti basi hata hizo *Sober House* zingepungua kwa wingi. Kwa sababu hii imekuwa kama biashara sasa hivi kwa wanaoathirika wende pale wakatibiwe na kila mwezi wanatakiwa hawa walioathirika walipe shilingi 60,000/-. Mheshimiwa tunafanya nini hapa? Wananchi wetu tunawapa matatizo makubwa na maisha yanazidi kuwa magumu kwao wao, kwa sababu wanapoathirika wanakwenda *Sober House*, wanapopona wanarejea tena kwenye kuvuta hayo madawa ya kulevya.

Mhe. Naibu Spika, mimi na Jimbo langu la Bububu. tunaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwanza kabisa nimshukuru Mwenyezi Mungu aliyenijaalia kuwa katika hali ya uzima

na afya kuniwezesha kusimama mbele ya Baraza lako tukufu ili kutoa maoni yangu katika kuchangia.

Mhe. Naibu Spika, vile vile na mimi nichukue fursa hii kumpongeza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa hotuba yake nzuri aliyoitoa mbele yetu pamoja na watendaji wake wote.

Mhe. Naibu Spika, kwa sababu muda haukidhi haja itabidi niende moja kwa moja katika mchango wangu. Nikienda katika ukurasa wa sita hapa kuna mambo ya vipaumbele katika ofisi hii lakini moja kwa moja leo tunakuta hapa inasema kufanya utafiti na kukusanya taarifa juu ya shughuli zinazoelekezwa na Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais.

Mhe. Naibu Spika, kufanya utafiti ni jambo zuri sana kwa sababu ukifanya utafiti utajua unachokwenda kukifanya ni kitu gani, lakini bila ya utafiti basi huelewi unachokifanya ni nini. Lakini mimi niseme tu katika hapa kwenye utafiti, hao wanopelekwa kufanya utafiti lazima wapewe elimu ya kujenga uwezo juu ya kupenda nchi yao. Kwa sabahu unaweza kwenda kufanya utafiti lakini ukagundua mambo ukarushwa kule kwa kugundua. Sasa unaweza baada ya kufanya utafiti ukapewa rushwa ukayaachia yaliofanyika. Kwa hivyo, tunasema kwamba hawa waweze kuipenda nchi yao na kufanya vizuri katika yale mambo wanayofanyia utafiti ili kuweza kufikia malengo yetu.

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli katika hali ya nchi yetu inavyokwenda ukizingatia hali ya mazingira tumefikia katika hali mbaya sana. Vile vile kwanza nimpongeze Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa kuweza kufikia ufanisi mzuri katika kukabiliana na mifuko ya plastiki, hapa tunampongeza sana. Lakini jengine kumezuka jambo moja ambalo linashinda hiyo mifuko ya plastiki katika uchafuzi wa mazingira. Tukiangalia mitaani kwetu kuna chupa hizi za *drop*, chupa hizi watu wanazitumia vibaya kwa sababu wanatumia kwa mambo ya kukojolea mle halafu wanazitupa na chupa zile zile zinaokotwa zinakwenda kufanyiwa mambo mengine, basi hili linaharibu mazingira zaidi.

Kama haitoshi Mhe. Naibu Spika, katika mambo ya mazingira basi nchi ya Zanzibar ina mazingira machafu. Namuomba Mhe. Waziri afanye kutembelea asikae tu ndani ya gari, aangalie pale *block No. 7* Nyumba za Maendeleo za Michenzani jinsi palivyochafuka kama bahari, usiangalie upande wa barabara angalia upande wa pili. Pale *chamber* zinatoa uchafu sehemu yote ni chafu, nadhani akitoka hapa tufuatane akaangalie aseme kama niliyosema ni uongo na hii kuna wasimamizi, sasa kama usimamizi wetu haukuwa mzuri hatuwezi kufikia malengo hata siku moja. Sote ni mashahidi hapa, katika mambo ya

kudhibiti mazingira hapo kulitumika mikakati mikali katika kuwadhibiti wavuvi katika habari ya mazingira.

Mwaka jana watu walichomewa nyavu zao kwa nini hawa tusiweze kufikia katika ufanisi? Hebu tujiulizeni katika kuwachomea nyavu zao tumepata maendeleo gani ila kuwaangamiza tu, lakini kuna mambo ambayo yamekabiliwa hapa tukafikiri nchi yetu ikawa nzuri. Mhe, Naibu Spika, naomba waziri atembelee katika soko la samaki lilioko Malindi, kuna uchafu umekithiri kule na kule samaki analiwa ni chakula ambacho kinajenga mwili, lakini ukiangalia katika sehemu wanayowekwa ni mbaya. Watu wanajisaidia ovyo katika sehemu ile ya matishali kule, afanye kutembelea na akitaka mimi nitamuongoza katika sehemu hizo.

Mhe. Naibu Spika, katika uharibifu wa mazingira hata katiba yenyewe tunasema serikali nayo inaharibu mazingira, na mimi nasema mtu yeyote kila jambo analoanzisha basi anaharibu mazingira lakini anaharibu mazingira kwa kiasi gani. Tunaingia mikataba na watu katika mambo ya miundombinu kwa kujenga barabara lakini mtu anaambiwa akitaka kuchimba kifusi achimbe mita tatu anakwenda mpaka mita sita anakuta maji ya bahari. Suala hili liko Micheweni kule limejitokeza kabisa na ukiona kule utaona madimbwi kama bahari ni tatizo, tusiangalie wananchi hata sisi serikali tunapoingia mikataba na hawa wakandarasi wetu tujue. Micheweni na Vitongoji kule halikadhalika mambo ni mabaya.

Halafu katika kitabu hiki ukurasa huu huu wa sita kuna kifungu hapa kinasema kutoa huduma maalum kwa watu wenye ulemavu. Hili ni jambo jema, hawa kuwapatia huduma maalum watu wenye ulemavu ni jambo zuri sana, lakini tuzingatie hawa walemavu wako sehemu mbali mbali tuwajue, wako mjini na mashamba. Tumeshuhudia walemavu wakiwa omba omba kwa kukosa hizo huduma. Kwa hivyo, kama tutawapa huduma maalum na tuwajue kwanza ni wangapi na wako wapi basi wakipata huduma hizi angalau tunaweza kukidhi haja. Lakini tunashuhudia walemavu wanakuwa omba omba kabisa hawana sehemu ya kujisaidia kupata rizki zao ni tatizo.

Mhe. Naibu Spika, vile vile katika kudhibiti mazingira anatuomba pesa hapa ili kwenda kufanya hayo, lakini kuna kamati ambazo zinasimamia mazingira, haya sisi tunasema mabadiliko ya tabianchi, koko hizi zikikatwa maji huvimba sana lakini mbona hizi kamati hatuzisaidii. Kwa mfano, kamati iliyoko kule kisiwani Kojani kina koko nyingi sana, upande wa Kaskazini kuna koko nyingi sana lakini wale kamati wanashindwa kufanya kazi zao katika kulinda mazingira kwa sababu hawana vitendea kazi. Mtu unamwambia alinde mazingira hana vitendea kazi. Mheshimiwa wale watu

wa Kojani wanataka kusaidiwa mashine japo ndogo ya *horsepower* 25 inawafaa.

Mhe. Naibu Spika, Wakojani kwenye kamati ya kudhibiti mazingira ya kuhifadhi mikoko ina-*suffer* kutoka pale kisiwani Kojani wanapoishi na kwenda katika sehemu ya mikoko iliko. Kwa hivyo, wanaomba msaada angalau wapatiwe mashine ya nje kupata msaada wa kulinda yale mazingira, kuna koko nyingi sana tu kule. Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, tukiwapelekea watadhibiti yale mazingira namna ya kulinda, lakini kama basi hawawezi kufikia malengo siku na siku mikoko inakatwa bahari inachimbika kabisa na ardhi inamegwa.

Mhe. Naibu Spika, katika kuendelea na mchango wangu haya mabadiliko ya tabianchi jambo hili kusema kweli Mwenyezi Mungu ndiye mwenye kujua mambo haya. Kwa sababu kuna mambo mengine ni amri yake Mwenyezi Mungu. Kwa mfano kimbunga kikija hapa huwezi kukizuwia, ije *tsunami* huwezi kuizuwia, lakini sisi tunavyotakiwa tujipange vizuri tu katika kukabiliana na mambo hayo, yakitokea yale maafa angalau tuwe tumeshajipanga. Mhe. Naibu Spika, ikiwa tutakuwa hivyo tutakuwa tumefikia malengo.

Nikitoka hapo nije katika madawa ya kulevya. Madawa ya kulevya kila siku yanaongezeka na wanaotumia madawa hayo nao wanaongezeka tunao mitaani tunaishi nao, kwa nini hatutungi sheria inayowadhibiti hawa. Leo mtu ukimpa kesho alilolipata kule *Sober House* basi anaweza kwenda kutubia kwa yale yale madawa ya kulevya, ni afadhali kuwe na sheria maalum ambayo inawadhibiti. Mhe. Abdalla Juma Abdalla kazungumza hapa ni bora kuwapeleka huko jela wakenda wakakaa ijapokuwa adhabu haitakuwa kubwa, lakini watakosa kupata yale yalioko nje na akitoka pale amepata mafunzo. Lakini bila ya hivyo kila siku tutatenga fungu na tutatumia fedha za wananchi walipa kodi wetu na hatuna mafaniko yoyote tunayoyapata hapa.

Kwa hayo machache Mhe. Naibu Spika, nasema ahsante sana na naunga mkono hoja.

Mhe. Raya Suleiman Hamad: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu (*S.W*) aliyetuwezesha kufika hapa na akatuamrisha kusema. Halafu nimpongeze Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais mwanamke Bi. Fatma Abdulhabib Ferej kwa kitabu na hotuba nzuri na kilichozingatia mambo mengi sana. Nampa hongera sana na nampongeza.

Mhe. Naibu Spika, mimi sitazungumza sana kwa sababu watu wameshazungumza lakini ni wajibu wangu kusema. Mimi nitazungumza kidogo tu ukurasa wa 28 kifungu 54.

Mhe. Naibu Spika, kifungu 54 walemavu kwanza tuseme kuwa katika nchi ndio watu duni, ndio watu waliokuwa wanaishi na mazingira magumu. Huyu hawezi hata kupokea mkoba wa mtu akasema angalau nikamuwekee pahala anigaiye shilingi hawezi. Lakini vile vile ndugu yangu hapa anasema kuwa walemavu wanakuwa ni omba omba. Namwambia omba omba ni watu aina zote waliokuwa walemavu na wasiokuwa walemavu na wengine ni watu na nguvu zao wana tabia hizo. Hawa tukisema wanaomba watakuwa wanaomba kwa akili zao lakini kuna na wengine ni hali duni sio walemavu ni waombaji. Kwa hivyo, serikali iwe makini katika watu hao.

Mimi nataka niseme tu kwamba walemavu kuna wa hali ngumu na katika walemavu wa mijini na wa vijijini. Walemavu wa vijijini ni watu walio na hali ngumu sana. Tukitembelea katika hali za watu wenye ulemavu kwenye vikundi, kwenye taasisi, walemavu wa vijijini ni watu ambao wanaishi katika hali za mazingira magumu na ni watu ambao ni duni kimaisha.

Mhe. Naibu Spika, walemavu wa vijijini hawana visaidizi, wananyanyapaliwa kijinsia kwa hali na mali tusikatae. Mimi napita katika vijiji hata elimu zao ni duni kwa sababu kuna walemavu wa aina mbali mbali. Mimi Mhe. Naibu Spika, namuona pale nguo aliyovaa na nyuma yake najua kumeandikwa kitu gani, lakini kuna watu hawaoni, walemavu wa *ZANAB* hawaoni, kuna watu wa akili wana mazingira magumu katika skuli zao hadi wapatikane walimu wa taaluma zinazoendana na wao. Tunaiomba serikali katika kusomesha walimu wachague walimu wanaowasomesha fani hizi za watu hawa kuweza kuwasaidia kupata elimu.

Kila siku hapa mimi nasema Mhe. Naibu Spika, kwa nini tuwe na elimu ya mazingira haya kuwa kila pahala iwepo moja, pale ipo Michakaeni, mtu atatoka wapi Kisiwapanza amlete mtoto pale, au atatoka wapi mtoto Msuka aletwe pale. Tulisema tujengewe kila wilaya skuli kama zile za mahitaji maalum, watu waliokuwa wana mahitaji maalum, wale wengine ambao tunaweza kuingia kwenye elimu mjumuisho tutaingia.

Mimi na mama Asha tukiingia na Bi, Fatma akisomeshwa na mimi nasiki naona kama yeye, kila mmoja na akili yake lakini hawa wana matatizo ya vifaa hakuna. Kuna mashine ndogo ndogo za kusomea hakuna za mitanuru, ukienda watoto wanakaa walimu wale wanapewa mzigo hajui mtoto yule awasiliane naye vipi, hajui amsomeshe vipi, hataki upumbavu anatoka anamuacha hapo hapo. Tunaomba serikali ijitahidi sana katika watoto hawa

na hizi skuli kila Mkoa ingejengwa moja au pengine ijengwe moja tu japo kwa Pemba ya ghorofa mbili ya hawa wenye mazingira magumu, watoto wawe skuli pale wawekwe mpaka *boarding* tutalipia, waweze kujikwamua watoto hawa kimaisha tusiwachanganye tu katika watu wote tukasema kwa kuwa tumetaka tusitengwe, hata kama hawatengwi hawapati elimu.

Mimi nimeshakwenda skuli kukagua watoto hajui mwalimu kumuelekeza aliyekuwa haoni kuwa upande wako aliyepo ni Fatma au ni Moh'd hajui, anatoka mtoto pale anataka kwenda chooni hajui kumuelekeza kuwa mkono wa kushoto yako ndio kwenye choo. Kwa hili tusikatae tuna mazingira magumu ya watu hawa na serikali mpaka ijipange.

Halafu hapa pana vikundi kumi vilivyopata shilingi 1,700,000 kwa kila kikundi na mimi nashukuru vikundi vyangu vimo, jumuiya yangu imo na jumuiya yangu ya wanawake imo. Lakini nataka niulize hizi pesa wamepewa taslimu au pesa hizi wamenunuliwa vifaa wakakabidhiwa vifaa Mhe Waziri atueleze. Ikiwa wamekabidhiwa vifaa tupate *data* kifaa gani na gani cha pesa hizi walizosaidiwa. Kwa sababu hawa kwa kuweka pesa hivi tu, tukasema wamepewa hatujui kama ni taslimu mkononi au ni vifaa au vipi na kwa kila jumuiya ina matatizo yake.

Halafu Mhe. Naibu Spika, tukitaka tusitake kipindi tulicho tunakwenda na wakati, wenzetu katika dunia watu wenye ulemavu wanawawezesha, tunaomba serikali ifanye jitihada yoyote ya kuweza kuwezeshwa watu wenye ulemavu na katika skuli zitengwe gari za kuwachukua watoto hawa kuwapeleka skuli kwenda na kurudi. Nimeingia kwenye gari siku moja akaingia mtoto mlemavu, mlemavu huyu ni mlemavu wa ngozi hawa tunaowaita Albino. Nikaingia natoka Wete kwa sababu utundu wangu mimi wakati mwengine huwa sipandi gari yangu napanda gari hizi hizi za kawaida, kwa sababu usitoke kule ukaacha mbachao kwa msala upitao, ujifundishe.

Mhe. Naibu Spika, tukaja zetu mpaka njiani, kwa kweli mtoto yule alivyonyanyasika niliumia ndani ya tumbo kama mzazi, tena aliyekuwa akimtolea maneno ni mtu aliyekuwa yuko serikalini na yeye ndiye anayelinda jamii ambaye kuwa ni askari, ikabidi tumsimamishe dereva tukamwambia askari ashuke au tutateremka sisi. Haiwezekani kuwa sisi tuonekane kuwa huyu ni mlemavu na wewe jiwekee siku moja utakuwa ni mlemavu, sio kama Mwenyezi Mungu kakuumba mpaka uondoke duniani kuwa hutakuwa mlemavu, kuna maradhi aina kwa aina yanaweza kukupata. Tunaomba unyanyapaa kwa watu wenye ulemavu iwe ni marufuku, Mhe. Waziri akazie sheria atuwekee tukikuta mlemavu kafungwa kibwebwe anachezeshwa mtu achukuliwe hatua asimdhalilishe kwa sababu mtu yule kamuona ni duni akajiona yeye ndiye sahihi hatutaki.

Mtu mwenye ulemavu kugeuzwa majina hatutaki, mtu akiitwa jina lake kuwa ni Halima akaitwa UKIMWI, ikiwa jina lake nani akaitwa jina jengine hatutaki. Hawa ni watu kawaumba Mwenyezi Mungu ni sawa sawa na nyinyi. Kwa hivyo, tunaomba tupate haki binafsi kama wenzetu wote, kuanzia elimu, matibabu, malazi, mavazi, tuolewe, tufanyiwe haki zote. Mlemavu anamzaa mzima na mzima akamzaa mlemavu. Mimi ni mlemavu Mwenyezi Mungu amenipa watoto nimeolewa nimewapata sina mtoto hata mmoja aliyekuwa ni mlemavu, ni gere nikiwaletea hapa nyote mtaona wazima safi kwa sababu Mwenyezi Mungu hiyo ndio fani yake kwa nini mtunyanyapae, ikiwa wewe unakwendea magongo, au bakora ni sawa tu. Humo vijijini tukienda tunapata malalamiko mbali mbali, hiyo hali ni tete

Halafu mimi natoa wito katika jumuiya yangu ya watu wenye ulemavu katika kutoa mafunzo watu wenye ulemavu kila siku tunapata malalamiko wasiende wale wale tu Raya Suleiman na wenzake kwa kuwa tuko juu. Wachukuliwe watu vijijini kupewa taaluma. Utakwenda kwenye warsha kila siku unakuta watu wale wale hawabadiliki hata mara moja kwa sababu gani. Ikiwa ni Mjini/Magharibi wanakuwa watu hao hao kila leo ukienda Mkoani unakuta hao hao kila leo. Mhe. Waziri ukienda huko mabondeni ndiko utakuta walemavu wa aina zote na watoto wenye ulemavu wanaoshi katika hali ngumu.

Mafunzo yakitolewa vijijini watu wapewe taarifa wapate hayo mafunzo wasichukuliwe walio mjini tu na wao ni watu. Kwenye jumuiya hivi sasa wanakwambia hatutaki maana yake mnaandikisha wakubwa wanakula pesa zao sisi mnachukua majina, nyinyi ni watu wa taifa mnatudhulumu. Haiwezekani Mhe. Naibu Spika, haya malalamiko yapo. Kwa hivyo, mimi naomba watu wangu wenye ulemavu katika jumuiya tutizame sana tutapokwenda kufanya warsha zetu, ikiwa tunampa mtendaji barua tunakuja kufanya mafunzo, tukienda aliyefanyiwa mwaka jana na mara hii mwambie mimi sifanyi nitakaa hivi hivi sababu wako wengi.

Mhe. Naibu Spika, tunataka tupate takwimu sasa kwa sababu walemavu ni wengi na wanazaliwa asubuhi na jioni. Wanaume ni wangapi, wanawake ni wangapi, watoto ni wangapi. Hapo ndio serikali itakapojua kutupangia yale malengo ya kuweza kufanya kazi zetu na kuweza kutusaidia. Halafu asipelekwe mtu na miguu yake akenda akaambiwa akaandike atamuandika amtakae. Wapeni kazi watu wenye ulemavu kuanzia vijijini mpaka mjini kuwatafuta hawa wakuandikie walete orodha. Orodha iwepo kwa Makamu wakati sasa hivi ndiye anayetushughulikia ili aijue kama kwenda kuomba misaada wajulikane ni watu 300 au 200. Ijulikane kila Shehia ina watu wangapi hapa ndipo tutakapoweza.

Halafu hapo kwenye visaidizi kweli visaidizi vinaletwa nafsi yangu mimi nimekwenda kutembele mwahala nimeviona visaidizi nimeambiwa vimeletwa. Mhe. Naibu Spika, walemavu hawapewi mpaka walipe atoe wapi pesa. Tunataka tujue hivi visaidizi wameletewa wasaidiwe au wameletewa wanunue tuelezwe. Kwa sababu hii ndio hali halisi tusifichane ataambiwa achangie kisaidizi atoe laki nne au mbili na jumuiya isaidie, haiwezekani kuna wengine hawatimizi hata shilingi, hawana kazi wazee ni walemavu siku nyengine na watoto ni walemavu. Tukija katika maskuli hapa tupate msamaha nimeshakwenda kutembelea nakuta watoto wanazuiliwa kwa sababu hawatoi ada, mtoto mwenye ulemavu unajua kipindi kilichopita waziri alitoa msamaha wa watoto hawa. Kwa hiyo, mimi sina mengi naunga mkono hii hotuba ya Mhe. Waziri lakini naomba azingatie na yale niliyoyataka kuyauliza vile vile atupe majibu sahihi. Ahsante sana. (*Makofi*).

Mhe. Asha Bakari Makame: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwanza na mimi nichukue nafasi hii nimshukuru Mwenyezi Mungu ambae ametuwezesha siku hii ya leo kuwepo hapa katika hali ya afya na uzima.

Vile vile nimpongeze Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake ambao wamemsaidia kwa hotuba hii mwanana ya kutoa dira ya kuweza kufanyakazi. Mhe. Naibu Spika, na mimi nitarudia tu kwa sababu watu wengi wameshazungumza mambo muhimu lakini na mimi ni wajibu wangu.

Mhe. Naibu Spika, mimi nije tena katika watu wenye ulemavu. Kwa kweli kipindi cha mwaka jana tulipopitisha bajeti hii tulizungumzia suala la watu wenye ulemavu. Namuomba sana Mhe. Waziri watu wenye ulemavu ingawa mheshimiwa hapa amesema kwamba sote walemavu na ni kweli. Lakini ukiangalia idadi ya watu wenye ulemavu sio wengi ni vizuri wizara hii husika na watu wenye ulemavu wakapita kila kipembe kuhakikisha wanachukua majina na takwimu nzuri ili wakati wa kusaidia Mhe. Naibu Spika, waweze kuwasaidiwa hawa ni watu ambao kwa kweli hawajiwezi.

Lakini mimi namuomba Mhe. Waziri suala hili akae alitafakari ahakikishe kwamba watu wenye ulemavu wanasaidiwa kama wenzangu walivyosema. Hawa hawawezi kujihudumia, hawawezi kutoleshwa ada ya skuli. Hawa ni watu ambao Serikali ihakikishe inatenga fedha maalumu za kuwahudumia watu wenye ulemavu. Tunachukua pesa tunayafanyia mambo mengine ambayo hata ya kufanyiwa hazifanywii hizo pesa zinaangamizwa. Namuomba sana Mhe. Waziri kwamba watu wenye ulemavu awaangalie kwa busara, kwa sababu na hawa na wanao wana haki kama aliyonayo mtu ambaye hana ulemavu, ni haki yao katika nchi yao.

Nije katika athari za madawa ya kulevya wenzangu wamezungumzia sana Mhe. Naibu Spika. Lakini hapa mimi naona tumeshika tu *cocaine*, *heroine* tumesahau moja ambayo inawatia wazimu watoto wetu bangi. Ulevi wa bangi ni ulevi mbaya Mhe. Naibu. Siku hizi hapa Zanzibar mtu anakuvutia bangi mpaka chini ya miguu anavuta hata habari hana na bangi yake mkononi na hili suala la bangi nalo ni suala baya sana, vijana wetu wamepotea sana hawana akili kwa sababu ya bangi. Tusifikirie tu madawa haya ya *cocaine* na *heroine* lakini na bangi nayo ni mbaya sana kwa binadamu. Ingawa wenzetu wengine huko wanafanya ndio chakula lakini sisi si vizuri tukawaachia vijana wetu hawa bangi nayo ikaendelea kuvutwa.

Mhe. Naibu Spika, hao watu ambao wameathirika na madawa ya kulevya nayo pia yanachangia mambo ya Ukimwi. Nimuombe sana Mhe. Waziri kwamba kifungu maalum kitengwe katika *Sober House*. Mhe. Naibu Spika, tulikwenda kutembelea *Sober House* utaona imani na utaona huruma, na wala asikudanganye mtu hakuna dawa ya sindano ya kusema huyu amzuie madawa ya kulevya. Ni wao wenyewe kwa masomo yao wanayoyasoma. Namuomba sana Mhe. Waziri ahakikishe anashirikiana na Mhe. Waziri wa Uwezeshaji ili hizi *Sober Houses* ziwezeshwe kuhakikisha wanajikwamua wao wenyewe katika mambo ya umaskini. Kwa sababu ukimuwezesha yule akiondoka pale atakuwa na mtaji hatokuwa na haja kwenda kuiba hatokuwa na haja ya kupora, hatokuwa na haja ya kuwadhalilisha wazee wake katika mambo ya kuiba. Namuomba sana Mhe. Waziri *Sober Houses* ni muhimu.

Kwa hivyo, ashirikiane na Waziri wa Uwezeshaji kwa sababu tulipokwenda kwenye kamati tuliwachukua watoto wa *sober houses* tukawapeleka Wizara ya Uwezeshaji, kuna mipango mizuri Mhe. Waziri ameipanga. Sasa ni vizuri na wewe mwenyewe Mhe. Waziri kwa sababu hili liko katika Ofisi yako ukashirikiana na Mhe. Waziri wa Uwezeshaji ili kuhakikisha vijana hawa tunawawezesha. Lakini jengine kubwa zaidi sijui ni mara ngapi kwa sababu huko nyuma kulikuwa na kamati ya watu wenye kushughulikia madawa ya kulevya. Ile kamati ipo au imeshakufa, ni vizuri kamati kuifufua kamati ile watu hawa waweze kuwashirikisha na wazazi wao. Kwa sababu kuna vijana wengine wanasema wazazi na wao hawawataki tena. Na mimi nachukuwa nafasi hii kuwaomba wazazi kama ulivyopata shida ya kuchukua mimba mwezi wa kwanza mpaka mwezi wa tisa ukaweza kuzaa kiumbe ambaye amekupa Mwenyezi Mungu, nawaomba wazazi wasiwasusie wala wasiwanyanyapae ni vizuri wakawa na watoto wao ili kuhakikisha wanaweza kuwatumia kwa mambo mengine. Nakuomba sana Mhe. Waziri uwe una vikao vyako kwa kila baada ya kipindi kuwaita wazazi wa *Sober houses* pamoja na wao wenyewe ili na wao wakaweza kupata taaluma ambayo inaweza kusaidia.

Kwa kweli Mhe. Naibu Spika, bado mazingira yetu hayaridhishi katika nchi. Tunasema sana humu kwenye Baraza lakini hatua zinazochukuliwa kwa kweli si za kuridhisha. Mimi niseme kwamba ni vizuri Mhe. Waziri yeye mwenyewe akajihangaisha angalau kidogo akawa anapitia sehemu za mazingira kuona hali halisi ilivyo si vyema kukaa tu kwa sababu kuna baadhi ya watendaji wetu kwa kweli tukiwaendekeza tutashutumiwa kila siku humu kwenye Baraza. Namuomba sana Mhe. Waziri.

Mwisho namshukuru sana Mhe. Mohammed Haji Khalid jana alinipa sifa nyingi sana. Lakini ndio mimi Asha Bakari kada wa Chama cha Mapinduzi na mwengine yeyote yule ni feki. Niseme kwamba chama changu kimenipa mafunzo na sio mimi tu hata wao miongoni mwao waliotoka kwenye Chama cha Mapinduzi walipewa mafunzo mazuri sana ya ukada. Kwa hivyo, na wao wajue kwamba walipata mafunzo kutoka Chama cha Mapinduzi. Baada ya kusema hayo Mhe. Naibu Spika. Ahsante sana. (*Makofi*).

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii nikamalizia huu muda uliobakia unanitosha kabisa sina mengi ila na mimi wajibu wangu mbele ya wananchi au mbele ya nchi hii kuyazungumzia yale mambo ambayo yanahitaji kushughulikiwa na Serikali.

Namshukuru sana Mhe. Waziri kwa hotuba yake na maelezo yake ambayo ameyatoa katika kitabu hiki. Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri kwenye hotuba yake ametueleza kwamba malengo makuu ya ofisi yake ina jukumu la kusimamia na kuratibu masuala ya mazingira watu wenye ulemavu, udhibiti wa madawa za kulevya na Ukimwi, na ameyataja malengo makuu katika Ofisi yake kama ni manne.

Mhe. Naibu Spika, Ofisi hii ina majukumu makubwa na mazito na ni muhimu katika nchi yetu. Kama majukumu haya hayatosimamiwa ipasavyo basi nchi yetu itapata athari kubwa sana. Suala la mazingira, madawa ya kulevya ni janga la taifa. Kwa hivyo, ni jukumu la Ofisi hii kuhakikisha inasimamia ipasavyo.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri ameweka vipaumbele kama kumi ambavyo vipaumbele hivi amejipangia kuvitekeleza kwa mwaka huu wa fedha 2013/2014. Hivi ni vipaumbele ambavyo viko karibu kila sekta anavyosimamia lakini mimi leo nitazungumzia zaidi na kwa muda ulipo katika eneo moja hili ni muhimu sana.

Kipaumbele cha tatu ambacho amezungumzia kwamba alichokipata ni kuhusu kukabiliana na athari za kuhimili mabadiliko ya tabia ya nchi. Mhe. Naibu Spika, mabadiliko ya tabia ya nchi yanasababishwa na mambo mengi

ikiwemo ukataji wa miti ovyo, ujenzi usiozingatia sheria. Lakini pia mabadiliko ya tabia ya nchi yameshababishwa zaidi na wenzetu wakubwa wenye viwanda vikubwa huko ambayo yameshababishwa na hewa ukaa.
Sasa sisi kwetu katika nchi maskini nchi za dunia ya tatu hatuna viwanda vikubwa kama hivyo ambavyo vinaweza kuathiri, wenzetu nchi za Ulaya, Marekani, Japani huko ndio wenye viwanda vikubwa na kila wakati walikuwa wakishawishiwa kupunguza viwanda hivi ili tuepukane na mabadiliko haya ya tabia ya nchi na kupunguza hewa ukaa.

Lakini pamoja na maazimio mbali mbali na mikutano mbali mbali kwao imekuwa ni vigumu kwa sababu ni sehemu ya uchumi wa nchi zao. Lakini kwa kuwa janga hili litakuwa haliwaathiri wao na kuepukana nalo ni jepesi kwa sababu wana utajiri mkubwa. Sisi nchi zetu ni maskini lazima sasa tuchukue hadhari ya kujikinga na yale mambo ambayo yatasaidia katika kuepukana na mabadiliko haya ya tabia ya nchi ikiwemo kupanda miti kwa wingi ili tuweze kupata nafuu juu ya jambo hili.

Sasa Mhe. Waziri hapa moja kati ya vipaumbele vyake ni kukabiliana na mabadiliko ya tabia ya nchi. Sasa nimuulize Mhe. Waziri ni kwa kiasi gani ofisi yake imejipanga hasa katika eneo hili kwa kushirikiana na Wizara inayohusika Wizara ya Kilimo na Maliasili wamejipangaje. Na kwa sababu nchi hii kulipandwa miti mingi ukihesabu miti iliyopandwa katika nchi hii kama ingekuwa inashughulikiwa ipasavyo basi nadhani tungekuwa tunazungumzia lugha nyengine. Lakini inaonekana miti imepandwa kwa wingi lakini haishughulikiwi na matokeo yake sasa imekuwa kama vile hakuna jambo lolote ambalo limeweza kufanyika. Kwa hivyo, Mhe. Waziri katika eneo hili unatakiwa ujipange na wahakikishe kwamba miti inapandwa kwa wingi katika maeneo mbali mbali lakini isitoshe inahifadhiwa. Si suala la kupanda mti leo na baada ya wiki moja unapotea tutakuwa hatufanyi chochote.

Lakini jengine Mhe. Naibu Spika, ni uharibifu wa mazingira ni ujenzi usiozingatia sheria hasa katika maeneo ya fukwe na hili niliwahi kutangulia kulisema. Eneo hili nalo linasababisha uchafuzi mkubwa sana wa mazingira na kusababisha baadhi ya maeneo kupata athari hasa katika maeneo ya visiwa vidogo vidogo kama Kisiwa Panza na visiwa vyengine vya Mnemba.

Lakini pamoja na athari ya mazingira suala la ujenzi usiozingatia masharti watu wanaojenga kwenye Fukwe kunasababisha visiwa vile kuathirika na hili wala halitaki utaalamu. Kama maji ya chumvi yamejaa kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa yanakwenda wanagonga katika kuta matokeo yatarudi yataathiri vile visiwa vilivyoko na hatimae visiwa vile vitakuwa vinapata mmong'onyoko mkubwa.

Kwa hivyo, suala la ujenzi holela, suala la ujenzi usiozingatia athari za kimazingira nalo ni eneo moja kubwa ambalo Mhe. Waziri unapaswa kulishughulikia ipasavyo. Pamoja na kwamba umekuwa na maelezo mengi sana katika eneo hili kwamba wewe huna sheria mwenye sheria ni majenzi na mambo mengine. Lakini wewe ni msimamizi wa mazingira unatakiwa uchukue hatua juu ya jambo hili. Kama hakuna sheria itengenezwe sheria. Kwa kweli huo haujawa msamaha katika Ofisi hii kwamba huna sheria huna hivi. Sasa hivi hapa tuna karibu miaka miwili na nusu tumepitisha sheria mbali mbali tungetegemea na sheria hii itakayokupa wewe uwezo wa kuyashughulikia majengo yale au maeneo yale basi ingekuwa imeshawasilishwa hapa Barazani ili ipate nguvu ya kuchukua hatua.

Lakini bado unayo nafasi ya kushirikiana na zile taasisi ambazo zenye sheria sio kuziachia tu. Juzi Mhe. Naibu Spika, nilisikia Ofisi yako imechukua hatua za kuchoma misumeno ya moto jambo zuri ni hatua nzuri. Sijui katika kuchukua hatua ile ulitumia sheria aina gani lakini unaweza kuchukua hatua na kila mmoja akaona na hili linaonesha dhahiri kwamba tunatekeleza ule utaratibu kama huu uliozungumzwa wa kupambana na misumeno ya moto.

Pia umeweza kuchukua hatua mbali mbali juu ya mifuko ya plastik ambayo sasa hivi imepiga hatua kubwa. Sasa na hili Mhe. Waziri tunataka uchukue hatua hii ni jukumu lako la kuhakikisha unasimamia mazingira. Kipaumbele hichi ambacho umekiweka cha kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabia ya nchi hii ni *source* moja ambao inasababisha matatizo makubwa na inaleta athari kubwa katika nchi yetu.

Sasa hivi watu wanajenga karibu na fukwe wanajenga mahoteli wanajenga nyumba za kukaa zisizozingatia taratibu za kisheria, na wizara yako inakaa inaangalia tu inasema haina sheria. Lakini hata kama sheria huna lakini sheria si zipo Serikali hii inafanyakazi kwa pamoja, kama huna sheria wewe lakini mwenzio sheria anayo tunatakiwa tuzuie. Juzi Mhe. Naibu Spika, nimekweda katika maeneo ya Chwaka watu wameshazungusha makuta, mtu amezungusha ukuta watu wanataka kujenga nyumba katika maeneo ya Chwaka karibu na fukwe za bahari.

Je, hii kweli mtu anajenga kuta sisi tuko wapi Serikali za Wilaya ziko wapi, Halmashauri za Wilaya ziko wapi, Serikali za Mikoa ziko wapi. kwamba leo hivi tunazungumzia masuala ya uchafuzi wa mazingira watu ndio kwanza wanajenga karibu na fukwe za bahari. Nenda Mhe. Waziri katika maeneo ya Chwaka kule watu wanajenga makuta ili mtu ajenge nyumba. Leo nini tunazungumza masuala la mabadiliko ya tabia ya nchi. Kwa hivyo, jambo la kusikitisha na Serikali lazima ichukue hatua na ikiwezekana nyumba zote zile

ambazo zimejengwa kinyume na taratibu basi zivunjwe ili tuepukane na kadhia hii.

Nchi yetu hii Mhe. Naibu Spika, ni visiwa na kama tutaendelea kuachia basi baadae tutakuja kupata athari kubwa, kwa sababu wakubwa huko wanaosababisha mambo haya wanaendelea na wao kinga wanazo, lakini sisi ni wanyonge maskini. Kwa hivyo, Mhe. Waziri nadhani hii ni eneo muhimu kwako na kulishughulikia ili tuone tunaepukana na mambo haya.

Mwisho Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa jambo hili tumekuwa tukilizungumza muda mrefu kupitia kamati wachangiaji mbali mbali hebu utakapokuja kufanya majumuisho utueleze kwamba katika usimamizi wako huu hasa katika maeneo ya ujenzi ni majengo mangapi ikiwemo hoteli na nyumba za binafsi kwa Unguja na Pemba ambazo mpaka leo hii zimejengwa kinyume na taratibu za kimazingira. Hebu uje utueleze kama umeshafanya tathmini tujue. Mhe. Naibu Spika, Baraza lako tukufu lijue kwamba katika visiwa vyetu vya Unguja na Pemba kuna hoteli kadhaa zimejengwa kinyume na taratibu na majengo kadhaa yamejengwa kinyume na taratibu angalau tuweze kupata picha. Kwa sababu sasa hivi tumekuwa tukisema na tunaona tu maeneo mbali mbali.

Mimi nimpongeze sana ndugu yangu Makungu yule wa hoteli ya *Zanzibar Ocean View* ameweza kuvunja jengo lake lote ambalo lilikuwa limejengwa kuzuia mazingira. Baada ya kusikia kelele za Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi amelivunja lote ameondosha amejenga sehemu inayostahiki. Sasa kwa nini hawa wengine bado wanaendelea kukaidi. Kwa hivyo, Wizara lazima ichukue hatua kama sheria sasa hivi huna tengeneza sheria uilete, lakini sheria zilizopo basi kwa kushirikiana na watu wenye sheria ili kuona jambo hili linakwenda kwa mujibu wa taratibu.

Kwa sababu hata hawa wazungu wanaokuja kujenga hapa mbona kwao wanajenga kwa mujibu wa taratibu au kwa kuwa sisi ni wanyonge. Kwao wanafanya tararibu zote za kisheria lakini wanapofika hapa kwa kuwa sisi wenyewe hatuko makini wanajaribu kila wakati kutuona kama sisi hatuna maana. Na ukizingatia kwamba wao ndio wachafunzi wakubwa sana wa mazingira katika maeneo ya viwanda. Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, baada ya maeneo hayo mimi naunga mkono hotuba ya Mhe. Waziri. Lakini kubwa tusisitiza juu ya suala hili la mazingira ambalo linaweza kuja kutuweka pahala pabaya siku za baadae.

Mhe. Naibu Spika, ahsante. (*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe niwashukuru kwa mashirikiano yenu mazuri tangu asubuhi hadi mchana. Niwaombe kwamba jioni tuje mapema ili kusikiliza hoja tulizomuuliza Mhe. Waziri akitoa majibu na baadae tumpitishie bajeti yake.

Nina tangazo moja nimeletewa na Mwenyekiti wa Uwawaza kwamba Wawakilishi wote wanawake yale mafunzo yapo kama kawaida na pahala pale pale. Kwa hivyo, mnaombwa kikiahirishwa kikao hapa muende kwenye mafunzo hayo.

Baada ya kusema hivyo naakhirisha kikao chetu hadi saa 11:00 leo jioni.

(Saa 7: 00 mchana Baraza liliahirishwa mpaka saa 11:00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Mhe. Spika, kwa heshima napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu, kutokana na michango yao na ushauri walioutoa katika kuchangia hotuba ya bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa mwaka wa fedha 2013/2014.

Mhe. Spika, ni ukweli usiopingika kuwa michango yote iliyotolewa imekusudia kufanikisha mambo yanayotekelezwa na ofisi yetu ambazo ni shughuli muhimu, mtambuka na kila mmoja wetu ni mdau katika masuala haya.

Mhe. Spika, kwa kweli michango mingi iliyotolewa ilikuwa katika njia ya mapendekezo na maelekezo na imenipa faraja sana, hasa pale nilipoona baadhi ya Waheshimiwa Wajumbe wakitoa michango ambayo kila mmoja wetu ameona kuwa ni michango muhimu kwa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais.

Mhe. Spika, napenda kuwahakikishia Waheshimiwa Wawakilishi kuwa michango yao yote tumeipokea na tutaifanyia kazi.

Mhe. Spika, naomba niwatambue kwa kuwataja majina yao wale wote ambao walipata nafasi ya kuchangia kwa maneno na pia kwa maandishi, ambao ni hawa wafuatao.

1. Mhe. Hamza Hassan Juma

2. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
3. Mhe. Saleh Nassor Juma
4. Mhe. Ali Salum Haji
5. Mhe. Mbarouk Wadi Mussa
6. Mhe. Mohamed Haji Khalid
7. Mhe. Ismail Jussa Ladhu
8. Mhe. Marina Joel Thomas
9. Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali
10. Mhe. Bikame Yussuf Hamad
11. Mhe. Salma Mohamed Ali
12. Mhe. Hija Hassan Hija
13. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa
14. Mhe. Mohamed Mbwana Hamad
15. Mhe. Salum Abdalla Hamad
16. Mhe. Rufai Said Rufai
17. Mhe. Panya Ali Abdalla
18. Mhe. Mgeni Hassan Juma
19. Mhe. Abdalla Juma Abdalla
20. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu
21. Mhe. Hassan Hamad Omar
22. Mhe. Raya Suleiman Hamad
23. Mhe. Asha Bakari Makame
24. Mhe. Salmin Awadh Salmin

Mhe. Spika, waliochangia kwa njia ya maandishi ni;

1. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa
2. Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi
3. Mhe. Salma Mussa Bilali, na
4. Mhe. Shadya Mohamed Suleiman

Mhe. Spika, naomba niwashukuru wote hawa pamoja na ambao walitulia kimpya katika kuona kwamba wanaochangia wanapata fursa ya kueleza mawazo yao vizuri sana, nawashukuru sana.

Sasa Mhe. Spika, naomba nianze kutoa ufafanuzi pamoja na majibu ya maswali yaliyoulizwa na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa kupitia kila idara.

Ofisi ya Faragha

Mhe. Spika, Mhe. Makame Mshimba alitaka kujua juu ya bajeti ya Idara ya Ofisi ya Faragha ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais ambayo ni shilingi

milioni 515 ambayo anaiona imeongezeka. Napenda kumfahamisha kwamba bajeti hii imeongezeka kutokana na ununuzi wa gari ya Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais huko Pemba, kwa sasa Mhe. Makamu hana gari. Kodi ya nyumba Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais ambayo inategemewa kupangiwa nyumba huko Dar es Salaam. Lakini pia ununuzi wa vifaa vya ofisi kwa vile bado ofisi hii ni mpya na inaendelea kununua vifaa kuiweka katika hali bora zaidi ya utendaji wa kazi.

Mhe. Spika, kuhusiana na safari za Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais. Napenda kutoa ufafanuzi ufuatao. Jumla ya ziara tatu za nje ya nchi zimefanyika kwa mwaka wa fedha 2012/2013, ziara ya kwanza nchini Marekani kwa mualiko kutoka *National Democratic Institute* iliyofanyika Septemba 2012. Ziara hii ilihusiana na masuala ya uchaguzi na demokrasia, baada ya ziara hii alifanya ziara Washington ambapo alipata kuonana na *US Secretary of State* na kuwasilisha maombi kadhaa kwa Serikali ya Marekani, yakiwemo ya *Roadmap* ya dawa za kulevya na *Incinerator* ya Wizara ya Afya. Pia alifanya ziara ya matibabu nchini India ambayo ilifanyika mwezi wa Disemba mwaka huu na hivi sasa yupo ziarani nchini Seychelles kuanzia tarehe 20 - 27/06/2013.

Kifungu cha kodi ya nyumba ya Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais kimepanda kutoka shilingi milioni 24 za mwaka jana hadi milioni 98. Hii imesababishwa na kodi ya nyumba ya Pemba kwa mwaka wa fedha 2013/2014 na matarajio ya kukodi nyumba ya Dar es Salaam ambayo ni wastani wa dola 3,000 kwa mwezi.

Aidha, ni kweli kwamba gharama za kukodi nyumba ni kubwa na hasa ukilinganisha na hadhi ya Kiongozi. Serikali inajipanga kwa ujenzi wa nyumba za viongozi wa kitaifa, kwa kuanzia na ujenzi wa nyumba za Pemba. Kwa upande mwengine serikali inaendelea kujenga nyumba za ofisi za serikali hatua kwa hatua.

Kuhusiana na ununuzi wa jenereta ni kwamba hili ambalo limenunuliwa katika kipindi cha mwaka huu cha utekelezaji, ni kwa ajili ya ununuzi wa ofisi Unguja na linalotarajiwa kununuliwa ni kwa ajili ya matumizi ya nyumbani kwa Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais, nyumba ambayo iko Pemba.

Mhe. Spika, suala la uwiano wa bajeti ya Ofisi ya Faragha ya Makamu wa Kwanza na Ofisi ya Makamu wa Pili ambalo limeulizwa na Mhe. Hija Hassan liko katika taswira ifuatayo. Kwa upande wa Ofisi ya Faragha ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, jumla ya bajeti yao ni shilingi milioni 780, kati ya hizo shilingi milioni 244,072,000 ni mishahara na shilingi milioni 535,928,000 kwa kazi za kawaida. Kwa upande wa Ofisi ya Faragha ya

Makamu wa Kwanza wa Rais shilingi milioni 515,000,000 zimetengwa kwa matumizi ya kazi za kawaida. Fedha za mishahara yote zipo katika Idara ya Uendeshaji katika Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais.

Idara ya Mipango Sera na Utafiti

Mhe. Spika Wajumbe wengi walichangia kuhusu mradi wa kuangamiza kunguru weusi. Mhe. Spika, naomba kuchukua nafasi hii kuwashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe kwa pongezi walizotoa kwa ofisi yetu katika kusimamia suala la kunguru weusi. Aidha, kwa namna ya kipekee naomba nimpongeze Mhe. Saleh Nassor Juma, Mwakilishi wa Jimbo la Wawi kwa ueledi na ufahamu wake mkubwa wa mahusiano yaliopo baina ya viumbe, mazingira na mfumo wa kiikolojia.

Mhe. Spika, njia zinazotumiwa Zanzibar katika kuulia kunguru ni njia mbili kuu, yaani ya kutumia mitego na ya pili ni ya kutumia sumu. Njia hizi mbili ndizo sahihi za kuangamiza kunguru weusi zilizokubalika kimataifa na kikanda. Njia hizi zinatumika baada ya kufanya utafiti na majaribio maeneo mbali mbali duniani na kuonekana ndizo kuwa njia zinazoweza kuleta tija kwa shughuli hiyo. Sumu inayotumika imefanyiwa utafiti na kuonekana kuwa haina uwezo wa kukaa kwenye mazingira na kuleta athari kubwa kwenye mfumo wa kiikolojia. Njia ya kutumia makoho haijakubalika kimataifa, maana ndege hawa hula uchafu na mizoga, madhara ya ndege hawa baada ya kukosekana uchafu ana uwezo wa kula viumbe vyengine vidogo vidogo kama vile kuku na ndege wengine wa asili. Kwa hivyo, sio vyema kumtumia ndege huyo kwa ajili ya kazi ya kuangamiza kunguru hao.

Mhe. Spika, kunguru wameletwa Zanzibar kwa ajili ya kusaidia kuweka maeneo ya mji katika hali ya usafi. Napenda kuwafahamisha Wajumbe kwamba serikali imeanzisha Halmashauri za Miji ambapo pamoja na mambo mengine ni kusimamia usafi wa mazingira katika maeneo husika. Hivyo, ofisi yetu katika kuhakikisha jukumu hili linafanyika kwa ufanisi, itaandaa mkakati wa usimamizi wa taka ili uweze kutumika katika utekelezaji wa kazi hizi. Hii ni hatua muhimu ambayo inatoa mbadala wa kazi za kunguru weusi.

Mradi wa kunguru ulikuwa na lengo la kuangamiza kunguru wote, yaani *extermination.* Lakini katika kipindi cha miaka mitano, tumeweka lengo la kuangamiza kunguru 408,000 kwa mwaka na hadi sasa tumeweza kuangamiza kunguru 10,000 kwa fedha za serikali. Vita vya kupambana na kunguru ni vikubwa, kwa hivyo serikali itaendelea na zoezi hili mpaka kuhakikisha kunguru wote wameangamizwa. Naomba ifahamike kwamba sasa duniani hakuna mahala popote ambapo kunguru ameweza kutokomezwa

moja kwa moja, zaidi ya kisiwa kimoja kidogo kilichopo nchini Yemen. Inaonesha vita hivi vinahitaji nyenzo nyingi na za kutosha, ikiwa ni rasilimali fedha, rasilimali watu na pia kufanya utafiti pamoja na kutoa elimu kwa jamii.

Mhe. Spika Wajumbe walitaka kufahamu zaidi kama hakuna adui wengine ambao ni waharibifu wanaohitaji kuangamizwa kama kunguru weusi. Naomba nieleze kwamba wadudu kama panya, kima weusi na tumbili ni miongoni mwa viumbe ambao ni waharibifu na wadudu wengine ambao wanaangamiza na kuleta uharibifu wa mazao. Hao wote wanahitajika kufanyiwa juhudi za kutosha ili kupunguza uharibifu hasa wa mazao wanayofanya, ambapo Wizara ya Kilimo na Maliasili ndio msimamizi mkuu wa masuala hayo.

Mhe. Spika, Mhe. Salum Ali alitaka kujua vipi tunaweza kubagua baina ya kunguru vibaka na kunguru weusi katika uangamizaji wa kunguru kwa upande wa Pemba. Kwa upande wa uangamizaji kunguru unaofanywa na serikali umelizingatia hilo kwa kutopeleka mitego ya kunguru Pemba na badala yake imeonekana ni vyema kutumia sumu. Wakati wa kutumia sumu kunakuwa na hadhari kubwa ya kuhakikisha kuwa chambo kinachotumika kinatumiwa na kunguru weusi pekee. Pia maeneo yanayotegeshewa sumu ni maeneo yanayofikiwa na kunguru weusi peke.

Vile vile Mhe. Ali Salum Haji alitaka kujua matumizi ya mabeseni, mapanga na ndoo katika mradi wa kuangamiza kunguru. Vifaa hivi vinatumika katika kutoa huduma za mitego, ikiwemo kuwekea maji, kuwekea chambo, kukorogea sumu, kufyekea, kuchimba kwa ajili ya kufukia kunguru waliokufa na halikadhalika.

Aidha, sumu ilitosha na iliyobaki ni kilo moja na inaweza hata kutumika hata baada ya miezi minne ijayo. Hatuwezi kutengeneza sumu yetu hapa Tanzania, kwa sababu sumu hiyo inatayarishwa kwa leseni iliyothibitishwa kimataifa na bei ya kilo moja na nusu ya sumu iliyonunuliwa ni shilingi milioni 6,598,991,000.

Mhe. Spika, Mhe. Salma Mohamed alitaka kujua kwa nini utekelezaji wa mradi wa kunguru umehamishiwa Wizara ya Kilimo na Maliasili. Sababu kubwa ambazo zinapelekea shughuli hizo kuhamishiwa wizara hiyo ni hizi zifuatazo.

Kazi ya uratibu wa uangamizaji kunguru zinatekelezwa kupitia mchango wa serikali na wahisani, ambapo kwa sasa Wizara ya Kilimo na Maliasili ndio wanaopata fedha hizo za wahisani. Kwa hivyo, ni vyema suala hili liratibiwe

na taasisi moja tu, kuwa na takwimu zinazolingana na kusiwe na mpandiano wa takwimu na majukumu.

Idara ya Maliasili ina wataalamu wanaohusika na wanyama pori inayotosheleza kukamilisha kazi hiyo. Kwa muktadha huo, serikali imeagiza kuhamisha mradi huu kutoka Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais na kuupeleka Wizara ya Kilimo na Maliasili, kuanzia kipindi cha utekelezaji cha mwaka 2013/2014.

Mradi wa Mabadiliko ya Tabia Nchi

Mhe. Spika, nakiri kabisa kwamba suala hili ni mtambuka na kwa kiasi kikubwa ufanisi wa utekelezaji wake utategemea ushiriki wa wadau wote na kwa kulitambua hilo, mradi huu unatekelezwa na wadau kutoka sekta zote muhimu. Miongoni mwa matokeo muhimu ya utekelezaji wa mradi huu ni kuwa na mkakati wa mabadiliko ya tabia nchi, mkakati huu utatoa muelekeo wa utekelezaji wa vipaumbele vya kukabiliana na kuhimili athari za mabadiliko ya tabia nchi Zanzibar.

Aidha, suala la mchanganuo wa shughuli zinazotekelezwa kwa matumizi ya fedha za mradi huo ni kama zinavyohitajika na Mhe. Abdalla Juma ni kama ifuatavyo. Mhe. Spika, ninao hapa mchanganuo ambayo ni *document* kidogo refu sana, naomba niikabidhi *document* hii kwa Mhe. Abdalla Juma inayoonesha kabisa kila mdau ametekeleza shughuli gani. Nachelea Mhe. Spika, kuyasoma yote haya kwa wakati ambao kwa kweli ni mdogo na yaliyochangiwa hapa ni mengi mno.

Mhe. Spika, mradi wa kujenga kituo cha kurekebisha tabia. Ujenzi wa kituo cha marekebisho ya tabia haujaanza kutekelezwa kwa sababu fedha hazijaingizwa kama nilivyotoa taarifa ya utekelezaji wa miradi. Ofisi yetu imepangiwa kutumia shilingi milioni 100 ambazo zitaanza kutumika kwa shughuli za ujenzi. Mradi huu umepangwa kutekelezwa katika kipindi cha miaka mitano, mwaka 2012/2013 hadi 2017/2018. Ni imani ya ofisi yetu kwamba Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo itaweza kutenga fedha za kutosha ili kukamilisha ujenzi wa kituo hicho ndani ya muda uliopangwa.

Idara ya Mazingira

Mhe. Spika, naomba kuchukua fursa hii kuwashukuru Wajumbe wote waliochangia suala hili linalohusu sheria ya mazingira, wakiwemo Kamati ya Kusimamia Ofisi ya Viongozi Wakuu wa Serikali, Mhe. Makame Mshimba, Mhe. Ismail Jussa Ladhu na Mhe. Mbarouk Wadi Mussa.

Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, imechukua ushauri uliotolewa na kamati pamoja na wajumbe wote, kuwa tuharakishe kuwasilisha Barazani mabadiliko ya sheria ya mazingira. Ofisi yetu hivi sasa inayafanyia kazi marekebisho ya sheria hizo na ina lengo la kuiwasilisha sheria hiyo haraka iwezekanavyo. Aidha, ofisi imepokea ushauri wa kuwasiliana na taasisi nyengine, ili sheria za taasisi hizo zitumike pale ambapo sheria ya mazingira itashindwa kutumika.

Mhe. Spika, takriban Waheshimiwa Wajumbe wote waliochangia hotuba ya Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais, walichangia suala zima la uharibifu wa mazingira hasa unaotokana na usimamizi wa maliasili zisizorejesheka.

Mhe. Spika, maliasili zisizorejesheka yanaonekana katika maeneo mawili makubwa, ambayo ni uchukuaji wa rasilimali hizo kwenye maeneo yaliyoruhusiwa kisheria, lakini hakuna uendelezaji wa maeneo hayo. Pia uchukuaji wa maliasili hizo kiholela kwenye maeneo ambayo hayajaruhusiwa kisheria.

Mhe. Spika, katika kukabiliana na matatizo hayo, ofisi yetu imeandaa kanuni ya usimamizi wa maliasili hizo ambayo huko nyuma ilikuwa haipo. Kanuni hiyo itatoa fursa kwa ofisi yetu kusimamia vizuri na kuondokana na matatizo hayo. Operesheni mbali mbali zitafanywa kwa mashirikiano na polisi katika maeneo yanayochukuliwa mchanga kiholela na usimamizi wa kisheria umewekwa kwenye maeneo ambayo yanachimbwa kihalali.

Mhe. Spika, naomba nichukue nafasi hii kutoa wito kwa wananchi wote wa Zanzibar kufuata taratibu za kanuni mpya za maliasili, ili kupunguza athari za uchukuaji mchanga kwenye maeneo yaliyokuwa hayakuruhusiwa.

Mhe. Spika, ofisi yetu imechukua kwa dhati kabisa pongezi zilizotolewa za kusimamia ipasavyo marufuku ya mifuko ya plastiki. Pongezi hizi zinatuhusu wadau wote tunaoshiriki katika kusimamia kanuni hiyo, likiwemo Jeshi la Polisi, Baraza la Manispaa na Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko.

Mhe. Spika, naomba niwahakikishie Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwamba ofisi yetu pamoja na washirika wake na kamati ya kusimamia mifuko ya plastiki, hatutorudi nyuma katika kusimamia zoezi hili.

Mhe. Spika, tunashukuru kupokea mawazo ya Mhe. Saleh Nassor Juma juu ya biolojia ya mivinje kuwa inafyonza maji sana na haifai kimazingira na sio *nitrogen fixing species*. Ukweli ni kwamba duniani kuna aina 17 za mivinje na asili yake ni nchi ya Australia, baadhi ya nchi za Asia na Marekani ya Kusini. Aina ya mivinje tuliyonayo inaitwa *casuarina equisetifolia*, na tafiti

zinaonesha kuwa ina uwezo wa kutengeneza *nitrogen* na haikaushi ardhi kama vile mti wa mkaratusi. Mivinje imebainika kuwa na faida kubwa kwa kuongezea kipato kwa njia ya kuni na majengo.

Aidha, mivinje hukua haraka katika kipindi cha miaka mitano hadi kumi na imekuwa ni mbadala wa kupunguza utegemeaji na ukataji wa misitu ya asili ya maweni kwa kuni na makaa na pia miti ya kujengea. Si hayo tu Mhe. Spika, mivinje inashauriwa kupandwa kwenye maeneo ya maweni na yenye maji kidogo.

Mhe. Spika, ofisi yetu ilikuwa na nia ya kutayarisha kanuni za kupiga marufuku moja kwa moja uingizaji wa bidhaa chakavu za umeme na *electronic*. Hata hivyo, baada ya kushauriana na wadau imeonekana sio busara kupiga marufuku moja kwa moja uingizaji wa bidhaa chakavu, kwa kuwa bidhaa hizo zinachangia ajira na kuongeza kipato kwa wananchi, lakini pia ndizo wananchi wengi wetu ambao wanamudu kuzinunua. Kwa hivyo, ofisi yetu ilitakiwa kushirikiana na Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kutayarisha viwango vya uingizaji wa bidhaa hizo. Mawasiliano yamefanyika na ofisi yetu imeombwa kuipa muda Ofisi ya Bodi ya Viwango ya Zanzibar, ili iweze kujipanga na kutekeleza suala hili kwa ufanisi zaidi.

Mhe. Spika, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais imepokea ushauri wa kushirikiana na Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kutafuta njia bora ya kuondoa tatizo la kutuama kwa maji ya mvua katika eneo la Skuli ya Kisiwandui.

Mhe. Spika, ofisi yetu inakiri kuwepo kwa vikundi vya mazingira katika maeneo mbali mbali ya Zanzibar, ni wazi kuwa vikundi hivi vinahitaji msaada wa hali na mali, ili kuweza kufikia malengo waliokusudia. Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais itaendelea kuchukua jitihada ya kuvisaidia vikundi hivyo ili kufikia malengo yaliyokusudiwa, pamoja na kuvipatia ziara za kimasomo nchi za nje pale hali ya kifedha itakaporuhusu.

Mhe. Spika, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kupitia Idara ya Mazingira, ina maofisa wa mazingira kwa kila wilaya. Majukumu ya maofisa hao ni kuhakikisha kuwa shughuli za mazingira zinaendelezwa kwenye wilaya, ikiwa ni pamoja na kusaidia kutatua matatizo ya kimazingira kwenye maeneo ya wilaya. Aidha, ofisi yetu imepokea maoni ya Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza ya kuimarisha maofisa wa wilaya, ili kuongeza msukumo wa usimamizi wa mazingira.

Mhe.Spika, katika kufanya ukaguzi wa miradi, miongoni mwa mambo makubwa yaliyoonekana kwenye ukaguzi wa miradi hiyo 65, ni pamoja na

usimamizi duni wa taka, mmong'onyoko wa fukwe na ujenzi chini ya mita 30. Maelekezo ya usimamizi wa mazingira ya mambo hayo yametolewa.

Mhe. Spika, kuhusu ripoti ya Kiwanda cha Makonyo cha Wawi Pemba, ambayo wajumbe wametaka kupatiwa taarifa zake, ni kwamba ushauri mkubwa uliotolewa kwenye ripoti za ukaguzi wa kimazingira wa kiwanda hicho ni pamoja na hizi tatu. Kwanza kurekebisha *boiler* ya kiwanda hicho ili kupunguza uzalishaji wa moshi, ambao huenea wakati wa uzalishaji hapo kiwandani, kuimarisha bomba la kutolea moshi kwa kuweka jipya litakalokidhi haja ya kupunguza uchafuzi wa mazingira, lakini pia kuimarisha uzalishaji wa bidhaa za kiwanda hicho, ili uzingatiwe uzalishaji mdogo wa hewa ukaa kwa ajili ya kuongeza thamani ya bidhaa hiyo kimataifa.

Mhe. Spika, kuhusu suala la usimamizi wa taka na vipaumbele vya mazingira. Naomba nilifahamishe Baraza lako tukufu kwamba mara tu baada ya kuanzishwa ofisi yetu, ofisi ilijiwekea vipaumbele vyake, miongoni mwa vipaumbele hivyo ni suala la usimamizi wa taka. Majukumu ya ofisi hii kwenye suala la taka ni kutayarisha muongozo wa Zanzibar wa usimamizi wa taka pamoja na viwango vya mazingira na kusimamia utekelezaji wake. Mkakati huo utatoa majukumu ya kila mmoja kuweza kutekeleza kazi ya kukabiliana na usafi katika kipindi gani, fedha zitatoka wapi na viashiria ambavyo vitathibitisha utendaji wa kazi pamoja na njia ya kufuatilia, yaani *monitoring and evaluation*. Pamoja na yote hayo yataipa nafasi ofisi yetu kuweza kufuatilia kwa ukamilifu shughuli za usimamizi wa taka ndani ya miji yetu.

Mhe. Spika, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais imeorodhesha maeneo 123 kwa Pemba yaliyovamiwa na maji chumvi, na maeneo 25 kwa Unguja. Aidha, ofisi yetu hivi sasa imeshaanza zoezi la kuyaweka maeneo hayo kwa njia ya kitaalamu ijulikanayo kama *Geographical Information System*. Hadi sasa jumla ya maeneo 41 ya Pemba na maeneo yote ya Unguja yameshasajiliwa kwenye mpango huo, ujulikanao kama *Zanzibar Environmental Information Management System*. Kazi hii inatarajiwa kukamilika mwezi wa Disemba, 2013.

Mhe. Spika, kwa sasa ni vigumu Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kutoa taarifa kamili za eneo na ukubwa wa maeneo yaliyovamiwa na maji chumvi, hadi hapo zoezi zima hili litakapokamilika.

Mhe. Spika, kuhusu Idara ya watu wenye ulemavu. Idadi ya watu walemavu imeambatanishwa katika kiambatanisho nambari 6 ya kitabu cha bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais katika ukurasa wa 60. Aina mbali mbali za ulemavu ambao umo kwa watu wetu zimesajiliwa na ni kama

zifuatazo. Kwa upande wa Pemba wenye ulemavu wa akili ni 877, ulemavu wa ngozi ni 171, ulemavu wa uoni ni 757, ulemavu wa uziwi na matatizo ya kusema 1,352, ulemavu wa viungo ni 2,149, ulemavu mwengineo ni 385 na ulemavu mchanganyiko ni 952. Jumla kwa Pemba ni 6,445.

Kwa upande wa Unguja wenye ulemavu wa akili ni 621, ulemavu wa ngozi ni 141, ulemavu wa uoni ni 620, uziwi na matatizo ya kusema ni 809, ulemavu wa viungo ni 1,738, ulemavu mwengineo ni 213 na ulemavu mchanganyiko 844. Jumla kwa Unguja ni 4,986.

Mhe. Spika, idadi ya watu wenye ulemavu katika Mkoa wa Kaskazini Unguja ni kama ifuatavyo. Mhe. Mjumbe alitaka kujua kwa nini Wilaya ya Kaskazini haikuonekana ni kwa sababu *data* zake hazikukusanywa kiwilaya, zilikusanywa kimkoa na katika Mkoa huo idadi ya watu wenye ulemavu ni 3,200. Hata hivyo, ofisi hivi sasa inafanya mchanganuo wa kuweza kujua kila wilaya ina walemavu wangapi.

Mhe. Spika, idadi hii itakuwa ikiongezeka au kupungua siku hadi siku kutokana na vifo au kuzaliwa kwa watu wenye ulemavu. Mhe. Makame Mshimba anahisi kwamba kumuita mtu mwenye ulemavu, jina hili linadhalilisha. Naomba nimuarifu Mhe. Mjumbe kwamba sheria nambari 9 ya mwaka 2006 inatambua kuwa mtu mwenye ulemavu, yaani imem- *define* kuwa ni mtu mwenye ulemavu, wala haionekani kuwa ni lugha ya unyanyapaa. Wadau wa masuala ya watu wenye ulemavu na watu wenye ulemavu wenyewe wamekubaliana kuwa jina hilo linaondokana na unyanyapaa ambao Mhe. Mjumbe anadhani kuwa upo ndani yake. Suala muhimu hapa la kuzingatia ni kwamba tunaita mtu mwenye mlemavu na sio mlemavu.

Mhe. Spika, nakubaliana na Mhe. Makame Mshimba lakini pia na Mwakilishi wangu Mhe. Ismail Jussa kuwa ruzuku kwa Jumuiya za Watu Wenye Ulemavu ni ndogo. Hata hivyo, naomba niwaarifu Waheshimiwa kwamba ofisi yetu ilianzisha utaratibu huu na itakuwa inaongeza ruzuku hii kila hali ya fedha itakapokuwa inaruhusu. Aidha, kuhusu suala la ruzuku kutolewa kwa fedha taslim au vifaa, nakumbuka Mhe. Raya alililiuliza hili. Ofisi yetu imeweka utaratibu maalum wa kupokea maombi kutoka katika Jumuiya za Watu wenye Ulemavu kwa mujibu wa fedha zilizotengwa na kufanya manunuzi ya baadhi ya vifaa, na wengine huwapatia fedha taslim kutokana na matumizi waliyoyaomba, lakini hutakiwa warejeshe viambatanisho vya matumizi kama taratibu za fedha za serikali zinavyoagiza. Mhe. Spika, hili limezingatiwa katika kuona kwamba fedha hizi zinatekeleza yale majukumu ambayo taasisi hizi za watu wenye ulemavu wamejipangia, lakini hazigeuki kuwa zinakwenda mifukoni mwa watu binafsi.

Mhe. Spika, naomba kutoa ufafanuzi juu ya suala la matumizi ya shilingi milioni 25, lililoulizwa na Mhe. Mbarouk Wadi Mussa. Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais katika mwaka 2012/2013 kwa kupitia Idara ya Watu wenye Ulemavu iliomba milioni 25 kwa kupitia fedha za mradi kwa ajili ya kutengeneza *database* ya watu wenye ulemavu, ili takwimu za watu wenye ulemavu ziweze kuhifadhiwa na kuwa *updated* katika mfumo wa teknolojia ya kisasa. Fedha hizi hazikuingizwa kama tulivyoripoti katika kitabu chetu, badala yake Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo ikaona vyema fedha hizo za utengenezaji wa *database* za watu wenye ulemavu, kuziingiza katika fedha za matumizi ya kawaida kwa mwaka wa fedha 2013/2014.

Kwa hivyo, jumla ya shilingi milioni 30,000,000 zimetengwa kwa kazi hiyo na shilingi milioni 5,000,000 zitatumika kwa kutoa Mafunzo ya wataalamu wa ndani, ili mtaalamu mwelekezi atakapomaliza kazi yake, wataalamu wa ndani basi waweze kutumia *database* hiyo kwa maendeleo ya watu wenye ulemavu.

Mhe. Spika, aidha eneo la juu la jengo la Idara ya Watu wenye Ulemavu lina jamvi ambalo kwa sasa linavujisha sana, jambo ambalo linasababisha kuvunjika na kubanduka baadhi ya sehemu za ndani ya jengo hilo. Kwa hivyo, kabla ya kuleta athari zaidi, idara imetenga jumla ya shilingi milioni 25 kwa ajili ya ujenzi wa paa hilo linalohitaji kufanyiwa kazi.

Mhe. Spika, katika kuhakikisha kuwepo kwa mazingira rafiki ya watu wenye ulemavu, ofisi yetu kwa mwaka wa fedha 2013/2014 imepanga kuandaa sera madhubuti ya maendeleo ya watu wenye ulemavu, pamoja na kufanyia mapitio ya sheria nambari 9 ya mwaka 2006 ya haki na fursa sawa, ili kuhakikisha kuwepo kwa mazingira rafiki. Napenda kuwahakikishia kuwa miongoni mwa majengo mapya ya skuli 19 za sekondari zimewekewa mazingira rafiki kwa watu wenye ulemavu.

Mhe. Spika, kuhusu suala la serikali kuwa haina nia ya dhati ya kuwasaidia watu wenye ulemavu. Napenda kulithibitishia Baraza lako tukufu kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ina nia thabiti ya kuwasaidia watu wenye ulemavu. Tokea Mapinduzi ya mwaka 1964 serikali imekuwa mstari wa mbele katika kusimamia haki na fursa kwa watu wote wakiwemo watu wenye ulemavu.

Aidha, serikali imeanzisha idara kamili ya watu wenye ulemavu na kutayarisha sheria ya mwaka 2006 na Baraza la watu wenye ulemavu, ikiwa ni kazi ya kuratibu shughuli zote za watu wenye ulemavu hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, kuhusu vifaa vilivyotolewa na ndugu zetu walioko Canada. Nakumbuka Mhe. Hussein Ibrahim Makungu alitaka kulijua hili. Mhe. Spika, vifaa hivi viligaiwa kutokana na umoja wa watu wenye ulemavu. UWZ wenyewe walitupa wale watu ambao walitakiwa kupewa vifaa hivi, na walitoka Bumbwini Kiongwe, Kilindi, Kwarara, Kiembesamaki. Lakini pia walitoka Mikunguni, Bububu, Jozani na Hawaii. Mhe. Spika, havikuwa vifaa vingi sana ni jumla kama vigari 11 na vifaa vyengine vingi vilikuwa vya michezo ya watoto wadogo wadogo ambao waligaiwa watoto ambao wenye ulemavu kwa ajili ya kuchezea.

Mhe. Spika, naomba kwa ufupi sana, lakini kwa usahihi kujibu swali la Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, Mhe. Hija Hassan Hija na pia swali hili liliulizwa na Mheshimiwa mahiri wa Mhe. Ismail Jussa Ladhu ni kuhusu fedha ambazo zilitakuwa kutumika katika kununua visaidizi kwenye Idara hii ya watu wenye Ulemavu.

Naomba nikiri hapa kwamba kweli kuna tuhuma kwamba matumizi ambayo hayakufuata taratibu na sheria yalikuwepo katika suala hili. Lakini serikali imelifuatilia na mimi mwenyewe kama waziri nimelifuatilia na tumechukua hatua juu ya suala hili, hivi sasa liko kwa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, ambapo tumemuandikia aje kufanya ukaguzi na baadaye tunaweza kutoa taarifa zaidi ya kitu gani ambacho kimeonekana katika manunuzi hayo. *(Makofi)*

Idara ya Utumishi na Uendeshaji. Mhe. Fatma Mbarouk Said alitaka kujua lengo la kusimamia majukumu na utendaji wa wafanyakazi kwa mwaka 2013/2014 je halipo tena limeshafanikiwa na kwa kiasi gani.

Mhe. Spika, nakubaliana na wajina wangu huyu Mhe. Mjumbe, kwamba lengo hili halikuonekana katika mwaka huu kwa sababu zifuatazo. Kwa kweli utekelezaji wa lengo hili hauhitaji fedha na ni suala la usimamizi wa kila siku wa kazi za kawaida za idara. Kwa kweli wafanyakazi wote wameshapangiwa majukumu yao ya kazi na kazi zinaendelea.

Vile vile Mhe. Spika, katika hili naomba nieleze tu kwamba mara nyingi tunayapanga malengo yetu siku hizi kwa kuweza kuona kwamba vitatoa viashiria na kuleta ile *output* ambayo inategemewa kupatikana.

Tume ya Dawa za Kulevya. Mhe. Mbarouk Wadi Mussa alitaka kujua sababu zinazopelekea kushuka kwa bajeti ya Tume ya Uratibu wa Udhubiti wa Dawa za Kulevya. Mhe. Spika, napenda kuwafahamisha Waheshimiwa Wajumbe kwamba bajeti ya mwaka 2013/2014 haikushuka, isipokuwa ile ya mwaka jana ilikuwa imechanganywa na mishahara wakati mwaka huu imebaguliwa

baina ya mishahara na matumizi mengine. Kwa mfano, matumizi mengine mwaka jana yalikuwa ni shilini milioni 141 na mwaka huu ni shilingi milioni 160,117,000/=.

Mhe. Spika, napenda kuwahakikishia Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwamba serikali iko makini sana katika kudhibiti dawa za kulevya, hivi sasa serikali imeandaa mpango maalum wa utekelezaji wa Sheria ya Dawa za Kulevya kwa jina la kigeni tunaita *Roadmap*, ambapo utekelezaji wake unawahusisha wadau wa taasisi zote zinazohusika na mapambano ya dawa za kulevya.

Mpango huu tayari umeandaliwa, makisio yake ni makubwa na tayari ofisi yetu imeanza kuwasiliana na wahisani, pia serikali inafanya jitihada ya kuona kwamba fedha za utekelezaji wa mpango huo zinapatikana, ili shughuli hii iweze kufanikiwa.

Mhe. Spika, kuhusu suala la idadi ya watumiaji wa dawa za kulevya kwa mujibu wa *Size Estimation* ya mwaka 2012 watumiaji wa dawa za kulevya wanakisiwa kufikia 3000.

Mhe. Spika, suala la kuchangia mafuta kwa polisi katika za *Operation* ya Dawa za Kulevya, napenda kuwafahamisha Waheshimiwa Wajumbe kwamba kwa hivi sasa hatuna utaratibu huo. Lakini kama nilivyotangulia kusema awali kwamba ndani ya *Roadmap* kuna kifungu maalum cha mafuta kwa ajili ya ununuzi wa mafuta kwa Jeshi la Polisi.

Aidha suala la misaada ya kijamii kwa *Sober Houses* kuwa ni midogo, napenda kueleza kwamba kwa mwaka jana ofisi ilitenga shilingi milioni 15 na hivi sasa imetenga shilingi milioni 19, lakini kwa vile *Sober Houses* zimeongezeka na kuwa nyumba 12 basi mgao utabakia kuwa ni ule ule.

Mhe. Spika, vikao vya tume vimepangwa kufanyika mara mbili kwa mwaka. Kikao cha kwanza cha tume kilifanyika mwezi wa Januari na chengine kinatarajiwa kufanyika mwezi wa Julai mwaka huu.

Mhe. Spika, mapambano dhidi ya dawa za kulevya yanalenga kwenye mambo yote ya usambazaji na matumizi na mafanikio makubwa yanaonekana. Hali hii ni kwa sababu utekelezaji wake unawalenga zaidi watumiaji na ambapo gharama za utekelezaji sio kubwa na wataalamu wa Tume ya Dawa za Kulevya wanajaribu kuwafikia watu katika maeneo mbali mbali kama vile sehemu za kazi, skuli na mikutano ya kijamii, kwa lengo la kutoa elimu inayohusu athari za dawa za kulevya.

Usimamizi wa usambazaji wa dawa za kulevya ni jambo gumu na hasa kwa kuzingatia kwamba utekelezaji wake unahitaji ushirikiano wa dhati wa sekta mbali mbali na gharama zake ni kubwa. Hata hivyo, mpango huu maalum wa *Roadmap* ulioandaliwa na serikali unalenga zaidi kwenye usimamizi wa usambazaji.

Mhe. Spika, watu wanaokamatwa na wakaachiwa ni kutokana na hali halisi, kwamba mtuhumiwa yeyote ili atiwe hatiani ni lazima kukamilike kwa ushahidi na kuwepo vielelezo vya kutosha ambavyo vitairidhisha mahakama. Kwa hivyo, kwa wale wote ambao wamekamatwa na vidhibiti vikakosekana kisheria inabidi waachiwe.

Mhe. Spika, nawaomba sana wananchi watupe ushirikiano wa kutosha katika kuwafichua wale wote wanaojishughulisha na uingizaji na usambazaji wa dawa za kulevya na wala wasiwaonee muhali.

Aidha kuhusu suala la kuwa serikali inawajua wanaoleta dawa za kulevya, lakini labda inashirikiana nao. Mhe. Spika, ofisi yangu haijui mtu yeyote ambaye analeta dawa za kulevya na kama kuna kiongozi yeyote au raia yeyote anayemjua mtu anayeingiza dawa za kulevya, kwa kweli tunaomba sana Mhe. Spika, kwamba ashirikiane na ofisi yetu, ili tuweze kumchukulia hatua.

Kutokana na hali hiyo, zawadi maalum zimetengwa kwa mtu yeyote atakayetoa taarifa sahihi kwa wanaojishughulisha kwa njia moja au nyengine na biashara ya dawa za kulevya. Mhe. Spika, naomba niwahakikishie wale wote watakaotoa taarifa kwamba usiri wa taarifa zao na wao wenyewe unazingatiwa katika hali ya juu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kuhusu suala la uangamizaji wa dawa za kulevya zinapokamatwa ni kwamba hapo awali dawa zinazokamatwa zilikuwa zinaangamizwa na mahakama kwa kushirikiana na Bodi ya Dawa. Sasa mara baada ya marekebisho ya Sheria Nam. 9 imetoa muongozo wa uangamizaji wa dawa za kulevya. Lakini tokea kuanza kazi kwa mabadiliko hayo, hakuna kesi iliyofikia hatua hiyo ya uangamizaji wa vielelezo ambavyo vipo.

Mhe. Rufai Said Rufai ametoa rai kwa nini tusitumie neno kupambana na matumizi na usafirishaji wa dawa za kulevya, baada ya kutumia upunguzaji, usafirishaji au utumiaji.

Mhe. Spika, lengo la tume ni kupambana na hatimaye kuondoa kabisa matumizi na usafirishaji wa dawa za kulevya. Kwa kweli lugha iliyotumika kwenye hotuba ya bajeti ni lugha iliyozoeleka kama inavyotumiwa na Shirika

la Umoja wa Kimataifa linalohusiana na mambo ya *Supply Reduction and Demand Reduction*, lakini lengo kuu ni kuondoa kabisa.

Mhe. Salma Moh'd Ali alitaka kujua vigezo gani vinavyotumika vya ugavi wa fedha kwa *Sober Houses.* Mhe. Spika, wakati tukiandaa bajeti ya Tume mwaka jana jumla ya *Sober Houses* zilikuwa ni 9 tu, ambapo Unguja 7 na Pemba 2, hivyo mgao wa fedha ulikwenda kwa mujibu wa *Sober Houses* zilizopo katika maeneo hayo.

Vile vile katika *Sober Houses* hizo hakukuwa na *Sober House* ya wanawake kwa upande wa Pemba na fedha wanazopewa *Sober* ni kwa ajili ya mahitaji yao ambayo wanawasilisha Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais. Kwa mfano, kodi ya nyumba, chakula au matumizi mengine yoyote, ambapo ofisi yetu inayaridhia.

Mhe. Fatma Mbarouk Said alitaka kujua iwapo elimu ya dawa za kulevya inawafikiwa watu wenye ulemavu. Mhe. Spika, elimu ya dawa za kulevya inatolewa kwa kulenga jamii nzima na kupitia skuli, sehemu za kazi, mikutano ya shehia pamoja na kutumia vyombo tofauti kwa ajili ya kuyafikia makundi yote ndani ya jamii yetu.

Mhe. Panya Ali Abdalla alitaka kujua udhibiti wa dawa za kulevya umekuwa mgumu hawa waletaji wana nguvu kiasi gani. Mhe. Spika, suala la dawa za kulevya ni mategemeo yetu kwamba *Roadmap* inaweza kusaidia kwa kiasi kikubwa udhibiti wa dawa za kulevya katika suala zima la uingizaji na usambazaji, kwani taasisi mbali mbali ambazo zimo katika mapambano ya dawa za kulevya zina ushiriki wao kikamilifu.

Mhe. Spika, kuhusu kuongezeka kwa ruzuku kwa *Sober* ushauri tumeupokea na bajeti itakaporuhusu Mhe. Spika, basi tutafanya hivyo.

Mhe. Mgeni Hassan Juma alitaka kujua kuhusu choo cha uwanja wa ndege. Mhe. Spika, choo cha uwanja wa ndege tayari kimeshakamika na kukabidhiwa kwa vyombo husika na mpaka hivi sasa hakuna mtu yeyote aliyekamatwa kupitia njia ya choo hicho. *(Makofi)*

Ofisi Kuu Pemba. Mhe. Spika, kuhusu suala la bajeti ya ununuzi wa magazeti upo na ninamuomba Mhe. Hija Hassan Hija aangalie kifungu namba 220508 ambacho kina jumla shilingi 720,000/=. Kwa kweli kuna kila umuhimu wa Ofisi ya Pemba kupatiwa huduma ya magazeti kama zilivyo ofisi nyengine za serikali, ili kurahisisha upatikanaji wa taarifa.

Mhe. Spika, tunakubaliana na ushauri wa Mhe. Bikame Yussuf Hamad kwamba tuangalie uwezekano wa kusaidia maeneo yanayoingia maji ya chumvi na kuona ni kwa jinsi gani tutaweza kusaidiana na kukabiliana na suala hili.

Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais inaendelea kuwasiliana na watendaji wenzetu wa Tanzania Bara katika kupata fungu la utekelezaji kupitia Mfuko wa Wananchi Masikini unaotekelezwa kupitia Mkataba wa Kimataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi shilingi milioni 800 zilizoombwa kwa ajili ya mradi zimepangiwa kutekeleza kazi maalum ya kujenga uwezo wa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. Katika hili tunamuomba Mhe. Mjumbe binafsi kushirikiana na watendaji wetu ambao wako Pemba, ili kuona namna tutakavyoweza kupambana na suala hili.

Mhe. Spika, kuhusu bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais Pemba kuwa ndogo. Kwa kweli kimsingi ukiachia masuala ya uratibu wa shughuli za Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais ambazo zinasimamiwa na Ofisi Kuu Pemba ni kwamba kila idara inatekeleza shughuli zake zinazoihusu idara hiyo, kwa upande wa Pemba kupitia bajeti za idara, yaani *core functions* za idara mbali mbali bajeti zimo ndani ya idara nzima na haziko Ofisi Kuu Pemba.

Mhe. Spika, aina na idadi ya visaidizi kwa watu wenye ulemavu vilivyotolewa katika wilaya mbali mbali za Pemba kama nilivyotakiwa na Mhe. Mohammed Mbwana Hamad, Mhe. Spika ninayo hapa lakini nachelea kwa muda nayo naomba nimkabidhi Mheshimiwa maana yake naona *list* ni refu na ingeweza kutuchukulia muda. Lakini labda kwa ufupi nimueleze maeneo mbali mbali watu ambao wamekabidhiwa ni kutoka Msikiti Makuti, Mkungu Malofa, Pongwe, Uondwe, Muweza, Makadara, Maungweni, Kiuyu, Mamoja, Rahaleo na Tibirinzi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, uchambuzi wa matumizi wa vifungu kwa idara ni kama ifuatavyo. Mhe. Spika, naomba sana kuingia katika vifungu ambavyo Waheshimiwa Wajumbe kwa umoja wao wamevihoji vingi vyao na naomba nitoe maelezo hapa na pengine sitomtaja hasa nani aliuliza kifungu gani, lakini naomba mnichukulie kwa hilo kwa sababu wengine watu watatu mpaka wanne wamehoji kifungu kimoja. *(Makofi)*

Ofisi ya Faragha kifungu 220504 linalohusiana na vifaa vya *computer*. Mhe. Spika, kifungu hiki kimejumuisha ununuzi wa vifaa vya *computer* kwa matumizi ya ofisi pamoja na mashine ya uhariri, yaani *editing bench* inaitwa kwa lugha ya kigeni, kwa mwaka uliopita kifungu hichi kilikuwa na shilingi

milioni 3,960,000/= na kwa mwaka huu kinaombewa shilingi milioni 24,370,000/=.

Mhe. Spika, mpaka hivi sasa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais haina *editing bench* na ni suala muhimu sana kuwepo katika ofisi kubwa kama hii, kwa sababu taarifa mbali mbali za Mhe. Makamu wa Kwanza hazitakiwi zitoke nje kabla hazijawa *edited*. Kwa hivyo, ongezeko hili ni kwa ajili ya ununuzi wa mashine ya uhariri katika ofisi hii ili kuweza kutoa taarifa hizo.

Idara ya Mipango, Sera na Utafiti, Mhe. Spika kutokana na vipaumbele vya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kupitia idara hii, mpango mkakati, mpango mkuu wa utafiti na muongozo wa mambo mtambuka unatarajiwa kutekelezwa. Mafunzo kadhaa yakiwemo ya mbinu za utafutaji rasilimali, UKIMWI katika sehemu za kazi, utekelezaji wa mambo mtambuka na kadhalika yanatarajiwa kuendeshwa kwa watendaji wa ofisi yetu na sekta nyengine.

Mhe. Spika, Wajumbe wengi walitaka ufafanuzi wa vifungu vilivyopo katika idara hii na naomba nianze kutoa ufafanuzi huo kama ifuatavyo.

Kifungu 220301 kuhusu safari za ndani, fungu hili limeongezeka kwa shilingi milioni 7,680,000/=. Hali hii ni kutokana na idadi ya mwaka uliopita kwa sababu mbali na safari za kawaida kutakuwa na mafunzo mengi ambayo watendaji kutoka Pemba watahudhuria. Aidha kazi za ufuatiliaji na tathmini zinatarajiwa kuanza mwaka huu hasa kwa kuzingatia kwamba mtaalamu wa fani hiyo tayari ameajiriwa.

Kifungu 220401 gharama za petroli, gharama za matumizi ya mafuta zimepangwa kutokana na hali halisi ya matumizi hayo kwa kipindi cha mwaka 2012/2013.

Kifungu 2205017 utayarishaji wa mpango wa bajeti, gharama za fungu hili zimeshuka kwa sababu mwaka jana fungu hili lilikusanya kazi zote kuu za idara, lakini mwaka huu fungu hili limeshuka kwa sababu utekelezaji wa shughuli kuu za idara zimetolewa na kuelekeza katika maeneo mengine ya idara, fedha zilizobaki katika fungu hili ni kwa ajili ya matayarisho kwa mpango wa bajeti pekee.

Kifungu 211116 posho la vikao na kamati. Kifungu hichi kimekusanya fedha za kutumika kwa ajili ya kuwalipa washiriki wakati wa utekelezaji wa kazi zifuatazo:-

1. Kuandaa Sera ya Watu Wenye Ulemavu,

2. Kufanya Mafunzo ya Ukufunzi kwa Mambo Mtambuka,
3. Kusaidia Mafunzo ya Mambo Mtambuka kwa Sekta za Serikali,
4. Kuandaa Mafunzo ya Utafutaji Rasilimali na Mafunzo ya Utafiti na Uchambuzi wa Taarifa.

Mhe. Spika, katika kutekeleza kazi zote hizo jumla ya shilingi milioni 17,400,000 zimepangwa kutumika.

Kifungu 220201 chakula na vivyaji, kifungu hichi nacho kimepangwa kutumika kwa ajili ya kuwapatia chakula na vivywaji washiriki wakati wa kutekeleza shughuli zifuatazo:-

i) Mapitio ya *Medium Term Expenditure Framework (MTEF),*
ii) Utayarishaji wa *MTEF,*
iii) Kutayarisha hotuba ya bajeti,
iv) Kutayarisha Sera ya Watu Wenye Ulemavu,
v) Mafunzo ya *TOT* watu 50 kutoka wizara zote za Unguja na Pemba,
vi) Kusaidia kuendesha mafunzo ya mambo mtambuka,
vii) Mafunzo ya Ukufunzi wa *HIV,*
viii) Uhamasishaji juu ya *HIV,*
ix) Mafunzo ya Utafutaji wa Rasilimali.

Mhe. Spika, jumla ya shilingi milioni 31,353,500/= zimepangwa kutumika.

Kifungu 220509 hii ni ada ya ushauri. Mhe. Spika, ni dhahiri kwamba kuna baadhi ya kazi zinahitaji uweledi wa hali ya juu. Katika kutekeleza hili ofisi yetu inatarajia kuajiri washauri elekezi kwa kusaidia utekelezaji wa shughuli zifuatazo:-

a) Kuandaa Sera ya Watu Wenye Ulemavu,
b) Mafunzo ya Ukufunzi wa UKIMWI,
c) Kusaidia Mafunzo ya Mambo Mtambuka,
d) Mafunzo ya Wakufunzi wa Mambo Mtambuka,
e) Mafunzo ya Utafutaji wa Rasilimali,
f) Kufanya tafiti mbili katika maeneo ya ofisi yetu,
g) Mafunzo ya Utafiti na Uchambuzi wa Taarifa

Mhe. Spika, matarajio ni kwamba washauri watakaotumika katika kazi hizi wataelekeza vizuri ofisi yetu katika kufikia malengo waliyokusudia na jumla ya kifungu hichi ni shilingi milioi 29,300,000/=.

Kifungu 211108 malipo ya kujikimu na malazi. Mhe. Spika, kifungu hichi kimepungua kwa sababu mwaka jana kifungu hichi kilikusanya maposho ya

kujikimu kwa safari za kikazi ambazo mwaka huu posho ya kujikimu kwa safari imewekwa moja kwa moja katika fungu la safari.

Idara ya Utumishi na Uendeshaji. Katika idara hii Mhe. Ismail Jussa Ladhu alitaka kujua tarakimu sahihi kati ya zilizojitokeza kwenye kitabu kikubwa cha makisio, katika kiambatanisho cha Nam. 11 na ndani ya hotuba yangu mwenyewe.

Mhe. Spika, tarakimu halisi kulingana na mahitaji au matakwa ya kuidhinishwa ni kama inavyojionesha ndani ya kitabu kikubwa cha makisio pamoja na kiambatanisho cha hotuba iliyosomwa ambayo ni shilingi bilioni 1,329,827,000/= iliyojumuisha shilingi bilioni 1,037,000,000/= kwa ajili ya mishahara na shilingi milioni 292,827,000/= na tarakimu zilizomo ndani ya hotuba hazikuwa sahihi kutokana na makosa ya kibinadamu ya wachapaji wa hotuba hiyo. Mhe. Spika, naomba radhi kwa hilo.

Mhe. Spika, ufafanuzi wa vifungu ni kama ifuatavyo:-

Idara ya Utumishi na Uendeshaji kifungu 220508 suala la magazeti tofauti iliyojitokeza kwa mahitaji ya fungu husika imesababishwa na mambo yafuatayo. Uhaba wa bajeti kulingana na kikomo kilichopatiwa ambacho kimepelekea uchambuzi yakinifu, kuwa vipaumbele vya ndani ya Idara ya Utumishi na Uendeshaji hasa kwa kuzingatia majukumu ya idara husika.

Kufuatilia ukuaji wa teknolojia ya habari, idara ina lengo la kushajihisha zaidi matumizi ya mtandao katika kupata habari na hii itakwenda sambamba na uanzishwaji na uwekaji wa *LAN* ndani ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais pamoja na uboreshaji wa matumizi ya mtandao kwa wafanyakazi.

Kifungu 220108 huduma za mtandao. Mhe. Spika, ongezeko linaloonekana linatokana na uboreshaji wa huduma husika kutokana na matumizi ya gharama za kila mwezi ambazo kwa sasa ni shilingi 450,000/= na matarajio kwa mwezi ni shilingi milioni 1,000,000/= kutokana na ubadilishaji wa *package* na hata *domain* zinazotumika katika mwaka wa fedha ujao. Hali hii ni kusema kuwa zitumikazo kwa sasa hazitoshi kulingana na ukuaji wa matumizi husika.

Kifungu 220401 gharama za petroli, ongezeko hili limetokana na ukuaji wa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kiutendaji na kumepelekea hata kukua kwa kazi za kila siku zinazofanywa na maafisa wakitumia vipando vya ofisi. Kwa kipindi cha mwaka wa fedha ujao matarajio kwa mwezi ni jumla ya lita 350 pamoja na mazingatio ya mabadiliko ya bei kwa gharama husika.

Kifungu 220402 gharama za *diesel*, ongezeko kwa kifungu husika ni kutokana na gharama za matumizi kwa vipando pamoja na kinu cha umeme, yaani jenereta kwa matumizi ya ofisi, ambayo yamepelekea kuongezeka kwa watumiaji husika. Mhe. Spika, makadirio ya mwaka ujao wa fedha kwa kila mwezi tunaweza kutumia lita 600 pamoja na mazingatio ya bei.

Kifungu 220504 vifaa vya *computer*. Mhe. Spika, kifungu hichi kinaonesha mabadiliko kutokana na ununuzi wa vifaa pamoja na *server* kwa ajili ya *LAN* ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais. Gharama za uwekaji mfumo husika mpaka kufikia kiwango kwa ajili ya matumizi.

Kifungu 220504 vifaa vidogo vidogo kifungu hiki kimeongezeka kutokana na ununuzi wa vifaa vidogo vidogo unaojitokeza mara kwa mara kutokana na kazi za kila siku kulingana na makisio ya sasa kwa kila robo mwaka hutumika jumla ya shilingi 100,000/=.

Imprest kwa ajili ya safari za kikazi zinazofanywa na maafisa katika uratibu wa ufuatiliaji wa kazi za kiutumishi na kiutendaji, matarajio kila baada ya miezi miwili ni jumla ya shilingi 500,000/=.

Mhe. Spika, *imprest* kwa mafunzo ya ndani ya kazi (*on job training*) kwa wafanyakazi pamoja na kulipia kupitia vifungu husika kwa mwaka wa fedha ujao mafunzo mbali mbali ya muda mfupi yatafanyika kwa wafanyakazi wote yakiwemo Sheria za Utumishi, Mafunzo ya kazi husika kama vile uhudumu, ziara za kimafunzo na hata mikutano ya wafanyakazi.

Katika kuimarisha ufanisi kazini matarajio ni kuweza kutumia shilingi 260,000/= kwa kila mwezi.

Kifungu 211110 posho maalum. Mhe. Spika, kifungu hichi hutumika sambamba na kifungu cha mishahara na ni kile chenye mchanganuo wa Mfuko wa Hifadhi kwa mwezi na hujumuisha mambo yafuatayo.

Posho la mafuta kwa viongozi wateule. Mhe. Spika, katika nyaraka hii ninayoisoma thamani yenyewe imeelezwa hapa, lakini naomba kwa sasa nitaje tu yale ambayo yanatengeneza kifungu hichi.

- Posho nyeti kwa watendaji,
- Posho kwa katibu muhtasi watendaji,
- Posho la dereva watendaji,
- Posho la matarishi kama ni watendaji,
- Posho la Ujumbe wa Baraza la Wawakilishi viongozi wateule,
- Posho la umeme kwa viongozi wateule,

- Posho la watumishi kwa viongozi wateule,
- Posho la takrima kwa viongozi wateule,
- Posho la simu kwa viongozi wateule,
- Posho la nyumba kwa viongozi wateule,
- Posho la masjala kwa watendaji,
- Posho maalum kwa watendaji,
- Posho la watendaji wa sheria na
- Posho la wahudumu.

Mhe. Spika, kiwango kwa mwezi ni shilingi milioni 30,374,000/= na kiwango kwa mwaka ni shilingi milioni 364,488,000/=.

Kifungu 211104 malipo ya likizo. Mhe. Spika, kifungu hichi kimeonekana kupungua kwa sababu haya ni makisio halisi kwa wafanyakazi watakaolipwa, ambapo wafanyakazi wanaokwenda likizo hawalipwi kila mwaka kwa likizo.

Kifungu 211107 malipo baada ya saa za kazi. Mhe. Spika, kifungu hichi kimewekwa kutokana na hali halisi ya mahitaji ya matumizi husika.

Kifungu 211108 malipo ya kujikimu na malazi. Mhe. Spika, malipo ya kifungu hichi yaliyopita yalikuwa yakilipwa kupitia mradi wa *SMOLE* na kwa mwaka huu huduma hiyo haipatikani tena kupitia mradi huo na idara italazimika kutumia kifungu hichi kwa fedha za serikali.

Aidha idara hupokea mchango mkubwa wa zawadi kwa ajili ya Sherehe ya Siku ya Mazingira kupitia mradi wa *SMOLE*, ambapo kwa mwaka huu kifungu cha zawadi 220202 kimetengewa fedha za serikali.

Mhe. Spika, kifungu 220301 safari za ndani kifungu hichi kimeongezeka kutokana na kuongezeka kwa safari za ufuatiliaji.

Kifungu 220401 gharama za petroli, makisio ya matumizi ya kifungu hichi yamepungua kutokana na hali halisi ya mahitaji.

Kifungu 220402 gharama za *diesel*. Mhe. Spika, hali halisi kwa mwaka ni kutokana na kuwa na vyombo vingi vinavyotumia mafuta ya *diesel* kuliko petroli na pia kuongezeka kwa shughuli za *Operation* za Kanuni za Maliasili Zisizorejesheka.

Kifungu 220806 gharama za bima na leseni. Mhe. Spika, hii ni kufuatia agizo la serikali la kuvikatia bima vipando na idara imepanga kutelekeza agizo hili kwa mwaka huu wa fedha.

Idara ya Watu Wenye Ulemavu. Mhe. Spika, hapa Mhe. Ismail Jussa Ladhu alitaka ufafanuzi juu ya maposho mbali mbali katika Idara ya Watu Wenye Ulemavu. Kwa hivyo, napenda kumjibu kwamba maposho yaliomo katika idara hii ni posho kwa ajili ya vikao vya Baraza la Watu Wenye Ulemavu, pia posho la vikao vya Maafisa Waratibu wa Masuala ya Watu Wenye Ulemavu. Aidha idara kwa kila mwaka huhudhuria mkutano mmoja wa kimataifa wa Watu Wenye Ulemavu huko New York Marekani kila ifikapo Septemba ya kila mwaka.

Tume ya Uratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya kifungu 311202 ununuzi wa gari. Mhe. Spika, mwaka jana fedha za ununuzi wa gari hazikupatikana, lakini mahitaji bado yapo na hivyo bei mpya imewekwa.

Ofisi Kuu Pemba kifungu 211108 malipo ya kujikimu na malazi na kifungu hichi kinajumuisha gharama za kuwalipia watendaji wa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais Pemba wanaosafiri kushiriki katika mikutano kama ifuatavyo.

- Mhe. Spika, hawa wanakuja Unguja kushiriki katika vikao vya Kamati hizi za Baraza, ikiwemo *PAC*,
- Kushiriki katika vikao vinne vya kuwasilisha utekelezaji kwa Mhe. Rais (Bango Kitita),
- Kushiriki vikao viwili vya matayarisho *nominal role*,
- Kushiriki vikao vinne vya Kamati ya Uongozi ya Ofisi,
- Kufuatilia marekebisho ya mishahara na maslahi mbali mbali ya wafanyakazi kadri hali inaporuhusu,
- Kushiriki katika kikao cha bajeti kila mwaka.

Hata hivyo, malipo haya ya kujikimu ni kwa ajili ya kuwahudumia maafisa wanne kwa siku tatu tu kwa mwezi kati ya safari saba za Wakuu wa Maidara wanaohitajika kusafiri kwa shughuli mbali mbali za kikazi ukiachilia mbali watendaji wengine wa maidara ambao kutokana na ufinyu wa bajeti hawakuweza kupangiwa huduma hii.

Kifungu 220404 gharama za vilainishi ni *oil* na *break fluid* na ununuzi wa vichujio *oil filter diesel or petrol filters*. Mhe. Spika, kwa kawaida vinanunuliwa na taasisi husika na fundi wa kuhudumia *service* analipwa gharama ya ufundi wake.

Kifungu 311202 ununuzi wa gari. Mwaka jana fedha halisi za ununuzi gari hazikupatikana na mahitaji bado yapo. Hata hivyo, bei ya ununuzi nayo imepanda.

Kifungu 220504 vifaa vya *computer*. Mhe. Spika, kifungu cha ununuzi wa vifaa vya *computer* imeongezeka mwaka huu kutokana na kuongezeka idadi ya *computer* kutoka nne hadi nane, pia kuongezeka kwa idadi ya *printer* kutoka tatu hadi saba na kuongezeka kwa *photocopy machine*.

Kifungu 211208 malipo ya huduma ya ulinzi. Mhe. Spika, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais haina mlinzi wa kuajiriwa, kwa hiyo kifungu hichi ni kwa ajili ya kutoa huduma za ulinzi kutoka Kampuni ya Ulinzi zinazotambulika.

Mhe. Spika, naomba sasa nijibu masuali yanayohusiana na Tume ya UKIMWI. Mhe. Spika, naomba kwanza kuwashukuru Wajumbe wote wa Baraza lako tukufu na kama itatokea bahati mbaya kutomtaja Mjumbe yeyote ambaye amechangia katika fungu hili naomba radhi sana. *(Makofi)*

Kwa hivyo, naomba kuwataja kwa majina ambao wamechangia katika sehemu hii ni:

1. Mhe. Ismail Jussa Ladhu
2. Mhe. Hija Hassan Hija
3. Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohamedali
4. Mhe. Bikame Yussuf Hamad
5. Mhe. Mohammed Mbwana Hamad
6. Mhe. Salim Abdalla Hamad

Mhe. Spika, na wengine ambao kwa bahati mbaya sana hapa nitakuwa nimeacha kuwataja. *(Makofi)*

Mhe. Spika,Waheshimiwa Wajumbe hao walitoa michango yao katika maeneo yafuatayo. Tume ya UKIMWI hutumia mabilioni ya fedha kwa mikutano na makongamano bila ya kuwafikia walengwa. Lakini Tume ya UKIMWI hutumia fedha katika maeneo yasiyo na tija, fedha zinapelekwa siko na wala hakuna matokeo, UKIMWI unaongezeka na huyo alikuwa ni Mhe. Ismail Jussa Ladhu, Mhe. Bikame Yussuf Hamad na Mhe. Hija Hassan Hija. *(Makofi)*

Vile vile Mhe. Hija Hassan Hija alielezea kwamba fedha za UKIMWI nazo ziweze kuhaulishwa na zipelekwe katika mafungu mengine. Gonjwa la UKIMWI ni hatari sana linapoteza nguvu kazi ya taifa, mikakati madhubuti iwekwe Mhe. Mohammed Mbwana Hamad alituasa sana juu ya suala hili.

Mhe. Spika, ili kupambana vyema na UKIMWI masuala ya maadili, silka na utamaduni haya yalipewa nafasi kubwa katika mazungumzo ya Mhe. Salim Abdalla Hamad na Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohamedali.

Mhe. Spika, naomba uniruhusu kuwajibu Waheshimiwa Wajumbe kama ifuatavyo. Kwanza kuhusiana na majukumu ya Tume. Tume ya UKIMWI imeundwa kupitia Sheria Nam. 3 ya mwaka 2002, ambayo ilipitishwa na Baraza lako hili tukufu. Majukumu ya Tume ya UKIMWI yametajwa katika sheria hiyo, ambayo kwa ufupi sana ni haya yafuatayo:-

1. Kuratibu shughuli zote za mapambano ya UKIMWI kitaifa,
2. Kutafuta na kusimamia fedha kwa ajili ya mapambano dhidi ya UKIMWI,
3. Kuwajengea uwezo wadau katika kukabiliana na changamoto za mapambano hayo,
4. Kuandaa miongozo, sera na mikakati ya kitaifa katika kukabiliana na mapambano ya UKIMWI,
5. Kuandaa mfumo wa ufuatiliaji, tathmini na utafiti katika shughuli za mapambano dhidi ya UKIMWI,
6. Kuwaratibu wadau wote wanaojihusisha na mapambano dhidi ya UKIMWI.

Mhe. Spika, napenda kukuarifu kwamba Tume ya UKIMWI imekuwa ikiyatekeleza vizuri majukumu hayo niliyoyataja.

Mhe. Spika, kuhusu hoja kwamba fedha za mapambano haziwafikii walengwa na hazina tija. Kwa kweli kuhusiana na hili, naomba tuuangalie UKIMWI katika sura ya shilingi, yaani UKIMWI kama shilingi una sura mbili Mhe. Spika.

Sura ya kwanza ni idadi ya watu ambao tayari wameshaambukizwa na wanaishi na virusi vya UKIMWI hawa ni asilimia 1 kwa sasa katika jamii yetu. Sura ya pili ni idadi ya watu ambao hawana virusi ni asilimia 99 na hawa nao wanatakiwa walindwe, ili wasitumbukie katika janga hilo.

Mhe. Spika, kupanga ni kuchagua je, tuzichukue fedha zote za mapambano dhidi ya UKIMWI tuzitie kwenye asilimia 1 kwa kutegemea asilimia 99 iliyobaki itajilinda wenyewe bila ya hatua zozote.

Mhe. Spika, tunaelewa kuwa jamii inaeleweshwa vya kutosha katika kipindi chote cha mapambano, na tunajua kuwa uelewa kuhusu UKIMWI uko juu ndani ya jamii yetu. Lakini pamoja na juhudi zote hizo za kujenga uelewa huo mkubwa, naomba sana Mhe. Spika tujiulize je, ni kwa nini bado kuna ugumu

wa watu kubadili tabia zao? Kwa nini bado tunashuhudia maambukizi mapya?

Mhe. Spika, suala la UKIMWI ni zaidi ya fedha na ni suala si la kuiachia Tume UKIMWI peke yake, isipokuwa ni suala la kila mmoja wetu katika nchi hii. Lakini kubwa zaidi ni suala la kila mmoja wetu kubadilika kitabia na kimtazamo, tukiendelea kumuona anayeishi na virusi vya UKIMWI pekee ambayo ni asilimia moja afanywe ndiye mlengwa pekee na tukaiacha sehemu kubwa ya jamii ambayo ni asilimia 99 mtazamo huu hautatusaidia sana Mhe. Spika. *(Makofi)*

Kwa kweli mkakati huu unaotumika kwa asilimia 99 ni kuelimisha. Sasa katika hali hiyo mikutano na makongamano hayakwepeki, tunapokea mchango juu ya njia bora zaidi ya kuielimisha jamii.

Mhe. Spika, kuhusu ongezeko la asilimia 0.4 la maambukizi ya virusi yaliyotolewa na utafiti wa hivi karibu wa Maleria na Ukimwi nchini Tanzania. Napenda kusema kuwa ni kweli utafiti umeonyesha kuwa ongezeko kwa upande wa Zanzibar kutoka asilimia 0.6 hadi kufikia asilimia 1.

Mhe. Spika, napenda kutoa tahadhari katika kuzitafsiri takwimu hizo. Ni kweli kuwa kuna hoja nyingi zimejitokeza tangu kutolewa kwa takwimu hizo na kila mmoja anatafsiri aonavyo yeye. Ipo haja ya kufuatilia zaidi kwa wahusika ili kupata tafsiri iliyo sahihi. Mhe. Spika, hakuna ubishi kuwa maambukizi mapya bado yapo lakini suala je, kiwango cha maambukizo hayo kimeongezeka kiasi gani, nadhani hilo ndio suala la kujiuliza.

Mhe. Spika, napenda hapa kutoa takwimu za maambukizo kwa wanaopima kuanzia mwaka 1986 ambapo kesi tatu za mwanzo katika hospitali ya Mnazi Mmoja ziliripotiwa, hii ni *document* ambayo inaonesha watu waliopima ukimwi kwa kila mwaka na asilimia ya watu ambao wamegundulikana na ukimwi, lakini nayo ni *document* ambayo ni refu lakini kwa ufupi inaonesha wale wanaopimwa na wale wenye Ukimwi takwimu inashuka.

Aidha takwimu hizi zinaonesha kuwa kiwango cha maambukizi hasa katika miaka kumi ya mwisho kinashuka ukiangalia asilimia waliogundulikana na Ukimwi. Hali hii inaonesha kuwepo tija juu ya juhudi zinazochukuliwa.

Mhe. Spika, kama nilivyosema hapo kabla takwimu zilizotolewa za Malaria na Ukimwi za hivi karibuni zinahitaji kufuatiliwa zaidi na Wizara yetu kupitia Tume ya Ukimwi, itashirikiana na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu na wataalamu wa Wizara ya Afya kupata tafsiri sahihi ya hali hiyo. Nawaomba

Waheshimiwa wa Baraza wawe na subra hadi hapo wataalamu wetu watakapokuja kututafsiria usahihi wa takwimu hizi.

Fedha za Ukimwi zihalalishwe zipelekwe katika mafungu mengine. Mhe. Spika, kama nilivyosema kwamba Tume ya Ukimwi imeundwa kisheria na majukumu yake yameainishwa. Kama Wajumbe wa Baraza lako Tukufu Mhe. Spika, wanahisi sasa Tume hiyo haihitajiki, nadhani wanayo haki ya kuishauri serikali, sisi bado kama ofisi tunahisi tume hii inahitajika na tunathamini sana kazi wanayoifanya.

Wizara inatoa tahadhari kuwa hakutokuwa na mikakati madhubuti kwa hiyo asilimia 99 ya jamii ambayo ipo salama, hasa kama Tume haitokuwepo tutakaribisha hali ya hatari zaidi na mafanikio yaliyofikiwa yatatuponyoka na kuingia katika ile hali ya nchi zilizo Kusini mwa Bara la Afrika. Hata hivyo fedha hizi ni za wafadhili ambazo wametenga maalum kwa mapambano dhidi ya Ukimwi, ulimwengu mzima umekuwa ukipiga kelele kwamba fedha za mapambano zinapungua kila uchao, tunaiona hali ni tofauti.

Mhe. Spika, tunakubaliana na hoja za Mhe. Mohammedraza Hassanali, Mhe. Mohammed Mbwana na Mhe. Salum Abdalla, kwa mikakati maalum kwa ajili ya kuangalia makundi maalum silka, maadili na utamaduni pamoja na namna ya kuzishirikisha taasisi za dini katika mapambano ya virusi vya Ukimwi. Hali hiyo imezingatiwa vizuri katika mkakati wetu wa pili wa mapambano dhidi ya Ukimwi, ambao umeanza utekelezaji wake mwaka 2011/2012, hivi sasa tupo kati kati ya utekelezaji wa mkakati huo na tunatarajia kufanya tathmini hivi karibuni.

Mhe. Spika, wachangiaji wa leo hii, mchangio wa Ukimwi ulifanywa siku mbili, leo tumempata na Mhe. Rufai Said Rufai, Mhe. Fatma Said, Mhe. Panya Ali Abdalla, Mhe. Mgeni Hassan Juma na Mhe. Abdalla Juma.

Mhe. Rufai alisema kwamba tume ya Ukimwi haitekelezi majukumu yake ipasavyo zaidi wafanyakazi wanaangalia kujinufuisha wenyewe. Mhe. Spika, napenda kuwahakikishia Wajumbe kuwa Tume ya Ukimwi inajitahidi kutekeleza wajibu wake kama ilivyoainishwa katika majukumu yaliyomo katika sheria Nam.3 ya mwaka 2002 ambayo nimeitaja kabla.

Kuhusu suala la fedha kutumika katika ngazi za mawizara tu sio sahihi. Shughuli nyingi pia zinafanyika katika ngazi za shehia ndani ya wilaya zote za Unguja na Pemba kupitia mradi maalum wa kujenga uwezo. Ningewaomba sana Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu wakafuatilia katika majimbo yao ili kuona kwamba shehia zao zinafikiwa kupitia mradi huu.

Mhe. Spika, nakubaliana sana na Mhe. Fatma Said aliyetaka kufanyiwa juhudi zaidi katika kuibua sababu zinazopelekea tatizo la Ukimwi kuendelea kuwepo katika jamii. Tunauchukua ushauri huo kwa kuufanyia kazi. Aidha tunakubaliana na Mhe. Panya kwamba Ukimwi hautoondoka kwa nyimbo wala semina, makongamano na mikutano mingi. Ila kwa kufuata maadili, silka na tamaduni zetu na kuzuia matamanio ya nafsi.

Mhe. Spika, kulijitokeza suala zima la fedha ambazo zilionekana katika Fungu la Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais linalohusiana na Kamati ya kuratibu miradi ya *Global Fund* Zanzibar. Hii ni kamati ya taifa ambayo ina jukumu la kuratibu na kusimamia miradi inayofadhiliwa na mfuko wa *Global Fund*. Kamati hii imeundwa kwa matakwa ya Shirika hilo la *Global Fund* na ipo nchi zote zinazopata msaada wa shirika hilo.

Hapa Zanzibar Kamati hiyo ipo chini ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Kamati hii inaratibu sio Ukimwi peke yake lakini pia inaratibu Malaria na inaratibu magonjwa ya TB. Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati wanaotoka kwenye taasisi za serikali, sekta zisizo za serikali na wadau wa maendeleo. Tume ya Ukimwi, Malaria na TB ni Wajumbe waalikwa kama *Principal CPMs* wa misaada hiyo.

Marekebisho ya vifungu vya kuhaulisha kutoka Tume ya Ukimwi, kama ilivyojitokeza katika hoja nyingi zilizotolewa na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza wakati wa kuichangia hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Tume ya Ukimwi imeridhia kuhaulisha jumla ya shilingi milioni sabini na moja laki nane na tisini kwenda kwenye fungu la Idara ya Dawa za Kulevya kama ilivyoshauriwa na Wajumbe wa Baraza lako Tukufu hata kwamba hatua hiyo itaathiri utekelezaji wa shughuli muhimu za Ukimwi.

Mhe. Spika, baada ya kuyasema hayo naomba nikushukuru sana na niwashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe kwa kuwa wavumilivu wakati wote nikitoa maelezo, kwa kweli Mhe. Spika, kwa wale ambao nitakuwa labda sikuwagusa katika michango yao sio nia yangu wala si nia ya Ofisi yangu, tumepokea michango yote. Naomba sana Waheshimiwa Wajumbe nyote kwa umoja wetu muiunge mkono hotuba hii. Mimi mwenyewe naiunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia. Imani yangu kwamba nanyi mtaiunga mkono.

Mha. Spika, baada ya hayo naomba kutoa hoja.

)

Mhe. Spika: Sasa niwahoji Waheshimiwa Wajumbe wale wanaokubaliana na hoja hii ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa Mwaka 2023/2014 wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Mhe. Spika, kwa kuwa Baraza limejadili na kuikubali hotuba ya bajeti ya Ofisi yangu ya Makamu wa Kwanza wa Rais, sasa naliomba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Matumizi ili iweze kuvipitisha vifungu vya matumizi vya ofisi yangu.

KAMATI YA MATUMIZI

FUNGU 6 - OFISI YA MAKAMU WA KWANZA WA RAIS

Kifungu 0901 Idara ya Mazingira **10,500,000**

FUNGU 6 - OFISI YA MAKAMU WA KWANZA WA RAIS

Kifungu 0301 Ofisi Kuu Pemba

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Bismillahi Rahmani Rahim. Mhe. Mwenyekiti, kabla sijauliza ninalotaka kuliuliza naomba kwa sababu mimi ni wa mwanzo kusimama, kwanza namshukuru na kumpongeza Mhe. Waziri na watendaji wake wote kwa ufafanuzi wake wa kina. Kwa kiasi kikubwa nadhani hoja zetu nyingi umezitosheleza.

Baada ya pongezi hizo katika fungu hili nilikuwa nataka kupata maelezo, Mhe. Waziri akitujibu vizuri na si peke yake na serikali kwa ujumla wake itatuepushia maswali mengi sio kwa Ofisi Kuu tu Pemba kwa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais lakini hata kwenye Idara nyengine zote za Ofisi hii, pia hata Wizara nyengine zinazokuja. Hili Mhe. Mwenyekiti ni suala linalohusu posho maalum, *vote* 211100 ambapo *vote* ndogo ni 211110 Posho maalum.

Mhe. Mwenyekiti, katika fungu hili kuna 19 milioni na laki sita, katika maelezo yake katwambia kwamba fungu la posho maalum huwajumuisha viongozi wateule na zile posho mbali mbali ambazo zinakwenda sambamba na mishahara. Mimi nilikuwa naomba anisaidie kwa upande wa Ofisi Kuu

Pemba kwa hatua hii naomba anisaidie hili. Hawa viongozi wateule wanaostahiki kupata posho maalum ni wangapi na ni wepi, ili niridhike kwamba fungu hili ni sahihi kwa yale maelezo ambayo kuwa ametupa katika ufafanuzi wake. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Ahsante sana Mhe. Spika, naomba kutoa maelezo ya kifungu hiki kama nilivyotakiwa na Mhe. Ismail Jussa Ladhu kama ifuatavyo.

Katika fungu hili la 211110 Kiongozi ambaye ni Mteuliwa wa Rais anayepata posho maalum hapa ni Afisa Mdhamini katika Ofisi Kuu iliyoko Pemba ya Makamu wa Kwanza wa Rais. Lakini vile vile niliwaeleza awali kwamba posho hii sio tu kwa ajili ya wateuliwa lakini inawahusu, madereva, Katibu Muhtasi ambaye atakuwa anafanya kazi pamoja na Afisa Mdhamini huyo lakini pia watu wa Masjala na Wahudumu.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa Unguja hasa kwa ngazi labda Mawaziri na Makatibu Wakuu naweza kukuelewa, lakini nilikuwa naomba unisaidie kwa Ofisa Mdhamini na kwa hawa wasaidizi aliowataja, najua Afisa Mdhamini anaweza akawa dereva, akawa Katibu Muhtasi, lakini hawa wahudumu ni wahudumu wepi ambao wanaingia katika fungu hili.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Mhe. Spika, naomba arejee tena sikufahamu vizuri.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, hili sio lazima anijibu Waziri huyu kwa sababu serikali inawajibika kwa pamoja na linawahusu watu wote. Kwamba kwa upande wa Pemba katika hii orodha ambayo imetajwa kwamba ni wasaidizi ikiwajumuisha amesema madereva, Katibu Muhtasi, watu wa masjala, lakini vile vile ametaja na wahudumu.

Sasa nilitaka kusaidiwa kwamba kwa upande wa Ofisa Mdhamini Pemba dereva naweza kuamini na kufahamu kwamba anatakiwa naye bila ya shaka atakuwa ni mtu wa masjala, bila shaka anaweza kuwa Katibu Muhtasi. Lakini nilikuwa nataka kujua kwa upande wa wahudumu kwa upande wa Ofisi Kuu Pemba kwa suala la Afisa Mdhamini ni kiasi gani wanapata wahudumu hawa katika *category* yake hiyo. Bila shaka pia itakuwa inawahusu na Wakurugenzi wakati ukifika nitaomba maelezo vile vile katika hilo. Hili Mhe. Mwenyekiti naliuliza kwa sababu moja tu. Nadhani kama nilivyosema kwamba tukisaidiwa maelezo mapema yanatupunguzia muda vile.

Hili Mhe. Mwenyekiti, linakuja kwa sababu narudia pale pale kwamba serikali itimize ahadi zake kwetu. Juzi tulivyokuwa tukipitisha vifungu vya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, tulipitisha kwa ahadi kwamba tutaletewa *break down* ya posho maalum ili ituongoze kwa pale tuliridhia shingo upande. Lakini kwa masharti kwamba tutaletewa, sasa kama hatukuletewa. Jana nilipokuwa nikichangia Mhe. Waziri atakumbuka, nikakumbusha tena kwamba hili tunaliuliza litakuja kutupa tabu kwa sababu ahadi mnazotupa hamtutekelezei. Sasa Mhe. Mwenyekiti, tuone hili la juzi kwa leo hamjaletewa, seuze mnapokaa mwaka mzima, maagizo yanayotolewa katika Baraza hili yakawa hayatekelezwi.

Kwa hivyo nilikuwa nasema hebu watusaidie *proper* katika utawala wa serikali hili posho maalum hasa hatulijui, ili turidhike kwamba kuna mafungu haya na huko tunakoendelea kwamba kutakuwa na wizara nyengine. Kwa hiyo naomba anisaidie suala langu kuhusiana na Ofisi Kuu Pemba natoa maelezo hayo kwa sababu nataka ituongoze na kutakapobakia kote ni nani hawa wahudumu ambao Afisa Mdhamini Pemba anao hasa kwa upande wa wahudumu. Kwa sababu Katibu Muhtasi, dereva, masjala naelewa hawa wote, lakini hawa wahudumu ambao wanapata posho maalum kwa upande wa Afisa Mdhamini Pemba naomba anisaidie.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, namshukuru sana Mhe. Ismail Jussa kwa swali lake la kutaka serikali kwa jumla lakini kupitia kifungu ambacho amekitaja kutoa ufafanuzi wa posho maalum ni watu wa aina gani wanaolipwa posho la aina hii.

Ni kweli kama alivyokwishasema Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwamba posho hili linamuhusu Afisa Mdhamini mwenyewe, Katibu Muhtasi wake, Makarani wa Masjala na wahudumu wa Makamu wa Kwanza wa Rais wale waliokuwepo Pemba.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, naomba nisaidie mimi si mzoefu wa Utawala wa serikali lakini kwa ninachokiona kwa upande wa huduma ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa Pemba mara nyingi naona ni wale wale ambao wanatoka Unguja anasafiri nao, dereva huona ni wale wale, wahudumu wa nyumbani naona ni wale wale, Makatibu wake ni wale wale. Sasa hebu nisaidie hao waliokuwepo Pemba ni wepi.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti ni kweli Kiongozi wa kitaifa yoyote yule anaposafiri ana wahudumu wa namna mbili. Ana wahudumu ambao wale ni *parmanent* ambao hao wapo mpaka nyumbani kwake, kwenye makaazi yake na hao ndio

wanakuwa wahudumu wa *parmanent* na anaposafiri nje miongoni mwao husafiri nao ama mmoja au wawili. Lakini katika kila makaazi yake kiongozi wa kitaifa anakuwa na wahudumu wa kudumu kwa ajili ya kushughulika na huduma za kwenye yale makaazi ambayo yapo katika eneo lile.

Kwa hiyo hawa wahudumu ambao nimewasema hapa ni wale wahuduma ambao wapo Pemba na Ofisi yangu imetoa kibali cha kuwaajiri wahudumu hawa kwa sababu mwanzo kulikuwa hakuna wahudumu. Kama anakumbuka Mhe. Mjumbe kwamba tuliwahi kusafiri mimi na yeye na Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais tukafikia kwenye nyumba yako Mhe. Spika, alisafiri na wahudumu wake, lakini katika huduma zile waliazimwa pia wahudumu wa serikali kutoka Ikulu ya Chake Chake. Sasa kuondosha usumbufu huo na kwa sababu wakati ule alikuwa Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais ndio kwanza ameteuliwa katika miezi ya mwanzo mwanzo.

Kwa hivyo bajeti ya Ofisi yake ilikuwa haijazingatia kuwepo kwa wale watu, kwa hivyo mwaka mwengine uliofuta tulilazimika ofisi ya utumishi wa umma kuweka kwenye *nominal role* katika kipindi cha mwaka wa bajeti hiki kinachomalizikia sasa wahudumu kwa upande wa nyumba ya Makamu wa Kwanza wa Rais kule kisiwani Pemba na sasa hivi wameshakodi nyumba anaitumia Makamu wa Kwanza Rais. Na katika bajeti ijayo naambiwa kwamba imesema kwamba atakodiwa nyumba Dar-es-Salaam nako vile vile inabidi tuajiri wahudumu kwa ajili ya Makamu wa Kwanza wa Rais.

Kwa hivyo kama alivyokwishasema Waziri wa Nchi Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais na mimi nikasema kwamba posho hili linamuhusu Afisa Mdhamini, Makarani Muhtasi, Makarani wa Masjala pamoja na wahudumu. Wahudumu wanaokusudiwa hapa sio wale wa Ofisi ya Afisa Mdhamini ni wale wa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa upande wa Pemba, ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, kwa ufafanuzi huo nimeelewa na nimeridhika. Lakini nataka kutanabahisha jambo moja Mhe. Mwenyekiti. Niliwahi kusema juzi katika Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, kwamba maelezo haya yanaifunga serikali na yanatufunga na sisi yanabakia katika *hansard*. Nasema hivyo kwa sababu juzi nilitahadharisha kwamba nitakapofika katika vifungu huko mbele tutakuja kukumbana navyo kwamba ikiwa hivyo wanavyonieleza wao kama ni hivyo fungu hili halipaswi kuwa linabadilika mara kwa mara na likawa lina *fluctuate* hasa kwa sababu linakwenda na mishahara kwa hapa halina tatizo na ndio maana nikasema kwa hapa naliridhia.

Haya nayakubali na nayakubali maelezo haya kwamba yameingia katika *hansard* kwa sababu tutakuja kuona huko, mara hii Mhe. Mwenyekiti, niseme kabisa sisi wengine hatutokubali utaratibu wa mwaka jana kwamba ikifika kila Wizara tukaletewa mahesabu mapya, yanaletwa ghafla sio yale yaliyokuwemo katika Kamati. Hili nasema nalikubali tuendelee Mhe. Mwenyekiti, lakini mjue serikali kwamba tumeyapokea maelezo hayo kwamba hatutoyakubali kwa wizara za mbele ikaonekana kwamba yanabadilika badilika haya mafungu, sio mshahara unaongezeka posho maalum limepungua, mshahara umeshuka posho maalum limepanda inakuwa haiendani na ile *principle* nzima aliyokuwa kaibeba Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Mhe. Mwenyekiti, nakubali kwa hapa tuendelee. Ahsante.

Mhe. Spika: Tuzingatie angalizo hilo alilolitoa Mhe. Mjumbe, tunaendelea.

Kifungu 0301	Ofisi Kuu Pemba	330,175,000
Kifungu 0401		

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nimeona nianzie hapa ili kupata ufafanuzi kwa maelezo ya Mheshimiwa wangu Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, alivyoeleza kaeleza vizuri sana lakini sikupata maelezo yaliyokuwa ya kina kabisa ya kunifurahisha kuhusu fungu la fedha za walemavu.

Mheshimiwa naomba sana anisaidie *details* zile ambazo mimi nitaweza kuridhika nayo lugha yake hasa katika matumizi. Kama nilivyosema kuwa fedha zile tulizipitisha mwaka jana lakini katika utumiaji wake zilitumiwa milioni 16 na watu wamepewa *tender* na vifaa vilivyoletwa ni kidogo na hizo dawa zenyewe hazina thamani ya hizo fedha zenyewe. Nimemuomba sana Waziri mimi leo sitaki niwe mkaidi leo na hasa watu wenyewe walemavu tunavyowaona uhalisia wao, japo hilo jina sipendi kulitumia lakini sheria kumbe imenipa niweze kulitumia. Naomba sana Mhe. Waziri ili niweze kukupitishia kifungu naomba nieleze niridhike.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kama inavyoonekana katika fungu kwa mwaka wa fedha uliopita huu ambao tunaumalizia 2012/2013 Idara ya Watu wenye Ulemavu kupitia Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, tuliitengea fedha na kupitishiwa katika Bajeti shilingi milioni mia tatu kwa ajili ya ununuzi wa visaidizi vya watu wenye ulemavu.

Mhe. Spika, mchakato wa kuvipata visaidizi hivyo ulifanyika ndani ya Ofisi kuanzia mwezi wa Machi, na taratibu ilikuwa taasisi mbali mbali zile za watu

wenye ulemavu waliandikiwa na Ofisi kuleta mahitaji yao wangependa wapatiwe mahitaji gani na wote walileta katika ofisi. Kati ya waliowasilisha maelezo yao juu ya vifaa vinavyohitajika walikuwemo ZAPDD, hii ni jumuiya ambayo inahusiana na watu wenye ulemavu wa akili na wao waliletwa mahitaji yao kwamba wangependa kununuliwa dawa hizo kama sehemu ya walemavu kwa ajili ya kusaidia kutokana kwamba, lakini nilimsikia pia Mhe. Makungu akisema wakati mwengine kunatokea tatizo katika kupata dawa hizi.

Ofisi iliingia katika mchakato wa kuweza kununua dawa na visaidizi hivi na matangazo yalitolewa kukiwa na nia ya kutumia shilingi milioni mia tatu. Lakini mpaka wakati huo ikiwa tayari imeshaingizwa milioni mia moja tu ndani ya mfuko wa Ofisi yetu. Wizara ya Fedha iliahidi kwamba mara tu vifaa vile vitakapokuwa vimeletwa basi wangelipa zile milioni mia mbili kwa ajili ya kukamilisha ununuzi.

Mhe. Mwenyekiti, kumetokea matatizo ambayo mimi kama Waziri nimeyabaini gharama ambazo zilikuwa zinazungumziwa juu ya ununuzi wa dawa hizo zilikuwa ni kama milioni mia mbili na kumi na mbili, lakini kwa ajili ya visaidizi wa vifaa vyengine ilikuwa ni fedha zilizobakia pale kama milioni thamanini na kitu. Nilishtushwa kidogo kwa sababu awali nilipata taarifa kwamba kungetumika kama milioni thamanini na saba au thamanini na nane kwa kununua dawa hizi. Nilipohoji niliambiwa kwamba dawa hizi ni za ghali sana.

Mhe. Mwenyekiti, sikuridhika nilitaka majibu ya kina na nikaletewa pamoja na mchakato mzima wa shughuli ile ilivyokwenda na wale ambao walitenda katika shughuli hiyo. Nilichokigundua Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba maamuzi ya Bodi ya Zabuni ya Ofisi ambayo ndiyo yaliyokubaliwa na kikao cha bodi ya uzabuni ni kwamba kununuliwe vifaa vya watu wenye ulemavu kwa maneno mengine tunaviita visaidizi. Kidogo hii lugha ina tabu maana ukisema visaidizi dawa za watu wenye ulemavu wa akili nao ni sehemu ya visaidizi, lakini visaidizi hii bora niseme visaidizi na dawa ili ifahamike zaidi, nikisema visaidizi nakusudia vigari vya watu wenye ulemavu, magongo, lakini pia visaidizi vya kuweza kuwasaidia watu wasiosikia, fimbo nyeupe zile na vitu vya aina hii. Na nikisema dawa ninakuwa nakusudia sasa dawa hizi kwa ajili ya kusaidia ndugu zetu ambao wana matatizo katika ukuaji wa akili yao.

Maamuzi ya Bodi ya Zabuni kutokana na *evaluation team* ya Bodi ya Zabuni yalitoa fat-wa kwamba kwa sababu waliotoa tenda katika suala hili kuna utatanishi katika suala zima la bei ya dawa, basi dawa zisinunuliwe lakini suala hili lifuatiliwe. Isipokuwa tenda hii apewe kampuni inayojulikana kwa

jina la *Pison* 2008 *investment* ambayo kampuni hii ni ya Dar es Salaam na apewe tenda ya kununua vifaa kwa maana ya visaidizi vigari na vitu vyengine vyenye thamani ya shilingi 297 hiyo ndio ilikuwa maamuzi ya bodi na *minutes* hizo na nyaraka zote ziko ndani ya Ofisi. Sasa kilichotokea baada ya hapo naona kumetokea matatizo, lakini badala yake kukaingia mkataba ambao uligeuza maamuzi ya bodi ukataka kununuliwa dawa, mkataba ulioingia ni wa kununua dawa shilingi milioni mia mbili na kumi na mbili na ushei kidogo sina zile *figure* halisi, lakini ni kama hivyo na kama kidogo kilichobaki ndio kinunue visaidizi.

Mheshimiwa sio tatizo kutumia fedha hizo kwa ununuzi wa dawa maana yake ninaweza kusema *priority* kwa mwaka huu ni kuwasaidia hawa wenye ulemavu wa akili lakini miaka mengine wasaidie kwa wengine. Nilipokwenda ndani zaidi ya kulichunguza suala hili nikapata mashaka na bei ya dawa hizo. Mhe. Mwenyekiti, mimi mwenyewe nilifanya kazi ya kupita madukani kuangalia bei ya dawa hizo na nilishtushwa sana kwa sababu bei ya kidonge kimoja ni majina ya kitaalam hicho hicho ambacho kiliandikwa bei yake shilingi 9900, nikawa nasema mmh hizi dawa ghali lakini kuna kidonge ninakijua nacho kimeandikwa sijui shilingi mia sita au mia nane, nikasema sasa haya ni mashaka hebu kwanza nifanye *survey* Mhe. Mwenyekiti, mwenyewe nilipita madukani, maduka niliyopitia *survey* Shamsu na mengine ya mitaani humu tunamonunua dawa, nikagundua kidonge kile ambacho kimeandikwa shilingi 9900 bei yake ni shilingi 700 *retail*. Mhe. Mwenyekiti, hilo lilinisikitisha sana, na sikusita kufanya maamuzi ya haraka.

Katika hatua ya kwanza nilimuarifu Kiongozi wangu Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais na yeye alinambia endelea kulifuatilia na ikibidi chukua maamuzi unayoyaona sahihi. Nilifanya maamuzi ya kwanza kabisa nilimuagiza Katibu Mkuu wa Afisi kuvunja mkataba nao ulikuwa umeshakwisha. Mkataba ambao ulifungwa na huyo *Pison* kwa kuleta dawa katika bei ambayo haiingii akilini, haidhuru mkataba wenyewe ulikuwa unaishia tarehe 24 Mei, lakini wakati hali hiyo inatokea tarehe 29 mwezi wa Mei Ofisi ilipokea dawa na kuzikabidhi katika hospitali ya *Mental* maboksi manne ya dawa. Kwa hivyo haya yalikuwa yamepokelewa. Lakini pamoja na hayo yalikuwa yamepokelewa.

Lakini pamoja na hayo nikasema niende nikazione hizo dawa zenyewe nikakuta Mhe. Mwenyekiti, ni maboksi manne yapo pale lakini nikakuta wasiwasi wao uko kule kwenye hiyo hospitali kwamba na wao wamesikia thamani ya dawa hizo walizoletewa kwamba bei yake ni kubwa. Mhe. Mwenyekiti, nao walifanya kazi hao waliopelekewa dawa nawashukuru sana kwa wasiwasi wao. Maana wao waliogopa Wizara ya Afya wasije wakaambiwa wamepokea dawa ambazo zingeweza kutumika mwaka mzima

kwa thamani ya pesa hizo. Kwa hivyo walipita na wao na mimi nilipokwenda walinipa hesabu ambao wao walifanya *survey* kwenye maduka ilikuwa kama milioni kumi na sita na laki saba, ukilinganisha na milioni mia mbili na kumi na mbili.

Mhe. Mwenyekiti, nilifanya maamuzi wa kuvunja mkataba kulikuwa na *cheque* ya milioni sitini ambayo ilikuwa ilipwe tena kwa *Pison Investment* nikaagizwa ifutwe lakini pia nikaagiza suala hili lipelekwe kwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu haraka. Ninamshukuru sana Katibu Mkuu aliyatekeleza yote haya maagizo haraka sana. Lakini pia nilichukua juhudi ya kulipeleka suala hili kwa Mkuu wangu wa kazi ambaye anayesimamia shughuli za serikali Mhe. Makamu wa Pili wa Rais na sikusita katika kupeleka barua lakini nilikwenda nikamuona binafsi pia kutaka ushauri wake niendelee kuchukua hatua gani katika suala hili.

Na ninamshukuru sana yeye alinishauri kwamba Mhe. Fatma nakuagiza muandikie Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ili afanye ukaguzi katika suala hili, kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, katika hali hii huwezi kuthibitisha jambo mpaka lipatikane kisheria kabisa. Na tumekubaliana kwa mujibu wa Katiba mwenye uwezo wa kukagua mahesabu yetu ni Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali. Kwa hivyo mimi nikajibu, tuhuma ndani ya Ofisi ipo lakini tumeishughulikia na hivi sasa iko kwa *Control Auditor General.* Lakini taarifa hii pia nilimpelekea Katibu Mkuu Kiongozi na Katibu wa Baraza la Mapinduzi yeye kama Mkuu wa Shughuli za Utumishi kwa mujibu wa Katiba.

Mhe. Mwenyekiti, ninafikiri Mhe. Mshimba lakini na wengine ambao wameuliza suala hili waridhike na majibu yangu kwani sisi kama serikali tunapoona shughuli ambayo imetutia wasiwasi kidogo basi si kama vile wanavyosema kwamba sisi tunawafuga watu, aa tunachukua hatua na huu ni mfano wa hayo.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Makame Mshimba umesikia maelezo.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti niseme ni *historically* hii sasa hivi imejijenga katika Baraza hili na laiti ingelikuwa Mawaziri kama yeye huyu mama anapoambiwa jambo akali-*refer* vizuri na akaeleza jinsi gani hatua alizizozichukua, hakufanya hamaki, hivyo ndivyo tunavyotaka Mhe. Mwenyekiti. Lakini sio leo tunatoa hoja tunajibiwa hoja mtu anakujibu hoja kwa ubaya, kumbe ushalikuta lile dudu lipo. Yapo mengine yatakuja.

Sasa Mhe. Mwenyekiti mimi niseme hivi, pamoja na kukubali kupelekwa kwa Mdhibiti wa Mahesabu ningeomba Mhe. Mwenyekiti kwa heshima na taadhima tujiridhishe na sisi tuna Kamati yetu ya PAC kidogo na wao ikamsaidie Jasiri wetu mwanamama Waziri ili ripoti ile tunaitaka ifike hapa kama desturi yetu inavyokuwa. Tunaomba sana Mhe. Mwenyekiti hiyo ikubalike, akinikubalia hivyo tu nitasema tuendelee.

Mhe. Mwenyekiti: Huo ni utaratibu wa kawaida kazi hiyo itaripotiwa hapa kwa hivyo nadhani tuendelee moja kwa moja. Lakini tumpongeze sana Mhe. Waziri amechukua hatua kubwa, maana mambo yanayohusu mtu kupewa haki yake apewe.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti mimi nataka nizungumze mambo mawili kwa sababu zimebakia hoja mbili. Moja ni hii hii kwa sababu na mimi niliichangia anakumbuka Mhe. Waziri kwa ukali sana. Lakini nataka nimpongeze kwa kuwa muwazi na kuwa mkweli kwa Baraza hili. Na nawaomba Mheshimiwa leo ka-*create incident* nzuri sana kwa Baraza hili, niwaombe na mawaziri wengine wote wasiwe wao ndio kichaka cha kuwafichia watendaji wao wanapofanya madudu kama haya. Wasibebe misalaba iliyokuwa si yao. Sasa Mheshimiwa katika hili ili na mimi niruhusu tuendelee katika hili kwa sababu nimesema yapo mawili. Mimi mbali ya maelekezo yaliyokuwa yametolewa nilikuwa na ombi na suali moja.

Mimi ningelitamani sana lakini kwa sababu umeshaagiza na ninakuheshimu sana Mhe. Mwenyekiti kwamba ripoti yake itakuja hapa nakubali. Nilikuwa nataka niseme kwamba huyu aliyehusika na hili atutajie humu ndani ya Baraza leo. Lakini tumeheshimu uongozi wako kwamba litachunguzwa halafu iletwe ripoti yake hii ninaheshimu. Lakini nilikuwa nataka kusema kitu chengine Mhe. Mwenyekiti katika maelekezo ya Kamati hii nzima ya Baraza sasa hivi na ikiwa Waziri na Serikali kwa sababu inawajibika kwa pamoja ikinikubalia basi kwa hili la ubadhirifu huu nitasema tuendelee.

Mhe. Mwenyekiti jana katika Bunge Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Mhe. Wasira katika Jamhuri ya Muungano alizungumza kitu ambacho kinahusiana na hili, alisema kwamba :-

"Inashangaza sana huu utaratibu uliowekwa ambao umekusudiwa ukwepe na iisaidie serikali kukwepa matumizi mabaya, utaratibu wa kwenda Kamati na taasisi za zabuni katika mawizara haiwezekani".

Kwamba inastaajabisha leo kifaa ambacho unakwenda kukinunua wewe binafsi ukienda ukikiuliza bei yake tofauti na ni ndogo lakini ikiingia katika taasisi ya zabuni basi inakuwa mara kumi zaidi yake kama ilivyoonekana

katika dawa hizi. Sasa mimi nilikuwa nataka kusema kwamba serikali ilichukuwe kwamba ipitie tena utaratibu mzima huu wa kamati za zabuni, na kama kuna haja ya marekebisho ya sheria mbali mbali zinazohusika tuletewe hapa ili tukomeshe utaratibu huu.

Mhe. Mwenyekiti mfano huu unatoa hali halisi, tunaposema hapa watendaji wanajenga majumba mtu alikuwa hana chochote hebu fikiria Mhe. Mwenyekiti thamani ya shilingi milioni kumi na sita ikafika kukisiwa kwamba ni thamani ya zaidi ya shilingi 290 milioni. Hiyo ni *transition* moja tu Mhe. Mwenyekiti inakuonesha kama mtu huyo anapata *transition* tatu hajajenga nyumba ya ghorofa Mhe. Mwenyekiti. Na hii ni moja tu kwa hivyo nasema ni suala zima la zabuni serikali ilipokee kwamba lifanyiwe marekebisho hilo moja.

Mhe. Mwenyekiti la pili la vifungu vya Idara ya Mipango Sheria na Utafiti sasa hivi sio la sera ya jumla ya wizara lina vifungu mahsusi, tena ninamshukuru Waziri kwamba katupa maelezo katika vifungu ambavyo tulikuwa tumevihoji, sasa mimi Mhe. Mwenyekiti nilikuwa naomba maelezo ya ziada. Bado napata tatizo na haya maposho, posho maalum kwa sasa hivi naivutia pumzi kutokana na maelezo aliyokuwa katupa lakini hapa kuna mafungu kuna posho ya gharama za safari, maelezo ya waziri hii Mhe. Mwenyekiti ukurasa wa 80 *vote* 220301 katwambia imeongezeka kutoka milioni tano hadi milioni kumi na tatu kwa sababu Idara hii imepangiwa sasa kufanya masuala ya mafunzo kuhusiana na mambo mbali mbali yanaratibiwa na Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais.

Lakini katika maelezo yake na naomba afanye *reference* mwenyewe kasema ni pamoja na suala la mafunzo ya kuwatoa watu kutoka Pemba kuja Unguja kushiriki mafunzo hayo. Sasa watendaji hawa wa Wizara au Ofisi hii ninavyofahamu mimi Mhe. Mwenyekiti kwa Pemba wana bajeti yao ambayo tumeipitisha punde Ofisi Kuu Pemba na pale pia pana fungu la gharama za safari, ambalo madhumuni yake hasa ni kuwawezesha hawa kutoka Pemba kuja Unguja pale wanapohitajika.

Sasa hiyo imenipa mashaka Mhe. Mwenyekiti kwa sababu gani, hapa tumepewa maelezo hayo, lakini katika lile la viburidishaji vile vile katika Idara hii hii tumeambiwa kwamba ni kuhudumia hivyo vikao liko katika 220201 sikusudii kuhoji mengine nahusisha pamoja tu. Lakini ukienda katika posho, vikao na kamati pale juu kuna milioni kumi na saba tunaambiwa zimetajwa sehemu zile zile, sasa najiuliza kwamba shughuli moja kwa nini mambo yake yawe kila pahala hoja ndio ile ile.

Kwamba ukija katika viburudishaji ni semina kuhusu walemavu, dawa za kulevya, ukija katika posho za malazi ndio zile zile, vikao na kamati maelezo ni yale yale, gharama za safari maelezo ni yale yale. Na kama nilivyosema ikiwa itakuwa unatoka Pemba tayari wana fungu lao la gharama za safari kutoka Pemba. Kwa hivyo nilikuwa bado naomba Mhe. Waziri katika hili anisaidie maelezo. Kwamba kwa nini kwa jumla fungu la Idara ya Mipango, Sera na Utafiti katika mafungu kama haya limenona na kumekuwa na tofauti kubwa sana kutoka mwaka jana ukilinganisha na mwaka huu katika mafungu hayo niliyokuwa nimeeleza Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Ahsante sana Mhe. Spika, naomba nitoe maelezo yafuatayo kwamba lile fungu la Pemba ni kwa ajili ya uratibu na shughuli za usafiri kwa wale wafanyakazi wa Ofisi Kuu iliopo pale Pemba. Lakini ikisha kuna kazi. Kuna Ofisi ya Idara ya Mazingira Pemba, kuna Ofisi ya Idara ya Watu wenye Ulemavu, kuna Kitengo cha Sera na Mipango kule Pemba. Sasa kwa zile *core functions* hizi zilizopo hapa katika sera na mipango ni *core functions* za sera na mipango katika utekelezaji wa shughuli zake ambazo ndio fedha zake zinaonekana hapa. Zile zilizoko Pemba ni kwa ajili ya wale *staff* na nimesema wale *mastaff* wanaokuja hapa kwa ajili ya kupanga bajeti, kwa ajili ya kuhudhuria vikao vya Baraza, kwa ajili kushughulikia shughuli za utumishi na stahiki za wafanyakazi zile za uratibu wa shughuli za Ofisi Kuu.

Lakini zile moja moja basi zile ziko zinaonekana hapa katika Sera na Mipango. Na hizi za hapa ni katika *core function* ya sera na mipango ndizo zitakazopelekwa kule kwa ajili ya kuwaleta wale kule kwa ajili ya shughuli hii.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti kwanza nimshukuru Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa ufafanuzi mzuri, nilikuwa niongezee hili jengine linalohusu zabuni ambalo Mhe. Jussa amelitolea ufafanuzi.

Mhe. Mwenyekiti ni kweli utaratibu tulionao wa zabuni haujatusaidia sana, ukiangalia mara nyingi maneno ambayo Mhe. Wasira ameyasema na Mhe. Jussa ameyasema yana ukweli ndani yake, kwamba utaona vitu kupitia zabuni vinakuwa ghali zaidi kuliko kama wewe mwenyewe ukienda kununua utaviona bei yake iko chini kidogo. Kwa sababu hiyo basi hili jambo tumeanza kulifanyia kazi na kwa *speed* hii ambayo Waheshimiwa Wawakilishi wanaliunga mkono basi tutalifanyia kazi serikalini tutizame utaratibu gani mzuri zaidi utakaotusaidia ili fedha za umma ziweze kutumika kwa yale mahitaji ambayo kama yalivyokusudiwa na kwa bei muafaka. Kwa sababu ni kweli inajitokeza wakati mwengine kuwa na gharama kubwa. Kwa

hivyo ushauri huu tunauchukua tutaufanyia kazi Mhe. Mwenyekiti . Ahsante sana.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti kwa hili la upande wa taratibu za zabuni ninashukuru maelezo ya Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ambaye katika Baraza hili ndiye Mnadhim Mkuu wa Serikali, lakini vile vile ndio Waziri mwenye dhamana ya uratibu wa shughuli za serikali. Kwa hivyo ninachukua kauli yake ni kauli nzito na kwamba ataisimamia na kuifanyia kazi.

Hili la vifungu Mhe. sitaki niizuie kamati hii ya matumizi hapa nataka niruhusu tuendelee lakini kwa maelezo yafuatayo Mhe. Mwenyekiti.

Kwanza naendelea kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji kwamba kama walivyosema wenzangu amekuwa wazi na mkweli katika kujibu hoja zake zote. Lakini nasema mimi siamini kwamba haya ni matatizo ya Mawaziri yaliyojitokeza. Kwa hivyo nataka niruhusu niendelee lakini naomba kama nilivyosema juzi na alitueleza vizuri Mhe. Mwenyekiti, kwamba kamati inayohusika na itakapofika Tume ya Ukimwi Mheshimiwa nimejiandaa vizuri hapa nitakuja kuelezea msingi wa hoja hiyo sitaki kuendelea kurudia kila wakati, ikifika huko nitakuja kueleza.

Lakini naomba kamati inayohusika na bahati nzuri Mhe. Hamza Hassan Juma Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa lakini pia ana kofia mbili, Mwenyeviti wa Wenyeviti maana yake yeye kama Mhe. Seif Bakari Mwenyekiti huyu ana viti vingi Mhe. Mwenyekiti. Nategemea kwamba atalisimamia hili na haya mafungu ambayo tumeyahoji haya kama nilivyosema kuanzia posho vikao na kamati, kwenye chakula na vinywaji na safari ziridhishe na ziakisi yale maelezo ambayo Mhe. Waziri na mimi nina hakika kapewa na watendaji wake. Kwa sababu anasema yeye anatayarishiwa na watendaji wake. Tuone kwamba kweli fedha hizi zinafanywa shughuli iliyokusudiwa yaani kwamba watapotoka watendaji Pemba kuja hapa kwamba zinahudumia hizi na kama zitafanya shughuli zile *core function* kama alivyosema Mhe. Waziri katika kupanga masuala ya fedha. Kwa sababu gani Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu katika hizo Idara yenyewe zinazohusika yapo mafungu ya safari na katika maelezo yake mwenyewe Mhe. Waziri katwambia kwamba Idara inahudumia Unguja na Pemba, kwa hivyo anategemea fedha zile zinatumika pia kusafirisha Wajumbe baina ya Unguja na Pemba. Kwa hivyo nasema maneno yale nimeyatia katika *Hansard* kwa hivyo naomba Kamati inayohusika ifuatilie. Kwa sasa naruhusu tuendelee Mhe. Mwenyekiti.

Kifungu 0401 Idara ya Mipango Sera na Utafiti 160,065,000
Kifungu 0501

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Mhe. Mwenyekiti nilipokuwa nachangia jana niliomba baadhi ya vifungu nipate ufafanuzi na ninashukuru Mhe. Waziri alipokuja hapa amejitahidi kutoa ufafanuzi lakini bado naomba ufafanuzi wa ziada juu ya kifungu 212101. Katika mchango halisi wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii. Mwaka jana Mhe. Mwenyekiti tumetumia milioni kumi na nane lakini mara kuna milioni sitini na sita. Sasa naomba ufafanuzi wa kina zaidi.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Ahsante Mhe. Mwenyekiti niombe radhi ni kweli hilo alilihoji Mhe. Mahmoud lakini nilisahau kulitolea maelezo. Mhe. Mwenyekiti mwaka huu katika muongozo ambao tulioupata serikalini shughuli ya maposho, mishahara ikiwemo pia mchango wa mfuko wa hifadhi wa ZSSF tulipewa muongozo kwamba hawa wawekwe katika fungu la Uendeshaji na Utumishi na ndio sababu fungu hili likaonekana kupanda mno. Hapa kuna Idara nyengine zimeingia.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti ukiondoa hili ambalo Mhe. Waziri ameshatoa ufafanuzi ingawa niseme tu kwamba limetupa tabu wengi mara hii. Kwa sababu kama muongozo wa Wizara ya Fedha ni huo tungetegemea ungefuatwa na Wizara zote lakini Ofisi ya Makamu wa Pili iliyopita kila Wizara na Idara ilikuwa na fungu lake. Kwa hivyo nasema hiyo ni serikali ikajirekebishe wenyewe tu, lakini nirudi katika hili Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Mwenyekiti katika mafungu ambayo yanaonekana kuongezeka katika Ofisi hii na katika Wizara nyengine mbali mbali ni fungu hili linalohusu huduma za mtandao.

Katoa maelezo nimeyapokea na hili lilikuwa linahusu kwenye voti 220100 kwenye gharama za vifaa huduma za mawasiliano kifungu kidogo pale cha 220108. Huduma za mtandao mwaka jana ilikuwa milioni nne laki tatu ishirini elfu, mwaka huu imekuwa milioni 12. Lakini kaungwa mkono na upande wa pili huku kwenye vifaa vya kompyuta, kwenye ukurasa wa 83 *vote* 220500 vifaa na huduma za ofisi kifungu kidogo cha 220504 vifaa vya kompyuta, ambapo mwaka jana ilikuwa milioni tano, mwaka huu milioni thalathini na mbili laki mbili hamsini elfu. Katika maelezo yake Mhe. Waziri katwambia wanakusudia kununua *server* yao wenyewe. Sasa Mheshimiwa nilikuwa naomba maelezo juu ya mambo hayo mawili. Kwanza serikali mwaka juzi ilikuja na kishindo kikubwa Barazani na mradi mzima wa mkonga wa taifa ulioambatana na *E-Government* na maelezo yake tuliambiwa

ni kwamba mradi ule ungepelekea gharama za mtandao kushuka kwa kiwango kikubwa sana si tu kwa serikali lakini mpaka kwa sisi wananchi wa kawaida.

Sasa mwaka huu tulichoshuhudia katika kila Wizara gharama za mtandao zimeongezeka baada ya kuwa mradi wa mkonga wa taifa umekamilika na *E-Government* imekamilika. Sasa nilikuwa naomba maelezo haya, lakini pia nilikuwa naomba anisaidie hii *server* inayoambiwa kwamba *server* ni ya mtandao iliyotoka kufikia thalathini na mbili milioni gharama zake halisi ni kiasi gani. Naomba anipe *break down* ya hivi vifaa vya kompyuta hapa ya hii milioni thalathini na mbili zaidi ya maelezo ambayo kayatoa.

Kwa hivyo nilikuwa naomba maelezo hayo moja kwa serikali nauliza kwa jumla kwa nini *E-Government* na mkonga wa taifa umekamilika gharama za mtandao hazijashuka zinapanda zaidi ya mara mbili? Lakini pili kwa nini katika hili milioni thalathini na mbili iliyokuwa imetajwa hapa limeongezeka sana na nini *break down* yake naomba maelezo Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Mhe. Mwenyekiti naomba kutoa maelezo yafuatayo. Hivi sasa nilitoa maelezo kwamba gharama zetu za matumizi ya mtandano wa *internet* kwa hivi sasa zimepanda. Kile ambacho tulikuwa tunatumia kutokana na ukubwa wa Ofisi na matumizi sasa hakitoshi na tumekuwa na mtandao ambao uko *slow* sana. Kwa hivyo tuna nia ya kuboresha na gharama zake katika mtandao huo sasa itakuwa ni shilingi milioni moja kwa mwezi.

Lakini vile vile katika suala zima hilo analolizungumzia la kuja kwa *E-Government* tumepewa maelekezo na serikali kwamba kila mmoja ajiandae katika kuweka *LAN* Mhe. Spika, kwa hapa sina *break down* halisi ya bei hii labda niombe nimletee hata kesho kwa kuwa suala hili sikujua kwamba litaulizwa hapa na *break down* zake, lakini ni maelekezo ya serikali kwamba hii ni miundombinu ambayo itahitajika ili huo mkonga uliopo uweze kutumika. Na hizo gharama kila ofisi imetakiwa izibebe wenyewe.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti ninamshukuru Mhe. Waziri bado nashindwa kuoanisha. Kama nilivyosema hili si la Ofisi ya Makamu wa Kwanza ni la serikali kwa ujumla wake; suala la kukamilika kwa mkonge wa taifa na mradi wa *E-Government* ambao tuliahidiwa kwamba kuja kwa *fiber optic* mkonge wa taifa kungepelekea gharama hizi kushuka, lakini kama nilivyosema inaonekana mwaka huu zimepanda katika kila Idara. Sasa nisipoteze muda naomba niruhusu tuendelee lakini kama nilivyosema Mhe. Mwenyekiti aidha kutapendekezwa hapa.

Kwanza Baraza hili limebadilika sana Mhe. Mwenyekiti kadri linavyokwenda tunajifunza zaidi na mafunzo mnayotupatia yanabadilisha uzalishaji wa kazi katika suala zima la kuisimamia serikali ambalo ni jukumu lake la Kikatiba. Sasa nilikuwa naomba kwa mwaka unaokuja Mhe. Mwenyekiti kila kamati tukishamaliza kupitisha haya, mwaka huu mmetusaidia sana Ofisi ya Katibu wako Mhe. Mwenyekiti, kwamba tulipewa katika kila kamati lile buku dogo ambalo lilikuwa na *vote* za Wizara ambazo zimefanyiwa Kamati husika. Sasa zile tutazokuwa tumezipitisha hapa zikikamilika basi tufanyiwe kama yale, yale ndio muongozo yale tulopitisha hapa kwa kila kamati katika kwenda kufuatilia matumizi halisi ya fedha hizi.

Kwa sababu moja katika kazi za kila Kamati Mhe. Mwenyekiti ni kuangalia *value for money*, thamani halisi ya matumizi ya fedha kulingana na lengo lililokusudiwa. Kwa hivyo nasema tusiendelee kuja kupiga kelele kwa mambo ambayo ni ya kitaalamu, tuiachie kamati husika lakini naomba Ofisi yako Mhe. Mwenyekiti kupitia Katibu itutayarishie yale tutakayoyapitisha yatakuwa yamebadilika, yatakuwa yamepunguzwa yamepelekwa kule, ili kuanzia sasa utaratibu wa kamati sio kupata maelezo tu lakini uende kwenye matumizi ya fedha halisi zilizokusudiwa.

Baada ya kwisha kusema hayo Mhe. Mwenyekiti naomba niruhusu tuendelee kwa kuelewa kwamba kaka yangu Mhe. Hamza atakwenda kutafuta bei halisi ya ile *LAN* katika vifaa vya kompyuta ajue kwamba zinaakisi milioni thalathini zilizokuwa zimetajwa hapo. Mhe. Mwenyekiti naomba tuendelee. Ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Ofisi yetu imesikia hiyo itachukua hatua zinazofaa.

Kifungu 0501 Idara ya Uendeshaji na Utumishi 1,329,827000
Kifungu 0601 Tume ya Taifa

Mhe. Salma Mohammed Ali: Mhe. Mwenyekiti wakati ninachangia nilimuomba Mhe. Waziri anipe ufafanuzi wa pale palipoeleza katika rasimu ya maelezo ya bajeti inayotumia programu ya PBB kuhusu kuwepo kwa jamii ya Wazanzibari kuwa huru na matumizi ya dawa za kulevya. Lakini Mhe. Mwenyekiti katika majumuisho sijapata jawabu hilo. Ninamuomba Mhe. Waziri anipe ufafanuzi.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, ni kweli Mhe. Salma alitaka maelezo juu ya hilo, na hapa niseme tu kwamba labda Kiswahili na tafsiri inategemea vile mtu anavyokitafsiri. Mfano nikichukulia kwamba mfungwa anayekuwa huru maana yake sasa anaweza kujifanyia mambo yake vile anavyotaka. Lakini

hapa ninachokiona ni kwamba imetumika *direct translation* ya kizungu kwenda kwenye Kiswahili. Tunachokusudia hapa ni kwamba kuwa na jamii ya Wazanzibari ambayo haitakuwa kwenye matumizi, itakuwa huru yaani haibugudhiwi na dawa za kulevya au kuingiliwa na matumizi ya dawa za kulevya. Sivyo hivyo vyengine ambavyo kwamba watakuwa huru hakuna sheria ya kudhibiti kwa hivyo atakuwa huru kutumia dawa za kulevya.

Ni *direct translation* ninafikiri si Kiswahili kizuri tunahitaji kurekebisha labda ili kieleweke vizuri. Kwa sababu tafsiri zinaweza kuwa kadri ya mtu atakavyoichukua kwa Kiswahili hichi tulichoweka. Tunalichukua hilo Mheshimiwa kwa ajili ya kufanya marekebisho.

Mhe. Mwenyekiti: Maneno mafupi ni kwamba sio uhuru wenyewe kwamba tubugie tu tena aa, ila ni kwamba nchi yetu iwe haina hayo matatizo.

Mhe. Salma Moh'd Ali: Mhe. Mwenyekiti, naomba kwanza nikiseme hichi kifungu chenyewe. Programu ya kwanza ni udhibiti wa dawa za kulevya ambayo tumaini lake kubwa ni kuweko jamii ya Wazanzibari kuwa huru na matumizi ya dawa za kulevya. Sasa Mhe. Mwenyekiti, mimi hapa nikitizama kuwa huru ni kuwa mtu afanye kitu bila ya kubughudhiwa bila ya kero, kwa hiyo namuomba Mhe. Waziri, ikiwa kuna neno jengine la kutumia hapa basi litumike, lakini kuwa huru kila atakayesema ataona kuwa karuhusiwa sasa kufanya au kutumia dawa za kulevya.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, nakubaliana naye na naahidi kwamba tutafanya marekebisho ili hii lugha isije ikaleta tafsiri nyengine.

Mhe: Mahmoud Muhammed Mussa: Mhe. Mwenyekiti, jana nilipokuwa ninachangia pia nilipofika katika eneo hili niliomba kupata maelezo vile vile katika eneo la ununuzi wa mashine na zana, katika kasma 311020 ilikuwa kuna ununuzi wa gari, hapa ununuzi wa gari unagharimu 51,000,000/=, lakini pia huku mwisho kwenye Ofisi ya Faragha kuna gari nyengine ambayo itakuwa inanunuliwa kwa 165,000,000/=. Sasa nilitaka kupata ufafanuzi hizi ni aina gani za gari wakati zote zinatumika katika ofisi moja. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa ufafanuzi ufuatao. Hii inayoonekana katika fungu 311202 shilingi milioni hamsini na moja na laki tisa, hii hivi sasa Tume ya Uratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya, Mhe. Mwenyekiti, hata kiongozi wake ambaye ndie Mkurugenzi Mtendaji hana gari, haina gari kabisa hii ofisi. Na kwa sasa tulitenga mwaka jana kuweza kununua, hata hivyo fedha hazikupatikana mwaka jana lakini imegundulikana pia kwamba kwa bei hiyo

tusingepata gari ambayo ingeweza ikatumika kwa muda kwa ajili ya shughuli za ofisi. Kwa sababu ni *multi purpose*, gari hiyo anatumia kiongozi lakini vile vile tuliitaka itumike kwa ajili ya kazi nyengine. Kwa hivyo tulipata makisio ya kununua gari ya shilingi milioni hamsini na moja nafikiri kutoka kampuni ya *Toyota* makisio kama yapo. Lakini pia lile jengine ni la Ofisi ya Faragha, hayo ni magari mawili tafauti Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nitatoa hoja fupi sana hapa, hasa kwa sababu Mhe. Waziri ni mpiga kura wangu katika Jimbo la Mji Mkongwe, na kura yake alinipa mimi nina hakika.

Mhe. Mwenyekiti, hapa sitaki kwenda katika vifungu kwa sababu kwa jumla yameulizwa ya kuulizwa. Katika mchango wangu Mhe. Mwenyekiti, niliuliza suala ambalo nafikiri kwa sababu Mhe. Waziri, tulimzonga na mambo mengi hili kidogo alighafilika nalo. Hili linahusu kwamba nilipochangia nilisema Tume ya Taifa ya Uratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya, hichi ndicho chombo ambacho tumekipa jukumu la kuendesha hayo mapambano kwa kuyasimamia, na nilikumbusha katika mchango mwaka juzi mapema nikiwa Mjumbe wa Kamati ya Katiba na Sheria ya Baraza lako Mhe. Mwenyekiti. Katika sheria ambazo zimeletwa mapema ni sheria ya marekebisho ya sheria inayounda chombo hichi ambapo ilikiimarisha zaidi. Sasa nilipokuwa nikichangia Mhe. Mwenyekiti, nilisema nastaajabu kwamba kwa chombo kikubwa kama hichi ambacho kimepewa jukumu, na nadhani kwa mujibu wa yale marekebisho ya sheria tuliyofanya kilikuwa kikutane angalau mara mbili kwa mwaka, kama sivyo atarekebisha Mhe. Waziri.

Mhe. Mwenyekiti, katika hotuba yake Mhe. Waziri, katuripotia kwamba kimekutana mara moja tu kwa mwaka mzima wa fedha, sasa nikasema na nakumbuka nilimletea orodha hapa ya matoleo mbali mbali ya habari yanavyochora taswira ya Zanzibar katika Ulimwengu wa kimataifa. Sasa nikasema kwa sababu tunasema kwamba tumejikita kupambana na hili nilitaka maelezo na hili sikulisikia kwamba nini kilikwamisha ikawa Tume hii muhimu ambayo inajumuisha Polisi, inajumuisha Idara mbali mbali za Serikali inazohusika na masuala haya, Vikosi vya SMZ, wao wenyewe katika ofisi yao, ni chombo ambacho kimewakusanya wakubwa wote ili kuweka mikakati na kupokea taarifa bila ya shaka ya haya mapambano. Sasa ndio nikasema kwamba katika kipindi hicho matukio mabaya mabaya yameripotiwa na inaharibu sura ya nchi yetu, sasa nikasema kwa nini walikutana mara moja.

Mhe. Mwenyekiti, mimi ninaliuliza kwa sababu gani, kwa sababu aliuliza hapa Mjumbe mmoja kuhusu bajeti yake na nashukuru katika maelezo kasema kwamba hii bajeti inaonekana imepungua kwa sababu imekata fungu

la mishahara na zile posho maalum ambapo nikitumia kigezo cha mwaka jana basi ilikuwa tuongezee milioni sabiini na nane na milioni kumi na nne za posho maalumu ingekuwa inakaribia na hii ya mwaka jana milioni mia mbili na arubaini na saba. Sasa hoja yangu Mhe. Mwenyekiti, kwamba je, ikiwa milioni mia mbili na arubaini na saba za mwaka jana hazikuwawezesha kukutana mara mbili na ni kikao kizito hichi, vipi kwa bajeti ile inategemea chombo hichi tukakiwezesha kikafanya shughuli vizuri. Aje anieleze Mhe. Waziri, kwamba vipi bajeti hii itawezesha kufanya Tume hii iweze kukutana angalau mara mbili ili mapambano haya ya dawa za kulevya, janga la taifa letu hasa vijana iweze kuendeshwa vizuri Mhe. Mwenyekiti, naomba maelezo.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli Mwakilishi wangu Mhe. Jussa, alihoji juu ya suala hilo na nilijibu kwamba kikao tulikifanya mwezi wa Januari ambacho naomba nitoe maelezo tu kwamba hicho kilijadili kwa kina mpango ule wa utekelezaji wa sheria ya udhibiti wa dawa za kulevya na kutengeneza hiyo *road map* kwa ajili ya utekelezaji wa sheria hiyo. Tulipanga kwamba *road map* hiyo iende Serikalini, ipitishwe na ilikwenda mara ya kwanza ikarudishwa kwa ajili kwamba iwekewe bajeti yake pia kabisa kwa kila mdau vipi ataweza kutekeleza majukumu yake.

Waheshimiwa Wajumbe wanatuasa juu ya *coordination*, kwa hivyo hii *road map* inaonesha hiyo *coordination* na kila mdau na vifaa anavyohitajia na fedha anazozihitajia kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli hii.

Tulipanga Mhe. Mwenyekiti, baada ya kufanya marekebisho ya kuuwekea bajeti mpango huo ulirudi tena Serikalini na hivi sasa umeshakuwa *approved* na Serikali kwamba uko tayari uendelee wenye thamani ya karibu zaidi bilioni moja na milioni mia saba.

Fedha zake sio kidogo kwa ajili ya wadau wote hawa, wahusika wote, lakini tunajua kwamba kiasi kilichotengwa hiki ni kidogo, kwa maana ya kufanya vikao viwili kwa mwaka fedha hizi hazina tatizo, lakini kwa maana ya utekelezaji wa shughuli zenyewe kwa kweli ni tatizo, lakini kwa kweli tunategemea kwamba fedha tuziombe na tayari maandiko ya kuombea fedha hizi yamepelekwa katika sehemu mbali mbali, lakini vile vile Serikali yenyewe ilisema itafanya kila jitihada ili kuona kwamba fedha zinapatikana ili mpango huu uweze kutekelezeka. Kwa maana ya vikao Mhe. Mwenyekiti, naomba nimuhakikishie Mhe. Mjumbe, kwa vikao viwili vya Tume bajeti inaruhusu.

Mhe. Ismail Jussa ladhu: Mhe. Mwenyekiti, kwa maelezo hayo ni mategemeao yangu kwamba bajeti itaruhusu na kwamba vitafanyika basi naomba tuendelee.

Kifungu 0601 - Tume ya Taifa ya Uratibu na Udhibitiwa Dawa za Kulevya 160,117,000/=

Kifungu 0901

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, katika fungu la Idara ya Mazingira au kifungu kidogo cha Idara ya Mazingira, nilikuwa naomba kupatiwa maelezo kidogo katika vifungu ambavyo viko katika ukurasa wa 89. Kwanza kuna fungu pale nambari 263100 ruzuku, fungu dogo la 263110 Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira. Mhe. Mwenyekiti, fungu hili ni milioni arubaini na tano laki nne na arubaini na tatu elfu, ambayo ni pungufu kutoka mwaka jana ilikuwa arubaini na tisa milioni lakini mbili ishirini na nne elfu.

Mhe. Mwenyekiti, Wajumbe wengi waliochangia hapa katika Ofisi hii nikiwemo na mimi, katika suala ambalo tumelipigia kelele sana ni suala zima la usimamizi wa kazi ya kuhakikisha kwamba mazingira yetu yanatunzwa, miradi ya mahoteli na ujenzi ambao hauzingatiwi mazingira. Uchafu katika miji na katika maeneo mbali mbali ya miji yetu, makaro yanayofoka ambayo yanayokosa usimamizi, uratibu wa Idara mbali mbali za Serikali zinazohusika na mazingira ili kuweza kutilia nguvu sheria na kanuni zake. Sasa nilikuwa najiuliza kwamba kwa kazi nzito kama hii ambayo athari yake imeanzia Tumbe kwa Mhe. Rufai mpaka Mji Mkongwe hapa Unguja. Lakini amekuja akazungumza vyanzo vyake vipi bajeti hii imeshuka na tutegemee kwamba milioni arubaini na tano zitatosheleza, je hichi ni kipaumbele cha Wizara au Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais katika kusukuma mbele suala la mapambano dhidi ya uchafuzi na uharibifu wa mazingira, nilikuwa naomba maelezo hayo.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa maelezo yafuatayo. Ni kweli hapa kunaonekana kuna upungufu wa karibu milioni nne hivi kutoka arubaini na tisa mpaka arubaini na tano, na hii haimaanishi kwamba hichi sio kipaumbele chetu, ni kutokana tu kwamba bajeti yenyewe nayo ni pungufu na kumejitokeza mahitaji mengine ambayo mwaka jana hayakuwepo au yalikuwa sio gharama kubwa na ndio zile kidogo zimekwenda kujazia katika mafungu yale.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, ningelikuwa mgumu lakini kwa sababu uko mbele nina akiba ya uchawi wa kusaidia kuliongeza hili fungu nasema tuendelee.

Kifungu 0901 - Idara ya Mazingira 127,884,000/=
Kifungu 2101 - Idara ya Watu wenye Ulemavu

Mhe. Hijja Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nikushukuru kunipatia nafasi hii kwa mara ya kwanza. Nilihoji jana kwenye Idara ya Watu wenye Ulemavu kwamba Wizara iliandaa chakula cha usiku na kuahidiwa fedha nyingi kwenye chakula kile cha usiku. Mhe. Waziri aliripoti kwamba sasa hivi Idara ina milioni mia moja tisini na nane nukta mbili. Naomba kujua kwanza ziko wapi hizi kwa sababu nimetishika kwamba kuna baadhi ya watu hutumia *deal* ya baadhi ya wagonjwa kwa kupata maslahi yao, kwa hivyo niambiwe hizi ziko wapi na ziko salama, na pili nikaomba kwamba hizi nyengine ambazo zimeahidiwa ni ngapi na lini zitapatikana, naomba maelezo.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa majibu yafuatayo. Ni kweli shughuli hiyo ya uchangishaji kwa ajili ya kutunisha mfuko wa maendeleo ya watu wenye ulemavu ilifanyika na nimeeleza kima ambacho hivi sasa kimo ndani ya *account,* na *account* hii ni salama ni *account* iliyopo katika Baraza la Watu wenye Ulemavu na mfuko huu upo kisheria umetajwa mule ndani ya sheria hii ya watu wenye ulemavu. Kilichokuwa hakijafanyika kwa sasa tunataka kuandaa kanuni na kuweza kuweka vipaumbele vya jinsi gani ya kutumia fedha hizo kwa sababu mahitaji ya watu wenye ulemavu ni makubwa mno kuliko kile kilichopo.

Mhe. Mwenyekiti, nasikitika kwamba sina zile *data* kwa ajili tu mambo yalikuwa mengi sana inayoonesha kima kilichobakia, lakini kwa ghafla hivi ni kama thamani hiyo hiyo iliyopo ndani ya *account* maana yake tulipata kama milioni mia tatu na kidogo. Na kwa kweli tunafanya jitihada na juhudi za kuwafuatilia wale ambao wametoa ahadi kuwahimiza na kuweza kuleta michango yao, siwezi moja kwa moja nikajibu ni lini mfuko huo utakamilika kama ahadi zilivyotolewa. Nitoe tu rai na Mhe. Mwenyekiti, wako wengine ni Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi humu wametoa ahadi nao niwashajiishe basi nao waweze kutimiza ahadi zao ili tuweze kuwasaidia ndugu zetu hawa wenye ulemavu. Na niseme kwamba mfuko huu ni endelevu si kwamba tumeuchangia mara moja, lakini wale wote wenye nia ya kusaidia basi wanaweza ku-*deposit* katika mfuko ili kuweza kuwasaidia watu wenye ulemavu.

Mhe. Hijja Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, niendelee kumpongeza Mhe. Waziri kwa niaba ya Wizara yake, lakini kwa sababu mwaka mmoja ni mkubwa naomba akubali kutuandikia, kuandikia ofisi yako kwamba ile ahadi iliyotolewa siku ile milioni fulani ili Wawakilishi iwe rahisi kufuatilia kilichopatikana na kilichobaki, na kama ilivyokubalika basi naomba tusaidiwe

maandishi hayo kwa kutumia ofisi ili Kamati zetu za Baraza iwe rahisi kufuatilia zile fedha. Mhe. Mwenyekiti, naomba kupatiwa maandishi hayo.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, ninaomba kidogo nimsaidie Mhe. Waziri baada ya kueleza maelezo mazuri, lakini naona kama hakuridhika Mhe. Hijja. Mimi ndiye Mwenyekiti wa Mfuko wa Maendeleo ya Watu Wenye Ulamavu, tumepata matamko sio fedha ni ahadi ya shilingi mia mbili na tisini na saba milioni ndio ahadi zilizotoka. Lakini tukapokea milioni mia moja na tisini. Katika milioni mia moja na tisini tulitumia kwa shughuli ile milioni thalathini na tano, kwa hivyo sasa hivi tunazo kitita milioni mia moja hamsini na tisa mia mbili tisini na tano mia mbili thalathini na sita, hizi zipo katika *account* hazijatumika mpaka hapo tutakapotoa taarifa kamili ya kutumia fedha hizi kwa walengwa.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, kwenye Idara ya Watu Wenye Ulemavu kulikuwa na masuala mawili; la kwanza liko katika ukurasa wa tisini na moja kati kati pale, fungu 220500 vifaa na huduma za ofisi, *office supplies and services.* Kijifungu 220504 vifaa vya *computer, computer accessories supplies*, mwaka jana ilikuwa 510,000/=, mwaka huu ni 35,920,000/=. Sasa kama na hapa inataka kunuliwa *server* na ile *line*, lakini kwa kadiri ya ufahamu wangu na naomba kama sivyo anirekebishe ninavyoiamini kwamba Idara hii iko pale pale Makao Makuu ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza, kama sivyo naomba nirekebishwe. Sasa nilitegemea ile tuliyoambiwa katika Idara ya Utumishi na Uendeshaji ambapo palikuwa na 32,250,000/= kwa shughuli kama hiyo ya vifaa vya *computer* hasa kwa hili la *server* lingefaa kwa wote katika majengo yao mawili ambayo yapo pamoja pale. Sasa naomba nilikuwa naomba kusaidiwa kwamba hivi vifaa vya *computer* 35,920,000/= ni vifaa gani, kwa sababu hii si *computer* ni *computer accessories* ndio itakayopatikana kwa thamani hii kubwa.

Mhe. Mwenyekiti, la pili nimalizie kabisa linahusu fungu liliopo katika kifungu kilichokuwa katika ukurasa wa 92, chini ya kijifungu 282100 pale kati kati matumizi mengineyo, katika kijifungu kidogo cha 282111 sherehe za kitaifa mwaka jana ilikuwa 6,200,000/= mwaka huu ni 15,047,296/= naomba maelezo.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, naomba nianze na lile la kwanza la vifaa vya *computer* fungu 220504. Na Mhe. Mwenyekiti, nililitolea maelezo hili kwamba kuna ongezeko la idadi ya *computer* mwaka 2012/13 zilikuwa nne lakini kwa mwaka 2013/14 sasa tunaokwenda nao kuna *computer* nane, lakini pia kuna ongezeko la idadi ya *printer* kutoka tatu hadi kufikia saba lakini vile vile

photocopy machine ambayo nayo huenda ikahitaji vifaa kwa ajili ya kutengeneza wakati mwengine inapoharibika.

Lakini katika fungu hili hili pia kuna fedha ambayo itahusika na utengenezaji wa *data base* ya watu wenye ulemavu, tumekusanya *data* na sasa tutatengeneza *data base*, kwa hiyo ununuzi kama wa *software* nafikiri hapa ndio muhusika vile vile.

Mhe. Mwenyekiti, jengine sherehe za kitaifa. Hizi ni sherehe ambazo ni za watu wenye ulemavu, siku ya watu wenye ulemavu na hizi tunazifanya safari hii ziwe kubwa kuliko ile awamu iliyopita kwa sababu sherehe yoyote ambayo ina-*fall* kuanzia Julai ya mwaka huu inatakiwa kuambatanishwa pamoja na sherehe ya miaka 50 ya Mapinduzi. Kwa hivyo hii kidogo itakuwa ya aina yake kwa sababu ni moja katika sherehe ambazo ni za kusherehekea Mapinduzi yetu matukufu.

Mhe.Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru na namshukuru kwa utulivu wake Mhe. Waziri, naomba atuelewe tu kwamba tunafanya kazi yetu ya kusimamia fedha za walipa kodi wala hatuna nia ya kumsumbua mtu yeyote. Mhe. Mwenyekiti, nashukuru tu kwa maelezo yote ambayo kayatoa na yamenifurahisha. Ombi langu na ushauri tu kwa ofisi yake nafikiri keshaligundua mwenyewe tumekuwa tunampa tabu na pengine ingelikuwa masuala yote hayapo, ingelikuwa wamefanya *proper break down* kama walivyofanya wenzao kwa mfano tuliokuwa tumeshapitisha mpaka sasa ni Ofisi ya Makamu wa Pili, ofisi hii imetupa shida sana jinsi mafungu namna yalivyowekwa kuanzia hilo la mishahara tumelizungumza lakini hata haya.

Mhe. Waziri, maelezo yake juu ya fungu hili la vifaa vya *computer* kachanganya *photocopy*, kachanganya *data base*, kachanganya *printer*, lakini hivi vyote vinavyo vijifungu vyake katika buku hili hili katika maofisi mengine, chini ya fungu hili hili au kijifungu hichi hichi cha vifaa na huduma za ofisi. Sasa ingelikuwa haijafanywa ile sitaki kutumia lugha mbaya ya kuchanganyachanganya vikawekwa pamoja tu, pengine ingelikuwa kila moja limegawiwa chini ya kijifungu chake basi ingelikuwa hata hatuna masuali hapa, lakini kwa sababu hapa limejumuishwa pamoja ndio yakaja masuala haya.

Kifungu 2101 - Idara ya Watu wenye Ulemavu 396,782,000/=
Kifungu 2102

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Ahsante ndugu Mwenyekiti, kwa mara nyengine tena jana nilipokuwa nachangia nilikuwa ninaomba kupata ufafanuzi juu ya kifungu 211201 Kodi ya Nyumba. Mwaka jana nyumba hiyo

hiyo nafikiri ilikuwa imelipiwa 24,000,000/= lakini mwaka huu nyumba hiyo inatakiwa kulipiwa 98,000,000/= naomba ufafanuzi zaidi katika hilo.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, nilitoa maelezo lakini labda ndugu yangu Mahmoud alikuwa nje nitayatoa tena kwa faida yake vile vile kwamba safari hii hapa kumeingizwa pia gharama ya nyumba iliyokodiwa Pemba, lakini vile vile kuna nia ya kukodiwa nyumba Dar es Salaam Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais na ndio maana gharama hizi zinaonekana kubwa.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, hapa nilikuwa na hoja lakini nashukuru nyingi kazijibu vizuri katika majumuisho yake Mhe. Waziri, na kabla sijazungumzia nukta yangu mimi nataka niipongeze Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, kwa kuamua kumkodia Makamu wa Kwanza wa Rais, nyumba hasa kwa Dar es Salaam, kwa sababu moja ambalo lilikuwa likinikera sana kwamba kwanza kwa kiongozi hadhi yake kukaa hoteli tofauti na viongozi wenzake, lakini mimi najua kwa hadhi yake hoteli aliyokuwa akikaa ilikuwa ni gharama kubwa, sasa suala hili la kwenda kukodi nyumba sasa mimi nalipongeza nategemea litaokoa fedha za walipa kodi wetu wa Zanzibar.

Baada ya maelezo hayo Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikuwa nataka maelezo yale mengine ya gari, ya *generator* nimeridhika nayo, lakini ilikuwa bado sikuridhika na fungu lile la vifaa la huduma za ofisi, fungu liko ukurasa wa tisini na nne kifungu 220500.

Hapa Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa naomba nisaidiwe kwanza kuna hicho cha mwanzo hapo 220501 vifaa vya kuandikia, mwaka jana ilikuwa 3,243,000/= mwaka huu imekuwa 13,925,000/=. Kwa hivyo angetusaidia Mhe. Waziri, wame-*exprience* au wamepata uzoefu wa mapungufu gani katika mwaka uliopita katika masuala ya vifaa vya kuandikia hadi kuhitaji 13,925,000/= kwa mwaka huu, lakini hapo hapo kuna tena vifaa vya *computer*, *computer accessories* ni vifungu katika ofisi hii kila pahala vimeshona, mwaka jana ilikuwa milioni tatu laki tisa ishirini elfu mwaka huu ni ishirini na nne milioni laki tatu sabiini elfu. Najua ni Ofisi ya Faragha inahudumia bila ya shaka nyumba zote pengine za Makamu wa Kwanza na hizo mpya zinazotaka kukodiwa lakini hebu atukinaishe kwamba hizi zinakusudiwa kufanywa nini hasa. Kwa sababu kwamba ni ofisi kuna Idara ya Utumishi na Uendeshaji kule tumesha-*cover* kwa hivyo hapa kwenye ofisi ya faragha anataka kitu gani zaidi katika hili, naomba maelezo.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa maelezo yafuatayo. Katika fungu hili la

vifaa vya kuandikia shilingi milioni tatu laki mbili arubaini na tatu kwa mwaka jana, lakini kwa safari hii milioni kumi na tatu, Mhe. Mwenyekiti, hii ndio hali halisi. Kunakuwa na *advantage* kidogo kwa ofisi hii kwamba iko pamoja na Idara ya Uendeshaji na Mipango ndani ya nyumba moja, mara nyengine hapa kulikuwa na mapungufu ambayo yalijazwa na uendeshaji na utumishi hasa kwa sababu bajeti hii iliathirika sana kutokana na kukatwa kwa mikato ya manunuzi ya meli, lakini hayo ndio makisio halisi.

Mhe. Mwenyekiti, fungu la pili hili la vifaa vya computer nafikiri hapa nilieleza kwamba tunahitaji kuweka *editing bench* wanaita wenyewe wataalamu. Watu wa habari wanapofanya shughuli zao wanahitaji ku-*edit* kabla ya kupeleka kwa ajili ya kutoa zile taarifa hasa kwa viongozi hawa wakuu hutakiwi kwenda ku-*edit* katika sehemu za watu wengine kwenda kuomba, kwa hivi sasa hiyo *editing bench* haipo hapa ndani ya ofisi ya Makamu wa Kwanza.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, hili la kwanza nimeridhika nalo la *stationaries* na maelezo yake mazuri, hili la pili hebu naomba anisaidie kanichanganya zaidi. Kule mwanzo tulipohoji katika nadhani ilikuwa Idara ya Mipango na Sera ile, ilikuwepo fununu tukaambiwa kumetengwa fungu la kununua vifaa hivyo hivyo vya ku-*edit* kwa sababu ya ofisi ya Makamu wa kwanza wa Rais, na hapa maelezo ni yale yale. Kwa hivyo, nilikuwa nasema hebu tusaidiwe vipi matumizi yale yale yana vijifungu tofauti katika idara tofauti.

Hapa Idara ya Faragha nitakubali kwa sababu ndio pahala pale hasa na kusema kweli ukilinganisha na Ofisi ya Makamu wa Pili nililinganisha mimi kule kuna fungu kubwa zaidi katika huduma za mawasiliano, kwa maana ya kuimarisha ile ofisi inayoshughulika na mambo ya habari na kutoa habari za Makamu wa Kwanza wa Rais.

Kwa hivyo, nawapongeza kama wanafikia hivyo, lakini imekuwa tatizo kwamba kule mwanzo walitupa maelezo kama hayo kuwa katika Idara ya Mipango sijui na Utafiti maana sikumbuki, au ilikuwa ni Idara ya Utumishi na Uendeshaji. Kulikuwa na fungu ambalo liliulizwa akatwambia kwamba ni la kununulia vifaa vya *editing* vile vile kwa ajili ya shughuli za Makamu wa Kwanza. Sasa sitaki kuitaja kwa sababu siukumbuki ni ipi hasa, lakini hapa maneno yanajirejea hii naomba nisaidiwe kwamba ni wapi hasa fungu hili la vifungu vya *editing* lipo.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, naomba kumuweka sawa Mhe. Mwakilishi wangu wa Jimbo la Mji Mkongwe kwamba maelezo niliyoyatoa yalikuwa katika kifungu hiki na

ninayo hapa, ambayo niliyatoa pale yanahusiana na Ofisi ya Faragha. Hii ndio inayohusika katika kununua au kutayarisha hili *editing bench*. Niliyatoa katika kifungu hiki ambacho yeye anakiuliza. Lakini kwa sababu vifungu vinakuwa vingi sasa naona tunaanza kuvichanganya.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Inawezekana kabisa Mhe. Mwenyekiti, mimi ni binadamu. Kwa hivyo, nashukuru kwamba anasema aliyatoa alipokuwa anatoa majumuisho kama ni hivyo nakubali tuendelee Mhe. Mwenyekiti.

Kifungu 2102	Idara ya Faragha	515,150,000/-
Jumla ya Fungu		**3,020,000,000/-**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU 12 – TUME YA UKIMWI ZANZIBAR

Kifungu 0201 Utawala

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, nilisema jana katika mchango wangu kwamba napendekeza Baraza lilikubali kwamba tuongeze matumizi ya fedha za Tume ya Ukimwi kwa hoja kwamba (a) faida kubwa hatuioni mbele ya jamii na (b) fedha hizi kubwa zaidi kuliko zile fedha ambazo zimetengwa kwenye Idara ya Mazingira ambayo nchi nzima hii iko hatarini kuzama kutokana na uharibifu wa mazingira.

Kwa mfano Mhe. Mwenyekiti, fedha zote za Idara ya Mazingira ni shilingi 127 milioni, lakini Tume ya UKIMWI imetengewa shilingi 768 milioni, hiyo ni mishahara na kazi za kawaida. Bilioni 1.7 wahisani na milioni 50 kutoka serikalini. Kwa hivyo, Mhe. Waziri nikamuomba kwamba tupunguze basi fedha hizi za Tume ya UKIMWI ili tuzipeleke Idara ya Mazingira ili badala ya kuganga ile tume peke yake tuwaokoe na Wazanzibari kwenye hatari ya mazingira ambayo kila tukienda Zanzibar imekabiliwa na mmong'onyoko wa ardhi kutokana na upandaji wa bahari katika maeneo ya makaazi na kilimo ya wananchi.

Kwa hivyo, nilimuomba Mhe. Waziri tupunguze fedha hii nyingi badala ya kuwaachia fedha nyingi na kuandika mabango tu Kiwani UKIMWI, Kengeja UKIMWI, Makunduchi UKIMWI huku wananchi wanakabiliwa na athari ya mabadiliko ya hali ya hewa na mabadiliko ya hali ya nchi na kuzama kwa visiwa.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, nakuwa mgumu kidogo kukubali, nachelea sana yale yaliyowafika wenzetu Rwanda yasije yakatupata na sisi. Nimeelezea suala zima la UKIMWI lilivyo na hali yenyewe. Sasa nawaomba sana Waheshimiwa waniachie fungu hili liweze kutekeleza shughuli zake kwa mujibu wa mafungu yaliyopangwa.

Mhe. Mwenyekiti: Muelekeo unaonekana kama Wajumbe wana hoja kuwa iendelee hivyo. *(Makofi)*

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, sijaifahamu hali ya Rwanda ilivyotokezea na wananchi wangu wa Kiwani hawaijui hali ya Rwanda. Kwa hivyo, labda atwambie ili watu wa Kiwani waijue hali ya Rwanda ili tupate kuridhika, atuelimishe kidogo. Kwa sababu mimi nakaa Kusini ya Pemba kule Mashariki sijajua hali ya Rwanda.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, kilichotokea Rwanda walifanya kampeni kubwa na semina na makongamano na kuwaendea wanafunzi katika skuli na kutoa elimu hii mpaka ikashamiri. Na katika nchi ambazo zilikuwa na *prevalance* kubwa ya UKIMWI moja ilikuwa Rwanda, lakini baadae wakaona imepungua kidogo wakajipa moyo wakapumzika, wakapunguza fedha katika mapambano haya dhidi ya UKIMWI. Kilichotokea ilipanda tena kwa kasi kubwa. Mhe. Mwenyekiti, nachelea sana hili kuja kutokea hapa kwetu. Tayari tumeona imetoka 0.6 na kwenda 1.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Hija Hassan nadhani hapa uko sahihi, basi ngoja tuombe muda kidogo.

(Baraza lilirudia)

KUONGEZA MUDA WA BARAZA

Mhe. Spika: Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais shughuli yetu haijesha. Kwa hivyo tuombee utaratibu.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwa kuwa shughuli iliyo mbele yetu imebakia si muda mrefu sana tumalize, na kwa kuwa muda tulionao hautoshi kumalizika, kwa hivyo Mhe. Spika, ningeomba Baraza lako tukufu tuongeze muda usiozidi saa moja ili tumalize shughuli zetu. Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe niwahoji basi wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

KAMATI YA MATUMIZI

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Ismail Jussa kwa kifupi tumeidhinisha muda wa saa moja tu kwa hiyo kwa kifupi.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nikupongeze kwa kuhesabu kura haraka haraka, lakini pili Wawakilishi wenzangu kwamba hata hiyo saa moja aliyoiomba Mhe. Waziri *Inshaallah* hatuimalizi.

Mhe. Mwenyekiti, katika mchango wangu nilizuia shilingi juu ya fungu la Tume ya UKIMWI. Mhe. Mwenyekiti, nimesikiliza kwa kina na kwa utulivu majibu ya Mhe. Waziri juu ya hoja ambazo amezitoa. Na punde hivi nimesikiliza vile vile hoja zake akijibu hoja tena inafanana kidogo na yangu aliyoitoa Mhe. Hija Hassan. Mhe. Mwenyekiti, mimi bado sijashawishika na nawaomba wenzangu katika hili tufanye ile kazi ambayo wananchi wa Zanzibar wametuleta na wametuajiri, wanatulipa kwa sababu ya hilo ambalo ni kuzichunga fedha zao.

Mhe. Mwenyekiti, ili hoja yangu ieleweke, Tume ya UKIMWI hapa tunapopazungumza pana Utawala Unguja na Utawala Pemba jumla ni shilingi 768,000,000/-. Lakini tutapofika tutakuja kuona huko kwenye fungu la Maendeleo kuna shilingi 1,769,000,000/-. Ukizijumlisha hizo Mhe. Mwenyekiti ni sawa sawa na shilingi 2,537,000,000/-. Juzi Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais tulipokuwa tukizozana kuhusu vifungu hapa alikuwa na fungu la 52 milioni alitwambia kwa ajili ya kuratibu fedha ambazo zinahitajiwa kutoka katika *Global Fund* kwa suala hili hili.

Na shughuli zinaonesha kwamba kunategemewa ingawa haijathibitishwa US$ 11 milioni, zikiidhinishwa hizo maana yake ni haraka haraka tu, hazipungui shilingi 1,800,000,000/-. Nikijumlisha pale Mhe. Mwenyekiti, kwenye shilingi 2.5 bilioni maana yake hapa patakuwa na shilingi 4,337,000,000/- za kupambana na UKIMWI. Bila shaka za *Global Fund* nyengine zitakwenda katika Wizara ya Afya, lakini tunazungumzia Tume ya UKIMWI hapa.

Mhe. Mwenyekiti, mimi hoja yangu kwamba ungelikuwa fedha hizi tija yake inaonekana na mara nyingi nimesema, tatizo letu matumizi makubwa tunayoyaweka yanaingia katika kazi za kiofisi na za mezani kuliko kwenda kuhudumia watu. Tumesema hapa, makongamano, warsha, semina nyingi zinaishia kwa watendaji wa serikali ambao tayari uelewa wao ni mzuri kuliko wake watu wa chini.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, hoja yangu mimi katika kitabu hiki Mhe. Waziri katwambia mwenyewe kwenye ukurasa wa 42 kwamba, maambukizi ya UKIMWI Zanzibar yameongezeka kutoka asilimia 0.6 takwimu za mwaka 2007 hadi asilimia moja katika utafiti uliofanyika mwaka 2011/2012. Katika hotuba yake kitabu chake mwenyewe akaja akakikana anasema itabidi tutafute wataalamu watutafutie upya, mimi sitaki nataka hiyo aliyoniletea katika hotuba akawasilisha mbele ya Baraza hili Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, asilimia moja unaweza kuona ni ndogo sio ndogo, ukichukua kama ilikuwa 0.6 ikawa asilimia moja pana ongezeko la 0.4. Kwa hivyo, katika 0.6 kuongezeka 0.4 maana yake Mheshimiwa tumeongeza ile kasi ya kuambukiza kwa asilimia 66 kuliko ilivyokuwa pale mwanzo. Sasa hoja yangu Mhe. Mwenyekiti, nimalizie kwamba ikiwa fedha hizi ambazo kwa miaka kadhaa iliyopita zingekuwa kweli zinaleta tija iliyokusudiwa na zinafanya kazi ilivyokusudiwa, badala ya kuongezeka ingepunguza. Kwa miaka mingi tukijisifu kwamba kiwango kilichobakia asilimia 0.6 leo tunaambiwa imefikia asilimia moja Mheshimiwa hicho sio kiwango kidogo.

Sasa mimi nilikuwa nasema Mhe. Mwenyekiti, kwamba nina hoja mbili na ndio maana nimesimama hapa, maana zile za wafadhili hatuwezi kuzigusa, tutaziidhinisha kwa sababu tutaambiwa labda hoja nyingi watendaji kwamba hizi za wahisani inategemea na mradi ambao umepelekwa. Sasa zile zipo Mhe. Mwenyekiti, ambazo nimesema pale shilingi 1,769,000,000/-.

Mhe. Mwenyekiti, katika fedha zote siku zote katika mradi linakuweko fungu la kusimamia mradi vile vile na *management* ya bajeti. Kina Mhe. Mgeni Hassan Juma wameshafanya kazi hizo wanajua masuala hayo. Mhe. Mwenyekiti, nataka kutoa hoja kama nilivyozuia shilingi, kwamba fungu hili la fedha za utawala kwa Unguja na Pemba tulikate. Nataka kuwa *very specific* sipendekezi tukate mishahara kwanza mishahara yao hawawezi kutoa katika fedha za wafadhili, si kwa Unguja si kwa Pemba, hata zile gharama nyengine. Lakini ninachopendekeza mimi Mhe. Mwenyekiti, katika mia 768,000,000 narudia kusema zitakuja na nyengine US$ 11 milioni. Mimi nilikuwa napendekeza Mhe. Mwenyekiti, na wala sipendekezi kwamba ziende mbali katika ofisi hii hii ambapo kuna mambo tumeshaambiwa na nilisema pale mwanzo, mazingira, Idara ya Watu wenye Ulemavu fedha zimekatwa.

Mimi Mhe. Mwenyekiti, nataka kutoa pendekezo kwamba katika fungu la Utawala Unguja ambalo lina jumla ya shilingi 573,710,000/- tuache mishahara na maposho yake yote yale ambayo ni shilingi 200,401,000 na katika zile gharama za *OC* tuwaachie angalau, mimi nilikuwa napendekeza katika hapa kwamba katika shilingi 573,710,000/- tukate shilingi 200,000,000/- katika gharama za *OC.*

Kwa sababu kuna mradi kule unafanyiwa *arrangement* na nusu ya hizi zinafaa na ningekuwa na *resource* sichelei kupoteza muda wako Mhe. Mwenyekiti, na wa kamati hii ningetaja kifungu kimoja kimoja ambacho nahisi mafungu yake yamekuwa finyu sana. Ningependekeza katika Idara ile tukate shilingi 200 milioni na Pemba vile vile, ingawa hatujafika lakini *sub voucher* yangu moja naomba niseme kwa pamoja.

Halafu kuna shilingi 194 milioni katika hizo Mhe. Mwenyekiti, mishahara na maposho yao ni shilingi 53,526,000/-. Tunasema wapewe nyengine za kuhudumia shughuli zao, lakini hapo hapo pakatwe shilingi 70 milioni.

Napendekeza Mhe. Mwenyekiti, katika fungu hili la jumla shilingi 768 milioni tuzikate shilingi 270 milioni na Mhe. Mwenyekiti, napendekeza hizo tuzigawe kuna fungu na haya ni mafungu tofauti, zile *actual activities* Mhe. Mwenyekiti, katika Idara ya Watu wenye Ulemavu lile fungu ambalo linakwenda kwenye huduma ya walemavu mwaka jana lilikuwa shilingi 373,500,000/- mwaka huu limeshuka mpaka 258,020,000/-.

Tumesema hapa kwamba zinawezakuwa zimetajwa tunasema zimepungua hazikutosha sasa hivi tunazikata zaidi. Lakini katika Idara ya Mazingira kila mtu kapiga kelele hapa, ile shughuli yenyewe hasa ya uhifadhi inayoshughulikia mazingira ambayo niliisimamia wakati ule imepungua kutoka shilingi 49 milioni imekuwa shilingi 45 milioni.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile kuna fungu la Tume ya Kupambana na Dawa za Kulevya. Mimi napendekeza aniambie hizi shilingi 70 milioni tuzigawe. Shilingi milioni mia moja tuwapelekee mazingira, milioni mia moja tuwapelekee Idara ya Tume ya Walemavu na milioni sabini tuwapelekee Idara ya Tume ya Kupambana na Dawa za Kulevya. Fungu la UKIMWI naamini bado litafanya shughuli zake kwa sababu bado wanazo shilingi 1,700,000,000 zilizokuwa zimetengwa kutoka kwa wafadhili na bado tutakuta tunawabakishia takriban zaidi kidogo ya nusu ya fedha hizi walizokuwa wameziomba wakafanya shughuli za usimamizi.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja hiyo na naomba wezangu waniunge mkono na Waziri aniunge mkono katika hili ili fedha za walipakodi wa

Zanzibar zikafanye huduma muhimu zaidi katika ofisi hii ya Makamu wa Kwanza wa Rais. Mhe. Mwenyekiti naomba kutoa hoja.

UTARATIBU

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, kwa kawaida huwa sitofautiani sana na Mhe. Ismail Jussa, lakini nilikuwa nataka nisaidie kitu kimoja. Mhe. Mwenyekiti, mimi kwa bahati hiki ni kipindi cha pili naendelea katika Kamati hii ambayo inashughulika na masuala ya UKIMWI.

Mhe. Mwenyekiti, tulipokuwa katika ziara zetu za kamati tulikutana na hao wenzetu wa *ZAPHA*$^{+}$ na wao kimoja walichokuwa wakitusikitikia kwamba sasa hivi wahisani wameanza kupunguza fedha kwa ajili ya kusaidia kufanya zile *activities* zao. Walitupa angalizo wakatwambia Waheshimiwa tunaomba sana muiambie serikali watafute namna yoyote kutafuta fedha ili kuweza kutusaidia kuwafikia wale waathirika kule chini ili tuweze kuwahudumia. Kwa sababu tukiweza kuwaacha wale maradhi haya yatakuja kuongezeka.

Mhe. Mwenyekiti, hili mpaka katika ripoti ya kamati yetu kila mwaka linajitokeza kwamba serikali watafute pesa sehemu yoyote ili kuziba lile pengo la wafadhili. Sasa mimi naomba Mhe. Mwenyekiti, kama fedha hizi moja kwa moja zinatumika kwenye utawala mimi ni mdau mkubwa sana wa mazingira, ni mdau mkubwa sana wa Watu wenye Ulemavu, lakini bado suala la UKIMWI Mhe. Mwenyekiti, huku kunahitajika fedha ili kuweza kuwasaidia wale wenzetu kwenda kutoa huduma. Kwa sababu wale waathirika wa ugonjwa wa UKIMWI Mhe. Mwenyekiti, wanahitaji huduma na mazingira maalum sio mtu yeyote tu anayeweza kutoa huduma.

Sasa mimi naomba fungu hili, na mimi kwa kuwa ni Mwenyekiti Mhe. Jussa mimi naomba sana unikubalie, leo nakuomba sana napiga magoti. Mhe. Mwenyekiti, naomba fedha hizi tuziangalie katika matumizi ya utawala, na kama itakuwa ni nyingi katika matumizi ya utawala ziende bado katika eneo lile lile la UKIMWI kuwasaidia wale *ZAPHA*$^{+}$ waweze kutoa huduma vijijini.

Mhe. Mwenyekiti, pale Chake Chake waliweza kufungua mpaka ofisi pale na ofisi yao wananchi tena sio ofisi ya serikali ni *ZAPHA*$^{+}$ wananchi wanakwenda pale wanatoa damu wanapata ushauri nasaha, waliopata maambukizo wanawafuata mpaka majumbani, ambapo wazazi wao au familia zao zinawanyanyapaa wale wanakwenda kuwahudumia. Sasa Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba fungu hili katika maeneo ya UKIMWI, Mheshimiwa UKIMWI ni hatari tena ni maradhi hatari sana. Tukipunguza fungu hili Mheshimiwa hiyo moja iliyofika sasa hivi kutoka 0.6 mpaka kuja moja itakuja kuwa mbili na ikiwa mbili hapa kila mtu atakimbia hapakaliki.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, mimi namuomba sana Mhe. Jussa tukubalie fungu hili tukae na wizara na ikiwezekana na yeye tutamualika, tuelekezane namna gani ya kufanya matumizi yake, kama fedha zitakuwa za ziada basi wapelekewe wale Jumuiya ya *ZAPHA*$^{+}$ Unguja na Pemba ili kuweza kufika kwa walengwa vijijini kwa kuweza kutoa huduma.

Mhe. Jussa nakuomba sana nikubalie hilo, wala msije mkanambia aa, sasa hivi keshakuwa kule aa, hapa tunatengeneza maisha ya wananchi wetu. Pahala pa kuisaidia serikali tutaisaidia na pahala pa kuwasaidia wananchi tutawasaidia. Mhe. Mwenyekiti, namuomba sana Mhe. Jussa katika hili.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri tumesikia maelezo ya pande zote mbili, tumemsikia Mhe. Hija Hassan, tumemsikia Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, naomba Mhe. Jussa akubaliane na Mwenyekiti wa Kamati ile ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa sababu anaelewa haya. Lakini labda kuamua fedha ziende wapi nafikiri tufanye kitu kimoja kinaweza kuwa busara zaidi kuliko kutoa maamuzi ya haraka. Tukae sisi ofisi yetu kwa maana ya Tume ya UKIMWI na Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais pamoja na kamati hii nzima tumualike na Mhe. Jussa, tupitie mafungu yetu yote na tukiona kile ambacho tunaweza kukipunguza bila ya kuathiri shughuli hizi na utekelezaji mwengine.

Sasa kwa sababu nachelea kidogo kwamba *ZAPHA*$^{+}$ tumewawezesha wao wenyewe kwa mwaka huu wameweza ku *solicit fund* zaidi ya shilingi milioni mia tano kwa ajili ya shughuli zao. Basi labda hicho kitakachozidi tukipeleke katika mafungu yetu mengine kiweze kusaidia. Lakini kwa kadri pia kamati na maamuzi tutakayokubaliana hapo, sina tatizo sana na hilo. Namuomba Mhe. Jussa atukubalie katika hili.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, ilikuwa nimwambie Mhe. Hamza Hassan rafiki yangu nilikuwa sina taarifa kwamba leo kateuliwa kuwa Waziri na ni Mjumbe wa Baraza la Mapinduzi, anatetea serikali na anajibu hoja zetu katika Baraza hili. Nimuombe tu kwamba asituharibie utaratibu wa Baraza hili Mhe. Mwenyekiti. Kwa sababu yeye ndio kioo chetu, akichukua jukumu yeye la kuwa mtetezi kitapokuja kumgeukia yeye sasa atakuja kupata tabu sana ndani ya Baraza hili. Na hasa kwa sababu wakati mwingi vilipokuwa vikipitishwa vifungu hivi yeye alikuwa safarini. Sasa Mhe. Mwenyekiti, namheshimu sana kaka yangu Mhe. Hamza lakini nachelea kuja kumpa tuhuma ambazo yeye si zake atapokuja kutetea vifungu kama hivyo. Naunganisha hoja yangu Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, nimesema mwanzo na wenzangu wanakuwa waoga wanaona labda nafanya ushindani tu, lakini mimi nilipokuja kuomba kuingia katika Baraza hili niliwaahidi wananchi nakwenda kufanya kazi na nilikataa kuwa sehemu ya serikali. Mara nyingi mlikuwa mkisema hili nifanye kazi ya kuwasimamia na kuwatetea wananchi maslahi yao.

Mhe. Mwenyekiti, muongozo tulipewa huu mapema sana, Mhe. Hamza mmoja katika watetezi wakubwa yumo. Katika sheria hiyo Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha *Public Finance Act* kuna kifungu cha 17(b) naomba nikisome Mheshimiwa ili ufahamike msingi wa hoja yangu ni nini. Mimi sijakataa, katika shilingi bilioni mbili laki tano zikipunguzwa shilingi 270 milioni zitawafanya nini, zitafanya nini Mhe. Mwenyekiti humu ndani.

Kifungu cha 17(1) cha *Public Finance Act* kinasema kwamba:

> *"Subject to Article 106 of The Constitution, the Minister shall cause to be prepared and tabled before the House of Representatives as soon as practicable before the commencement of each financial year"*

Kifungu cha 17(1)(b) kinasema kwamba:

> *"For each vote of expenditure a statement of the classes of out puts expected to be provided from that vote during the year and the performance criteria to be met in providing those outputs".*

Mhe. Mwenyekiti, na *underline* neno *outputs* ndio msingi wa hoja yangu. *Output* ya Waziri kwamba kuingiziwe mabilioni kila siku badala ya UKIMWI kupungua unaongezeka Zanzibar, pamoja na yote hayo aliyosema Mhe. Hamza.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nawapenda Wazanzibari vile vile na naamini kama niko katika UKIMWI tunapiga kelele sote na Mhe. Hamza mmoja katika wapigaji kelele wakubwa sana wa mazingira, aliwahi ku *walk out* tulipokuwa tukipitisha *vote* mwaka juzi hapa kwa kujua na jinsi kutuonesha yanavyokwenda mazingira, leo namshangaa! Kuwa mimi nataka kuhamisha mafungu ya utawala yanayotafunwa yeye atahudumia mazingira na watu wenye ulemavu na dawa za kulevya ikawa yeye asimame atetee kwengine.

Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, naomba tena Baraza hili kwamba hatuathiri chochote katika hayo mapendekezo, hofu yangu nimekubali pendekezo lililotolewa, lakini Mheshimiwa hapa tunapoweka rekodi fedha zinatutisha. Mimi sina tatizo naijua hii ni demokrasia Baraza likiamua vyenginevyo nitaheshimu, nitakaa katika rekodi mbele ya Wananchi wa Zanzibar kwamba

nilikataa ubadhirifu wa fedha, niliwatetea walemavu, niliwatetea mazingira, nilitetea dawa za kulevya sijakubali kutia ulimi puani Mhe. Mwenyekiti.

Kwa hivyo, nasema pendekezo lililokuja ni zuri lakini rekodi yake iko wapi? Kwamba tukakae pembeni, tukikaa pembeni tunapitisha mafungu yaliyokuwa yameletwa hapa haya, tukakae katika kikao halafu tukaamue msingi wake utakuwa nini Mhe. Mwenyekiti. Kamati ya kupitisha maamuzi ni hii hapa sasa hivi.

Bado nawaomba wenzangu, wananchi wa Zanzibar wanatuangalia, wanatupima kauli zetu na vitendo vyetu Mhe. Mwenyekiti, lazima wajue tunawasimamia kiasi gani. Naomba sana tukate 270,000,000 katika fungu la utawala kwenye Tume ya UKIMWI tupeleke zikaongeze mapambano katika mazingira, dawa za kulevya na walemavu ili huduma hizi zote katika Ofisi ya Makamu wa Kwanza ziweze kufanya shughuli zilizokusudiwa. Naomba Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimshukuru sana ndugu yangu Mhe. Jussa kwa namna ambavyo siku zote anavyotetea haki ili tufanye maamuzi mazuri. Amekuwa mstari wa mbele kutetea mazingira ya walemavu na hata hili la UKIMWI alilizungumzia kwa msingi ule ule nalo janga hili analijua uzito wake. Nataka nimshukuru sana mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa na Mhe. Waziri.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa kamati hii waliyazungumzia mambo haya na wakayaona uzito wake na ndio maana awali wakayapitisha, na kwa sababu tumezungumza sana na wizara na wakatoa ufafanuzi sana kuhusiana na fungu hili, na tusingependa kabisa tuje mahala ambapo tuvutane wakati sote tunatetea haki, tunatetea umuhimu wa kutazama sekta zetu kubwa tatu hizi; Sekta ya Mazingira, Sekta ya ndugu zetu Walemavu na tatizo la kupambana na janga hili la UKIMWI. Na ushauri uliotolewa na Waziri ulikuwa ushauri mzuri ambao kwa kiasi fulani ungetusaidia.

Vile vile nikubaliane na Mhe. Jussa kwamba tunapoondoka kwenye Kamati hii tayari inakuwa tumeshafanya maamuzi. Lakini mimi niiombe kamati yako hii kwa kuwa sote tuna nia njema na kwa sababu kamati inaweza kupitia pamoja na wizara husika.

Kwa hivyo, tuzidi kumuomba Mhe. Ismail Jussa Ladhu unajua jambo ambalo amelisema lina nguvu yake ya hoja. Lakini nimuombe Mhe. Ismail Jussa Ladhu twende tukae pamoja tupitie ili tujue kina cha mahitaji yao pengine

tukipunguza tunaweza tukaathiri pia katika suala zima la kupambana na Ukimwi.

Kwa hivyo, tutakapokwenda kukaa kwa pamoja tukalipia hili kwa kamati kwa kina sana na idhini ikatoka kwa kamati yako hii ili hayo yatakayokubalika kwenye kamati yaweze kuwa ni uamuzi uliofanywa na Kamati hii Mhe. Mwenyekiti.

Kwa hiyo, naomba Mhe. Ismail Jussa Ladhu atukubalie tukakae pamoja tulipitie kwa kina na kama kuna aina yoyote ya kufanya marekebisho basi kamati hii irudie ikafanye kazi hiyo Mhe. Mwenyekiti. Naomba sana Mhe. Ismail Jussa Ladhu tustahamilie tutafanye marekebisho. Ahsante sana.

Mhe.Mwenyekiti: Waheshimiwa zingatieni yote yaliyozungumzwa kwa sababu yote yana umuhimu. Mazingira yana umuhimu, watu wenye ulemavu wana umuhimu, kupambana na dawa za kulevya kuna umuhimu mkubwa na suala la Ukimwi kuna umuhimu wa pekee. Sasa yote hayo tuyaangalie na mchango wa Mhe. Waziri tuzingatie.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, wewe shahidi mzee wangu. Kwamba katika Mjumbe wako ambaye hana sifa ya ukaidi katika Baraza hili ni mimi. Kifungu si cha kwanza hapa lakini nikipewa maelezo ya kina na ya kuridhisha, sote wa kwanza mimi muungwana nikasema tuendele. Na wenzangu wanajua hapa wanawashawishi wao hapa kimya kimya ikiwa ni maelezo ya kuridhisha.

Sina zaidi Mhe. Mwenyekiti, lakini nataka tukubaliane jambo moja tuendelee. Mimi sioni tabu Mhe. Mwenyekiti, hata nikitundikwa peke yangu hata sishughuliki na historia itaniandika, kwa hivyo, hata sishughuliki mimi kama kuna makosa japo Baraza zima hili nitakaa pekee yangu iko siku historia itaniandika. Lakini si malengo nataka nilikubali pendekezo alilotoa Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais na akalieleza kwa uungwana kabisa. Nataka nimpongeze sana kabisa Mhe. Waziri huyu katika mawaziri waungwana ndani ya Baraza hili mmoja ni yeye. Siku zote anaelewa hisia zetu, amekuwa msikivu siku zote anajua uwiano baina wanayohitajia Wawakilishi na Mawaziri.

Lakini sitaki maneno matupu nataka Mhe. Mwenyekiti, kama tunakubaliana tuweke kwenye rikodi kwamba tunapitisha *subject to*, tunapitisha zile rikodi kwa sharti kwamba tunakwenda kukaa kunazungumzwa na ikiwa hoja niliyotoa ni sahihi au haina maelezo ya kina, mimi nilipendekeza ichukuliwe tu ile ambayo inakwenda kufanyiwa kazi na kamati ambayo imepangwa.

Moja Mhe. Mwenyekiti, nimesema bahati mbaya lile fungu kubwa hasa ambalo mimi naamini ndiko kunakotafunwa pesa hasa huko za wasajili. Mhe. Mwenyekiti niseme hii dhana hii aiondoe ya watendaji kwamba fedha zikiwa za msaada maana yake si fedha za Wazanzibari hatupaswi kuzihoji sisi?

Fedha hizi zinakuja mchango kwa wananchi wa Zanzibar si kwa watendaji wakatafuna wao. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti nalikubali pendekezo lililotolewa. Kwa masharti niliyoyasema kwamba tunakwenda kukaa na ikiwa hoja zangu nilizotoa za msingi na imeshindwa kuleta hoja zao. Kwamba lile nililolipendekeza ndilo litakalosimama.

Pili Mhe. Mwenyekiti, mimi nimuombe hapo hapo linafuatana na hili kwa ujumla wake kupitia kamati yako Mhe. Mwenyekiti, ya *PAC*. Lakini pia kupitia kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Mhe. Mwenyekiti, *Public Finance Act* ndio muongozo wetu. Kifungu cha 26(6) kinasema:

Subject to any duty imposed on him by any written law the Controller and Auditor General shall have complete discretion in the discharge of his functions and, in particular, in determining whether to carry out any such examination he shall take into account any proposals made by the Public Accounts Committee, the Local Authorities Accounts Committee and any other Committee of the House of Representatives.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mujibu wa kanuni zetu hizi. Kanuni ya 104 kamati ya Baraza zima ni miongoni mwa kamati za Baraza. Naomba tuagizie kwamba hapa Mhe. Mwenyekiti, *CAG* akafanye *special Audit* ya shughuli zote za Tume ya ukimwi na fedha zao ambazo wameziwasilisha, na *PAC* ifuatilie halafu ije itulee, hili ni jasho la walipa kodi.

Mhe. Mwenyekiti, nakubali kwa kuwa umeniomba na nakuheshimu sana Mhe. Waziri mwenyewe wa Sekta na Kiongozi Mratibu katika Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais nakubali tukakae tulipitie. Lakini nasema kuwa hoja kwamba ikiwa hoja zangu za msingi asilimia gani itakatwa na itakwenda katika shughuli ambazo nimependeleza. Tukikubaliana Mhe. Mwenyekiti, sina tatizo nitasema tuendelee. Ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Sawa mimi nafikiri tumefikia pahala pazuri. Kamati ikae na Mhe. Waziri, Mhe. Ismail Jussa Ladhu utakuwemo kwenye kamati hiyo ili tufikie pahala lile ambalo tutaafikiana na naomba kamati hii ya *Supply* ifanye hiyo kazi kwamba fungu hili linapitishwa *subject to* maamuzi ya kamati ambayo itafanya kazi hii, hilo moja.

Lakini la pili chombo hiki kina nafasi ya kuweza kutoa maelekezo kwa Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Pale ambapo pana jambo lina wasi wasi aweze kupitia mahesabu hayo na atakuwa anaweza kutoa taarifa kwa utaratibu kama kawaida.

Kwa hiyo, sasa nikubaliane kwa kuwahoji Waheshimiwa Wajumbe sasa hapo....

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe. Mwenyekiti, kabla hujatuhoji. Mhe. Mwenyekiti, hii *subject* ambayo Mhe. Ismail Jussa Ladhu ameileza pa kuzipeleka fedha hizo. Katika maeneo ya mazingira bado nna hoja juu ya eneo hilo. Na kwa sababu kwenye sehemu ya mradi katika maeneo haya ya mazingira kuna hoja juu ya fedha ambazo zimo humu na matumizi yake. Kwa hivyo, nahofia tusije kupitisha hoja juu ya *subject* aliyoitoa na mimi nna hoja juu yake katika Idara hii ya Mazingira juu ya fedha ambazo zipo katika miradi na matumizi ya fedha hizo katika miradi.

Mhe. Mwenyekiti: Hapa kuna maeneo mengi kuna sehemu ya Dawa za Kulevya, kuna sehemu ya mazingira ameyataja Mhe. Hamza Hassan Juma, kuna sehemu ya watu wenye Ulemavu. Lakini Mhe. Hamza Hassan Juma anasema tuangalie sana tusije tukageuza fedha zile 0.1 ikaja kupanda ika`wa 0.2. Sasa nataka niombe Kamati hii ya Matumizi ifanye kazi hiyo na Mhe. Ismail Jussa Ladhu akishiriki ili iangalie maeneo hayo na kufikia makubaliano ya maamuzi yale ya Muhusika. Ili maamuzi hayo sasa ndio yatakuwa maamuzi ya Kamati hii ya Matumzi juu ya mgawanyo wa fedha hizo kwenda katika hayo maeneo yote muhimu tuliyoyasema hapa. Maana yote ni muhimu pamoja na hili ambalo Mhe. Salmin Awadh umelizungumza au sijui labda sijakufahamu.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Ismail Jussa Ladhu ameonesha ni maeneo ya mazingira kwamba pesa zipelekwe katika sehemu ya mazingira.

Sasa mimi nna hoja sijafika hapa katika maeneo ambayo nataka kuhoji juu ya fedha milioni mia nane ambazo zitatumika katika maeneo ya mazingira. Sasa hofu yangu tusije kupitisha hoja wakati mimi nna hoja haijafika hapa juu ya matumizi ya Fedha ambazo zinakwenda katika maeneo ya mazingira. Sasa mimi natahadharisha kabisa kwa sababu mimi hoja yangu haijafika. Tusije tukapitisha *subject* ambayo Mhe. Ismail Jussa Ladhu ameiomba ziende mazingira. Lakini mimi nna hoja juu ya maeneo ya mazingira.

Lakini maeneo mengine sina matatizo. Na kwa sababu kuna fungu la fedha ambalo linahitaji kulieleza Mhe. Waziri anipe ufafanuzi katika maeneo ya

matumizi ya mazingira ambapo Mhe. Ismail Jussa Ladhu ameelekeza zipelekwe kule. Sasa tukikubaliana na hilo maana yake tayari Kamati imeshapitisha maamuzi. Kwa hivyo, hoja yangu itakuwa haina mashiko. Sasa hapo ndio nilipokuwa nataka kupatahadharisha juu ya hilo eneo moja la mazingira ambalo Mhe. Ismail Jussa Ladhu amesema tuzipeleke na hapa tunataka kupitisha maamuzi.

Mhe. Mwenyekiti: Hilo ni angalizo na pia tuzingatie na hoja utayoitoa juu ya hilo.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, ili nifahamike nadhani tumezungumzia vitu viwili tofauti. Sasa itapokaa kamati na Wajumbe itapata kupitia kwa kina kuliko katika utaratibu huu. Lakini mimi nilipanga kwamba katika ule ukurasa wa 89 pana fungu pale la uhifadhi na usimamizi wa mazingira hii ni katika pesa za *OC* ambazo Serikali ina jukumu. Tukasema haya mambo mengi ambayo wameyapigia kelele yanashindwa kutekelezwa kwa sababu fedha ni kidogo na bado zimepunguzwa kutoka mwaka jana.

Mhe. Mwenyekiti, nafikiri Mhe. Rufai Said Rufai alipokuwa akichangia aliipongeza Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais katika suala la mradi ambao unafanywa katika Jimbo lake. Nilikuwa namwambia Mhe. Mohammed Aboud Mohammed pembeni itabidi wakate katika mafungu yao ili kufanikisha mafungu ya mradi ule. Kwa hiyo tuseme katika *OC* imerekebishika.

Sasa lile la Maendeleo akifika na yeye atakuwa na haki ya kuhoji na kama fedha za mradi zitakuwa na malengo mahsusi na si peke yake kama mimi nilivyozifunga za Ukimwi. Kwa hivyo nahisi, kama na hili litakuwa makini basi na mimi nitamuunga mkono katika hilo.

Lakini zile za jumla za shughuli za *OC* katika Idara ya Mazingira kufuatilia yale mambo ambayo mmoja mmoja katika sisi kayapigia kelele hapa kila mmoja katika jimbo jinsi alivyokuwa anashindwa kuyasimamia kwa sababu ya hoja ya Bajeti. Nikasema hizi sehemu yake tumekubaliana huko ziende kule.
Lakini za maendeleo hata mimi aseme hoja yake na ikiwa ya msingi nitamuunga mkono Mhe. Mwenyekiti, ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Nafikiri tumefikia pahala. Sasa basi Waheshimiwa Wajumbe naomba nirudie kwamba Kamati hii ya Matumizi itoe kazi kwa Kamati ya kusimamia Ofisi zaViongozi Wakuu wa Kitaifa juu ya fedha hizi ambazo zimehojiwa hapa Mhe. Waziri wakae pamoja Mhe. Ismail Jussa Ladhu ashiriki kwenye shughuli hiyo ili kuzingatia maeneo yaliyotajwa

yakiwa ni masuala ya watu wenye ulemavu, masuala ya mapambano ya dawa za kulevya pia suala hilo linatokana na mapambano ya ukimwi nalo litakuwemo likizingatiwa pia na masuala ya mazingira. Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati hii naomba mridhie hilo. Lakini kule kuna mkono wa Mhe. Waziri wa Afya.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi na wala sipingi maamuzi ya kamati hii naomba kutahadharisha tu kwamba haya tuliyonayo huduma za Ukimwi zinahudumiwa na wageni. Sisi tumekuwa tunatia kidogo sana na ni moja katika sehemu tunayolaumiwa kwamba huduma hizi tunawaachia *Donors* na kwa taarifa ya Baraza hili wengi wao 2014 wanafunga virago.

Sasa kama hatutojibeba na sisi kuna hatari ya mambo haya kuwa magumu. Na mimi ninachokifahamu kwamba Ukimwi hauongezeki tu kwa fungu la pesa. Kuna sababu nyengine nyingi zilizo nje ya pesa zinazosababisha Ukimwi.

Kwa hivyo, na mimi nilitaka kuweka rikodi tu kwamba tuwe na hadhari kwamba fungu la Ukimwi maisha yote tunasaidiwa na *Donors* na sisi tumekuwa tunatoa kidogo tu. Kwa hivyo, mimi sizioni kwamba pesa hizi ni nyingi kustahiki kugawa mafungu mengine. Lakini sina pingamizi na maamuzi ya Kamati. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Tumefikia pahala kwamba mambo yote haya yazingatiwe, kuliko kuja kuondoa halafu tukakuta *deficit* kubwa, sasa baada ya kupungua huo ukimwi ukatandaa zaidi. Naomba sasa Waheshimiwa wana Kamati hii Waheshimiwa Wajumbe turidhie kazi hiyo kuipa kamati kama tulivyosema.

UTARATIBU

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, maamuzi yako yanaelekea kwamba yanakwenda vizuri. Lakini mimi napenda nitahadharishe tunapokubaliana kwa hilo suala ambalo unataka kuuliza na ukanyanyua mikono sote tutakubali, kinachofuata ni kitu gani kwa sababu hapa Kamati ya Matumizi ndiyo inayoidhinisha Bajeti ya Wizara.

Sasa tukikubaliana kwamba tuakhirishe hii ili ikazungumzwe *subject to* itakuwa kamati hii sasa hatuwezi kuidhinisha Ofisi ya Makamu wa Kwanza kwa sababu bado kutakuwa kuna pungufu. Sasa hilo ni suala moja inabidi tulitizame kiutaratibu na kikanuni.

Ninavyofikiria mimi Mhe. Mwenyekiti, hii tunawaza tukai- *suspend* kwamba tunafanya hiyo kamati ya matumizi haya hatuyapitishi kwa sababu Mhe. Ismail Jussa amesema ni *subject to*. *Subject to* ninavyofahamu mimi ni suala kubwa sana ni *subject to* na hayo makubaliano, *suppose* hayo makubaliano hatujakubaliana *what happen* kwa Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais tutasimama kama hatukukubaliana. Sasa tunakwenda nje ya kanuni kidogo.

Sasa mimi ninavyofikiria sikatai maamuzi yako, maamuzi yako mazuri na Wajumbe tunaweza tutakubaliana kwamba tunakubali kwamba hiyo kamati ya Viongozi Wakuu pamoja na Mhe. Ismail Jussa Ladhu na Mhe. Waziri wakae halafu wakishakubaliana waje hapa na sisi kamati tukubali. Kwa sababu hatuwezi ku- *delegate* sisi kwa kamati hiyo. Sisi lazima tukubali wananchi wanaweza kuamua hawa, sisemi kwamba wanaweza kuamua maamuzi yaliyokuwa sio. Lakini wanaweza kuamua maamuzi ambayo si mazuri au yatakuwa matatizo au yatakuwa yana matatizo na bajeti hii. Sasa hiyo italeta matatizo baadae.

Kwa ushauri wangu mimi Mhe. Mwenyekiti, tukubaliane kwa hiyo kamati kukutana na Waziri pamoja na Mhe. Ismail Jussa Ladhu bajeti hii tunai- *suspend* kwa sababu kama alivyosema Mhe. Salmin Awadh kuna mambo mengine ambayo na yeye ataongeza.

Kwa hivyo, je, tutaipitisha bajeti hii nusu tuisubiri hiyo *subject to* au tunaipitisha yote? Utaratibu kwamba tunaipitisha yote kama kifungu cha 98 kinavyosema kamati ya matumizi haina *delegation*, hakuna *delegation of power* kwa kamati ya matumizi. Sote lazima tufanye hivyo. Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa turidhie Kamati ikafanye kazi na irejeshe taarifa hiyo kwa kamati ya matumizi baadae. Sasa shughuli hii mimi nafikiri inafanyika kwa siku moja.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mimi nadhani tuangalie hoja zote zilizotoka pande zote. Na mara nyingi hutokezea katika Mabunge zikitoka hoja kama hizi Bunge huakhirishwa kidogo ili kuzipa nafasi kamati kwenda kujadili na baadae kuendelea. Kwa hivyo, hili lisiathiri shughuli zetu hizi mimi natoa rai kwamba tukubali tuakhirishe shughuli ili kamati kama ni usiku huu kama ni alfajiri yake kesho wakae ili Baraza lirudi ndio tuje tuendelee kama watakavyokubaliana katika Kamati.

Mhe. Mwenyekiti: Mimi shida yangu ni moja hii ni *issue* inayohusiana na fedha ambazo zimekasimiwa kutumika kwa ajili ya mapambano ya Ukimwi.

Kuna maeneo mengine hatujayamaliza. Sasa maeneo mengine mimi naona tuyamalize kazi hiyo ifanywe halafu tuta- *suspend* kama vile alivyosema Mhe. Waziri wa Sheria na Katiba, ili sasa tutaporudi ndio hiyo nilikuwa najaribu kuweka muda ili kazi hii tuipate kesho.

Nilikuwa nazingatia kwamba kazi hii tuimalize kesho kabla ya kuakhirisha kikao cha asubuhi. Maana nilikuwa najaribu kuona kama tunaweza kuifanya mara baada ya maswali na majibu. Lakini kuondoka usiku huu na asubuhi tutakutana saa ngapi ili asubuhi tuwe tumeshapata majibu. Kwa hiyo, tuifanye kabla ya kuakhirisha kikao kesho kipindi cha asubuhi. Kama pale kwenye saa saba tuimalize kazi hiyo halafu tena tuendelee.

Kwa hivyo, kazi ile tumeipa kamati ya kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu ikimshirikisha Mhe. Ismail Jussa Ladhu, Mhe. Waziri ndio mwenyewe kabisa na Waziri wa Afya na yeye ametoa angalizo kubwa na muhimu, sehemu kubwa ya mambo ya Ukimwi yako kwake.

Sasa kwa pamoja tukae shughuli hiyo tuifanye. Muda mtakaokaa kama mpaka ikifika saa saba pale shughuli hiyo imemalizika na mtoe taarifa ili tukamilishe kazi hiyo. Nadhani tumekubaliana hilo.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, nina ombi kama nimekusikia uzuri unasema baada ya kwenda kukaa kamati kama tulivyokubaliana, na kwa sababu ya hoja iliyotolewa na Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria pengine shughuli hii ya kumaliza tungeifanya saa saba.

Mimi ombi langu ni kwamba shughuli hii tungeifanya kabla ya kuakhirisha kikao cha asubuhi kesho, kwa sababu kikao kinaakhirishwa saa saba na saa saba ni wakati wetu wa mapumziko kurudi saa kumi na moja. Kufanya kikao saa saba maana yake tutaunganisha vikao hivi vya Baraza. Tufanye kazi hii wakati wa kikao cha asubuhi na isiwe saa saba.

Mhe. Mwenyekiti: Nadhani tumekubaliana kwamba kabla ya kuakhirisha kikao mchana kazi hii tupate taarifa na kumaliza. Kwa hivyo, tunaiachia kamati ifanye kazi hiyo.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikuwa nina ushauri mdogo tu kama utakubalika. Kwa sababu hii kazi si ndogo kama tunavyofikiria hawa tuliowateua itabidi wakae hivi sasa, pengine na asubuhi.

Kwa hivyo, mimi ninachofikiria na ninachopendekeza ni kwamba asubuhi tunapokwenda kwenye *Order paper* yetu kama kawaida maswali na baada ya

maswali kazi iliopo ni Mhe. Waziri kusoma hotuba yake akishamaliza hotuba yake kama ipo *time* basi pale tunaingia katika suala hili.

Lakini kama kwa mfano tumefika saa saba kwa hivyo hii imalizwe jioni yaani ije baada ya hotuba ya Mheshimiwa Waziri kusomwa. Kwa hivyo, na wale asubuhi watapata *time*, na kuna *time* ya ku-*print* na kuna *time* ya kufanya mambo chungu nzima, kwa sababu Wajumbe wote lazima tupate hiyo. Sasa tukifanya asubuhi mapema kidogo nahisi tutakuwa tumewabana sana, ile mantiki tutaikosa hatutaipata.

Kwa hivyo, mimi napendelea ombi langu ni kwamba baada ya Mhe. Waziri kusoma hotuba yake kesho halafu pale ikimaliza kabla ya mchango wake tunamaliza suala hili halafu tunaendelea na mchango wa Mhe. Waziri.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa rai na ombi tunalionaje. Mimi nafikiri hizi shughuli ni zetu na tunategemea zote tuzimalize kwa ufanisi. Asubuhi acha tuendelee na shughuli yetu kama kawaida kama *Order paper* itakavyoonesha maswali na majibu, acha Waziri asome tutaangalia kama kuna muda wa kutosha hata Mwenyekiti wa Kamati anaweza akatoa hotuba yake na baada ya hapo tutatizama muda ulivyo. Lakini tunakubaliana kwamba kamati ifanye kazi hii nadhani hapo ni sawa. Kwa hiyo tuendelee na sehemu iliyobaki hili tumeli-*suspend* kwa ajili hiyo.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima na taadhima naomba utumie busara zako uliakhirishe Baraza hili hadi kesho asubuhi tuweze kuendelea. Kwa hiyo, nafasi iliyobakia kwa sasa tuiache mpaka hatua hii itakapokamilika halafu tutakuja kuendelea na mambo mengine. Naomba tumia busara zako Mhe. Mwenyekiti. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti: Labda Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa anazingatia ule muda tulioukasimu. Maana tulijifunga na saa moja ambayo bado ni kama dakika kumi kufikia muda huo. Sasa hii maana yake kwamba hatutaweza kuendelea na shughuli hii kufika hiyo sehemu iliyobaki. Kwa sababu ya muda ambao tumejifunga nao, muda wa saa moja na zimebakia dakika kumi kufikia ule muda tulipoanza shughuli hii.

Sasa nadhani kazi hii haitoweza kumalizika hapa inaingia ile hoja aliyotoa Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa na kwamba inachukua uzito wake. Tumejifunga tayari maana kwamba tungelisema mpaka shughuli hii imalizike ingekuwa swali jengine, na pengine itatukumbusha kwamba tusitoe hizi kasma ndogo ndogo tuende mpaka tumalize shughuli yetu. Tuakhirishe Baraza.

(Baraza lilirudia)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe baada ya makubaliano ambayo tumeyajenga sasa niakhirishe kikao hichi hadi kesho tarehe 27/06/2013 saa 3.00 barabara za asubuhi. Kama tulivyokubaliana pale asubuhi tutakwenda na *Order paper* yetu ya kawaida maswali na majibu, tutamuomba Mhe. Waziri awasilishe muda ukiwepo Mwenyekiti wa Kamati atatoa hotuba yake. Baada ya hapo tutaona kama ni muda muafaka kuweza kufanya shughuli tuliyoibakisha. Tuje kesho saa 3.00 barabara asubuhi.

(Saa 2:30 usiku Baraza liliakhirishwa hadi tarehe 27/6/2013 saa 3:00 asubuhi)